Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Sita - Tarehe 10 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza shughuli zetu za kawaida naomba kutambulisha wageni waliopo katika *Gallery* ya Bunge hii leo.

*Honourable Members, I wish to recognize the presence in the gallery of the Honourable Members of the East African Legislative Assembly. You are most welcome into the Gallery of Parliament. (Applause)*

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report and Audited Accounts for the Commission for Human Rights and Good Governance for the Year 2001/2002).*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:**

Taarifa ya Kumi na Saba ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Seventeenth Annual Report and Accounts of the Cooperative Audit and Supervision Corporation for the Year ended 30th June, 2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 75

### Kushindwa Kufikiwa kwa Malengo ya Halmashauri

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri za Wilaya na Manispaa ndizo pekee zenye dhamana ya kuendesha na kusimamia maendeleo ya wananchi katika Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya zao na kwa kuwa mpaka sasa 90% ya Halmashauri zetu zimeshindwa kufikia malengo yaliyowekwa katika Wilaya na Mikoa yao:-

(a) Je, ni nini wajibu wa kisheria kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa katika kudhibiti malengo hayo ya Halmashauri na Manispaa katika Wilaya/Mkoa wake?

(b) Je, ni nini wajibu wa kisheria wa Halmashauri au Manispaa inayoshindwa kufikia malengo yaliyowekwa?

(c) Je, ni nini wajibu wa kisheria kwa Bunge linapobaini kuwa Halmashauri au Manispaa zimezembea katika kufikia malengo yake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo hazifikii malengo yaliyowekwa kutokana na sababu mbalimbali. Hivyo, jukumu la kwanza la kuhakikisha kwamba malengo ya mwaka yanafikiwa ni la Halmashauri yenyewe wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao ni Madiwani katika Halmashauri zao. Kwa upande wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wao kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya Mwaka 1997, wamepewa jukumu la kuziwezesha na kuzisaidia Halmashauri kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuweka mazingira yatakayoleta ufanisi wa Halmashauri na kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatekeleza majukumu yake ya kisheria. Aidha, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni Wenyeviti wa Kamati za Ushauri zilizoundwa kisheria katika maeneo yao. Moja ya majukumu ya Kamati hizi ni kujadili na kushauri kuhusu mipango ya maendeleo na utekelezaji wake.

(b) Mheshimiwa Spika, wajibu wa kisheria wa Halmashauri ni kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na kutoa huduma kwa wananchi. Inapotokea kwamba malengo hayakufikiwa, ni jukumu la Halmashauri yenyewe, viongozi wake wa Wilaya pamoja na wadau katika maendeleo kusaidia kutatua kasoro zilizojitokeza ili kufanikisha malengo ya Halmashauri. Hakuna Sheria yoyote ya Bunge au Sheria Ndogo inayotoa adhabu kwa Halmashauri iliyoshindwa kufikia malengo yake isipokuwa pale itakapobainika kuwa utekelezaji ulikwamishwa na mtu mmoja basi mhusika atachukuliwa hatua za nidhamu au kisheria kwa kushindwa kutekeleza wajibu aliopatiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Bunge kupitia taratibu zilizowekwa kisheria linao wajibu wa kushauri juu ya utendaji wa Halmashauri yoyote nchini. Taratibu hizi ni pamoja na Bunge kuwa na fursa ya kujadili makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia taarifa za hesabu za Halmashauri pamoja na kutembelea miradi yao na Kamati ya Sheria, Utawala na Katiba kupata fursa ya kuchambua na kushauri juu ya makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa pamoja na Halmashauri. Mara kwa mara Ofisi yetu imenufaika sana na ushauri unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge kupitia vikao vya Kamati nilizozielezea na Bunge lenyewe.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya ufasaha ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kisheria mwajiriwa hudhibitiwa na mwajiri wake. Je, ni lini Serikali itatoa mamlaka ya kuajiri Watendaji Wakuu wa Halmashauri?

Pili, kwa kuwa Wakurugenzi wengi wameshindwa majukumu yao katika Halmashauri na badala yake wamekuwa wakihamishwa hamishwa, je, ni lini Serikali itaacha utaratibu huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwajiriwa anadhibitiwa na yule anayemwajiri na katika mazingira yetu ya Halmashauri zote hapa nchini mfumo ambao sasa ndiyo tunakwenda nao ndiko tunakoelekea. Kama unavyojua *reforms* zinazoendelea sasa ndiyo zimeanza hasa huu utaratibu wa kuwaweka Watendaji Wakuu hawa chini ya mfumo wa ajira za Halmashauri zenyewe. Tulilazimika kuchukua muda kidogo kwa sababu inahitaji maandalizi ili wote tuweze kuelewa namna tutakavyokuwa tunatekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, si kweli kwamba, mara zote Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anapomhamisha Mkurugenzi ni kwa sababu ameshindwa kutekeleza majukumu yake. Uhamisho mwingi kabisa unatokana tu na umuhimu wa kubadili mazingira kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine hasa inapotokea kwamba mtu amekaa muda mrefu kama miaka saba, nane, tisa na mwisho anazoea mazingira. *(Makofi)*

**MHE. BENARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Ninalo tatizo kwa Mkuu wa Wilaya. Tukiangalia hali inayojitokeza ni kwamba, Mkuu wa Wilaya hana kazi anakuwa *redundant.* Je, Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kuangalia upya kazi ya Mkuu wa Wilaya ambaye kwa kweli hayupo hata kwenye Kamati ya Ushauri ya Wilaya kama tulivyoelezwa na hahudhurii hata vile vikao vya Halmashauri, upo uwezekano wa kukaa na kuangalia upya na kuoanisha kazi mpya za Mkuu wa Wilaya ili asiwe *redundant?*

**SPIKA:** Naona ni swali jipya, nafikiri Waziri anahitaji kujiandaa kutoa majibu mazuri ya swali lako.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa kuniona. Kwa kuwa kwa kipindi kirefu pamekuwepo na mvutano mkubwa kati ya Halmashauri na Serikali Kuu yaani Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kuhusu vyanzo vya mapato, pamoja na kwamba Serikali sasa inatoa ruzuku lakini vyanzo vikuu vya mapato ya Halmashauri bado vipo Serikalini. Je, ni lini Serikali itaendelea ku-*review* ili vyanzo vya mapato vya Halmashauri viongezwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sina hakika sana kwamba huu tuite mvutano mkubwa kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, nadhani jambo ambalo limekuwa linafanyika ni mazungumzo ya kawaida kati ya taasisi hizi mbili katika kujaribu kufikia kitu ambacho kinaweza kikatoa nafuu kwa pande zote mbili. Tulishawahi kulieleza Bunge lako Tukufu hapa kwamba zoezi la kuainisha vyanzo hivi limekwishakamilishwa chini ya utaratibu wa *Consultant* na mchanganuo wa taarifa hiyo ya mtaalam unaendelea kufanyika na mara zoezi hilo litakapokamilika tuna hakika kabisa tunaweza kuja kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya nini tumeweza kufikia kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika suala hili la vyanzo vya mapato.

Na. 76

**Kuondolewa kwa Madiwani Kwenye Bodi ya Zabuni**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imewaondoa Waheshimiwa Madiwani kwenye Bodi ya Zabuni za Halmashauri jambo linaloweza kuwafanya watendaji kutoa tenda kwa upendeleo na kupunguza madaraka ya Madiwani:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba uwakilishi wa usimamizi wa mali za Halmashauri/wananchi kwa utaratibu huo sio mzuri?

(b) Je, maana ya uwakilishi itakuwa wapi tena kama tunavyofahamu zabuni hutolewa kwa upendeleo au wakati mwingine watendaji kudai chochote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali iliwaondoa Waheshimiwa Madiwani kwenye Bodi za Zabuni za Halmashauri. Msingi wa kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi za Zabuni za Halmashauri ni kanuni zilizopitishwa zinazozingatia matakwa ya Kifungu cha 14(1) cha Sheria

Na. 3 ya Mwaka 2001 inayohusu kuundwa kwa Bodi za Tenda za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa, kazi za ujenzi na utoaji wa huduma ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha. Chini ya kifungu hicho, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zitaunda Bodi za Tenda chini ya Afisa Mhasibu kufuatana na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982. Bodi ya Zabuni ni chombo kinachotekeleza maamuzi ya Baraza la Madiwani ambayo yameidhinishwa katika mpango wa bajeti husika. Utaratibu uliomo katika kanuni mpya umezingatia *checks and balances* tangu zabuni inapotangazwa, inapofanyiwa uchambuzi wa kitaalam, inapojadiliwa na Bodi na uamuzi kutolewa hadi kufunga Mkataba. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kama Waheshimiwa Madiwani watatimiza wajibu wao kikamilifu, usimamizi wa mali za Halmashauri au wananchi utakuta hauna matatizo ya kutekelezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Watendaji wote wanafanya kazi kwa kutimiza wajibu wao kwa niaba ya Halmashauri na wakazi wake. Watendaji wanapaswa kuhakikisha kwamba, utoaji wa zabuni unafuata sheria, kanuni na taratibu zote zilizopo. Suala la Watendaji kutoa upendeleo au wakati mwingine kudai chochote halina sababu ya kuwepo iwapo kila Diwani atatimiza wajibu wake wa kusimamia Watendaji na pale itakapobainika kwamba vitendo vya rushwa na upendeleo vitajitokeza basi sheria zilizopo zitachukua mkondo wake dhidi ya wahusika.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali waliogopa kwamba Madiwani hawakuwa wakitekeleza wajibu wao au kutoa tenda kwa upendeleo na kwa kuwa watendaji wa Halmashauri ndiyo wanasimamia tenda, wanatoa tenda na kwa sasa hali ni mbaya zaidi ya wakati ule. Je, Serikali itafanya utaratibu gani wa kuwadhibiti hawa Watendaji kwa kutoa upendeleo kwao?

Pili, kwa kuwa Watendaji hawawapi Madiwani fedha za kwenda kuangalia miradi hasa wakijua kwamba kazi imefanyika chini ya kiwango. Je, Serikali itachukua utaratibu gani wa kuhakikisha miradi ya wananchi inatekelezwa ipasavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisisitize kwamba, utaratibu huu haukuanzishwa kwa sababu Madiwani walionekana wanafanya upendeleo au kutoa rushwa hata kidogo. Tunachokisema hapa ni msingi wa namna ya kutenda shughuli za Halmashauri. Madiwani ndiyo wasimamizi wa shughuli zote katika Halmashauri zetu na ndiyo maana ikaonekana ni busara na kwa kweli ni *logic* kwamba ili waweze kufanya kazi vizuri ni vizuri Watendaji wakawa ndiyo wenye majukumu fulani fulani ili Madiwani waweze kupata nafasi ya kuwahoji, kuwauliza na kusimamia shughuli kwa ujumla. Kwa hali ilivyokuwa sasa, Madiwani wanapokuwa ni wao wenyewe ndiyo watoa zabuni, inakuwa ni vigumu kusema nani sasa atamwuliza nani endapo kutakuwa na matatizo. Huo ndiyo hasa ulikuwa msingi mkubwa wa jambo hili. Lakini naomba niseme vile vile kwamba, si kweli kwamba, hali ni mbaya kuliko ilivyokuwa zamani. Ningependa sana Mheshimiwa Laizer kama angeweza kuja na *statistic figure* ya jambo hili, nina hakika ningeweza pengine kuliafiki. Kwa hali ilivyo sasa utendaji unaonekana unaanza kuimarika na tuna uhakika baada ya muda mrefu mtaona ninyi wenyewe kwamba ni jambo jema ambalo Serikali ilifanya.

Lakini la pili, kwamba Serikali haitoi fedha au Halmashauri haitoi fedha kwa Madiwani kwa ajili ya kwenda kutembelea miradi. Nadhani jambo hili ni *internal affair* kwa kila Halmashauri, sidhani kama Halmashauri yenye busara inaweza ikakataa kuisaidia Kamati ya Fedha au Kamati nyingine yoyote kwenda kutembelea miradi na suala si fedha kwa kweli, suala ni utaratibu wa kuwawezesha kwenda kutathmini miradi, kwa hiyo inaweza kuwa ni *transport* au njia nyingine yoyote, lakini si lazima zikawa fedha. *(Makofi)*

Na. 77

**Kusaidia Mikoa Iliyo Nyuma Kimaendeleo**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuisaidia Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo na inayokabiliwa na umaskini uliokithiri ikiwemo Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Rukwa, Tabora na kadhalika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba, Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Rukwa na Tabora, iko nyuma kimaendeleo na inakabiliwa na umaskini uliokithiri kama ilivyothibitishwa na kuripotiwa katika taarifa ya utafiti wa hali ya matumizi na mapato ya kaya ya mwaka 2000/2001.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya maendeleo inayopangwa na kutekelezwa na Serikali huelekezwa kwa nchi nzima, kama vile miradi ya elimu, afya, barabara na kadhalika. Zaidi ya hayo Serikali imekuwa ikihamasisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs),* sekta binafsi na wahisani wengine kwenda katika Mikoa iliyo nyuma ili wasaidiane na wananchi wa Mikoa hiyo kwa kupitia Serikali za Mitaa na vikundi vilivyoanzishwa na wananchi *(CBOs),* kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekuwa ikihimiza Serikali za Mitaa, kuamsha ari ya maendeleo kwa wananchi wa maeneo hayo. Katika Mikoa tajwa, Serikali imepeleka Mradi wa *TASAF* katika Wilaya za Shinyanga Vijijini, Bariadi na Meatu (kwa Mkoa wa Shinyanga) Tabora Vijijini, Sikonge na Urambo (kwa Mkoa wa Tabora), Kigoma Vijijini, Kasulu na Kibondo (kwa Mkoa wa Kigoma) na Wilaya za Sumbawanga na Nkasi (kwa Mkoa wa Rukwa).

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge na viongozi wengine, wafikishe wito huu wa Serikali wa kutaka wananchi wajitolee ili wadau wengine washawishike kuunga mkono jitihada za Serikali za kuleta maendeleo kwenye Mikoa hiyo.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, nina swali moja la nyongeza. Pamoja na maelezo ambayo ameyasema atakubaliana na mimi kwamba Mikoa hii ipo nyuma kimaendeleo kutokana na mgawanyo mbaya wa mapato ya Serikali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, hii si mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Makolo kudai kwamba mgawo wa raslimali katika Mikoa iliyo nyuma siyo mzuri. Wakati wa Bajeti ya mwaka 2003 na wakati wa semina iliyohusu vyombo vya fedha, jambo hili alilisema na mimi nilitoa maelezo kwamba kadri ninavyoelewa, Serikali inajitahidi kupeleka raslimali katika maeneo mbalimbali hasa kwa kuzingatia maelekezo ya mkakati wa kuondoa umaskini ambao umebainisha maeneo gani yapo nyuma kuzidi mengine na ni matumaini yangu kwamba, tutaendelea kulifanyia kazi hilo na Waziri wa Fedha yupo na Mawaziri wenzangu wapo hapa.

La pili, si suala la raslimali peke yake katika kuondoa umaskini. Kuna suala la kufanya kazi vile vile kwa bidii kwa mpangilio maalum, pamoja na kupeleka fedha lakini tupime vile vile umaskini upo wa aina mbalimbali, kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga ukichukua asilimia ya watu walio chini ya kiwango cha umaskini wa chakula ni 22%. Kwa maana hiyo wamepiga hatua kubwa na ya kupongezwa katika kujiondoa na umaskini wa chakula tunaoita *food poverty*. Kwa hiyo, katika eneo hili wamefanya vizuri. Kigoma 21%, Rukwa 12%, Tabora 9%, ndiyo kusema wameondokana na umaskini wa chakula kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, asilimia ya kaya zinazotegemea kilimo kwa maana ya kwamba huwezi kuondokana na umaskini bila kutegemea kilimo. Shinyanga wanategemea kilimo kwa asilimia 68, kwa hiyo nguvu za raslimali ni lazima ziongezwe eneo hilo la kilimo kwa sababu wamepiga hatua kubwa. Kigoma asilimia 76, Rukwa asilimia 76 pia na kwa hiyo raslimali lazima zikitolewa zipelekwe katika maeneo yale ambayo wananchi wenyewe wanatumia nguvu zao kujiondoa katika umaskini. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya upendeleo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa imedhihirika kwamba Mkoa wa Kigoma haujawahi kupatwa na baa la njaa na kwa kuwa tunayo mabonde mengi mazuri yenye rutuba na kwa kuwa tuna uwezo wa kuzalisha chakula cha kutosheleza nchi nzima. Je, Serikali itakuwa tayari kutujengea daraja katika Mto Malagarasi kusudi tuweze kusafirisha chakula kwa Watanzania wote? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hilo linahusu Wizara ya Ujenzi, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi ajibu swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali siyo itajenga daraja la Mto Malagarasi, Serikali imekwishajenga madaraja katika Mto Malagarasi na sasa hivi Mto huo unavukika. Kwa hiyo ni jitihada ya wananchi wa Kigoma kulitumia daraja lile kujiondolea umaskini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, baada ya kuwatambulisha Waheshimiwa Wabunge 24 wa Bunge la Afrika Mashariki walioko kwenye *gallery* waliingia wageni wengine ambao vile vile ni vizuri niwatambulishe. *I wish to recognize the presence in the gallery of the Dr. Andrew Pacol, The British High Commissioner and Members of his staff. You are most welcome into the Gallery of Parliament.*

Na. 78

**Uwanja wa Ndege Bukoba**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetamka mara nyingi nia yake ya kupanua Uwanja wa Ndege wa Bukoba Mjini kwa kuuwekea uzio, kuimarisha *runways* kwa lami na hatimaye kujenga uwanja mpya:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza mpango huo?

(b) Kwa kuwa Kiwanda cha Minofu ya Samaki kinajengwa kwenye maeneo ya *Kemondo Bay* na kwamba bidhaa za kiwanda hicho zitahitaji kusafirishwa kwa ndege kubwa kutoka Bukoba kwenda Mwanza au nje ya nchi kama Entebbe. Je, Serikali haioni kwamba kama mpango wa kuupanua uwanja huo haukutekelezwa haraka, upo uwezekano mkubwa kwa ndege kubwa kushindwa kutua katika uwanja wa sasa na hivyo kufanya usafirishaji wa bidhaa za kiwanda hicho kuwa mgumu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba, Serikali ina mpango wa kupanua Kiwanja cha Ndege cha Bukoba Mjini kwa kukijengea uzio, kuimarisha barabara ya kutua na kurukia ndege *(runway)* na hatimaye kujenga kiwanja kipya cha ndege. Katika kutekeleza mpango huo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imejenga uzio wa meta 172 upande wa jengo la abiria *(Terminal Area),* ikiwa ni awamu ya kwanza. Mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi milioni 35 kukamilisha awamu ya mwisho ya ujenzi wa uzio kuzunguka Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Uimarishaji wa barabara ya ndege *(runway),* umefanyika mwaka huu wa fedha kwa kukarabati sehemu korofi na kuongeza urefu wa njia ya kurukia ndege toka meta 1,220 hadi 1,280. Urefu huu utawezesha ndege aina ya *LET 410* kuweza kutua au kutumia kiwanja hicho kwa usalama zaidi. Sambamba na upanuzi huo, maegesho ya ndege *(apron),* yamefanyiwa upanuzi kuwezesha kupokea ndege tatu za aina hiyo kwa wakati mmoja. Uimarishaji wa *runway* kwa kiwango cha lami utafanyika kadri mahitaji ya ukuaji na ongezeko la ndege na abiria utakavyokua na utategemea upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshafanya upembuzi yakinifu na kubaini kuwa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba Mjini hakitakidhi mahitaji ya kuhudumia ndege kubwa kutokana na eneo kilipo kuwa na vikwazo vya kuwezesha ndege kubwa kutua kwa usalama kama vile kimezungukwa na makazi ya watu, miamba iliyoko usawa wa kutua na kuruka ndege *(Approach Surfaces).* Hivyo, imependekezwa kuwa kiwanja kipya kijengwe eneo la Omukajunguti, kilomita 41 kutoka Bukoba Mjini, mara fedha zitakapopatikana. Kwa kuwa upembuzi yakinifu ulizingatia tunachoita *economic and financial viability* ya Mkoa mzima wa Kagera, imependekezwa kuwa kiwanja kiwe cha daraja la aina ya *3C* chenye uwezo wa kuhudumia ndege za ukubwa wa wastani wa kati za *F50* na *DASH 8.*

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kutembelea eneo la Omukajunguti tarehe 26 Februari, 2002 nikiongozana na Mheshimiwa Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge na Viongozi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ndicho kinachotumika kupokea ndege kubwa za mizigo kusafirisha minofu ya samaki kwenda nchi za nje, ni vema kiwanda kilichopo Bukoba kitakapokamilika, kisafirishe hizo bidhaa kwenda Mwanza kwa kutumia njia ya maji *(Water Transport),* kutokana na ukaribu uliopo kati ya Bukoba na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kuuliza swali hili anatukumbusha suala la msingi sana. Suala lenyewe ni umuhimu wa kuendeleza viwanja vyetu vya ndege, usafiri majini, barabara na reli, kwa uwiano kwani njia zote hizi zinashabihiana. Hivyo basi, ujenzi wa barabara kutoka Kyaka mpaka Muhutwe kwa kiwango cha lami unaufanya Mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Omukajunguti uwe muhimu zaidi na tunamshukuru.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, pamoja na kuwa swali hili limechangia kusaidia, Serikali inatumia vigezo gani katika kupanga mambo muhimu hasa miradi ya maendeleo hususan kama vile viwanja vya ndege?

(b) Mimi mwenyewe nimebahatika wiki tatu zilizopita kutembelea kiwanda cha minofu ya samaki na kukuta kimeanza kuzalisha tani 10 na hivi karibuni kitazalisha tani 30. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa haraka kabisa kuhakikisha kuwa hatuwezi kurudi nyuma katika kuathiri maendeleo ya nchi yetu na hasa uchumi wa nchi yetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kupanga umuhimu wa miradi, Serikali inatumia vigezo vingi. Kwa upande wa viwanja vya ndege pamoja na kile nilichokiita *Economic and Financial Vialibity* ya mradi wenyewe. Kwa maana hiyo, ndiyo tumeamua kwamba tutajenga Uwanja wa Ndege wa Omukajunguti kwa sababu unakidhi vigezo hivyo. Tumeamua hivyo kwa sababu ili kuweza kuwa na kiwanja cha kati, cha *medium size,* kwa sababu Kagera inazungukwa vilevile na viwanja vikubwa vya ndege naweza kusema vinne ambavyo viko karibu navyo ni Mwanza, Entebbe, Kigali na Bujumbura.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya Kiwanda cha Minofu cha Bukoba, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Janet Bina Kahama kwamba, Serikali itafanya kila njia kuhakikisha kwamba, kazi inayofanywa na zao linalopatikana kutokana na kiwanda hicho linauzwa haraka iwezekanavyo bila kiwanda kupata hasara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Katika kuweka uwiano baina ya Chama Tawala na Kambi ya Upinzani, sasa namwita Mheshimiwa *Wilfred Lwakatare. (Kicheko)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mji wa Bukoba umedhihirika kwamba unakuwa na abiria wengi wanaotumia uwanja huo wa ndege kiasi kwamba ndege kubwa zinazotoka Dar es Salaam kwenda Mwanza mara nyingi zinabeba abiria wanaokwenda Bukoba na kutoka Mwanza kwenda Bukoba abiria hao hutumia ndege ndogo ambayo kwa siku huruka zaidi ya mara 5 au 6. Sasa kwa kuwa jambo hili la uwanja wa ndege limekuwa la muda mrefu tangu miaka ya 1970

nikiwa ninasoma *Primary School* wakati huo, tulielezwa kwamba uwanja wa ndege utakuwa Kyetema na sasa tunaambiwa utakuwa Omukajunguti. Sasa hadithi hizi za tangu mwaka 1970 mpaka hivi sasa zitaisha lini ili tupate uwanja wa ndege na tutokane na adha ya kupanda ndege ndogo?

**SPIKA:** Anauliza ahadi hizi zitakwisha lini Mheshimiwa Waziri? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahadi kama jina lilivyo, haziwezi kwisha, tutaendelea kutoa ahadi na kuzitekeleza. Pili, kutokana na ukaribu wa kiwanja cha ndege cha Bukoba kutoka Mwanza, ambao ni chini ya kilomita 200 kwa mstari ulionyooka, basi kwa muda wa kati tutaendelea kutumia ndege ndogo ili kiwanja cha ndege cha Bukoba kiweze kufanya kazi kwa uwiano na kiwanja cha ndege cha Mwanza kwa sababu ya ukaribu huo. *(Makofi)*

Na. 79

**Usafiri wa Abiria *MS. SEPIDEH***

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa *MS. SEPIDEH* ulikuwa muhimu sana kwa wasafiri kati ya Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mombasa; na kwa kuwa usafiri huo ulikuwa ukiwasaidia sana wananchi ambao hawakuwa na uwezo wa kusafiri kwa ndege:-

(a) Je, chombo hicho cha usafiri kiliondolewa kwa sababu zipi na kiko wapi sasa?

(b) Je, chombo hicho kinatarajiwa kurejeshwa lini Tanzania na kama hakuna mpango wowote wa kukirejesha tena, je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta chombo kingine cha kutoa huduma kwenye sehemu nilizozitaja?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *MS. SEPIDEH* ilisajiliwa Kingstone Jamaica na ilikuwa inapepea *flag of convenience* ya Jamaica. *MS. SEPIDEH* ilipelekwa kwenye matengenezo makubwa *(Dry Dock)* Uarabuni Novemba, 2002 na mmiliki wa meli hiyo aliahidi kuwa baada ya matengenezo ya boti hiyo kukamilika angeirudisha nchini mapema Aprili, 2003 ili ifanye kazi ya kutoa huduma kati ya Dar es Salaam, Zanzibar na Tanga. Hadi sasa imepita zaidi ya mwaka mmoja tangu alipoahidi kuwa angerudisha boti hiyo nchini na bado haijafanya hivyo. Aidha, uhakika wa ilipo boti kwa sasa haupo kwani suala hili limefuatiliwa mara nyingi bila mafanikio yoyote na hasa kutokana na kutopatikana mawasiliano na mmiliki wa chombo hiki. Haya ndiyo matatizo ya *flag of convenience.*

Mmiliki wa mwisho wa *MS. SEPIDEH* wakati ikienda chelezo ilikuwa ni kampuni ya *Toil Mega Speed Linears*. Kampuni hii haipo tena, wafanyakazi wote wa kampuni hiyo wamekwishalipwa mafao yao wala kampuni haidaiwi na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa hatuna mawasiliano na mwenye chombo hicho, hatuwezi kujua mipango yake ya baadaye ya kukirudisha chombo hicho nchini.

Hata hivyo, Serikali inafahamu upungufu wa huduma ya usafiri uliopo kwenye maeneo hayo na hivyo tutaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji ili kuboresha utoaji wa huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika maeneo hayo na sehemu nyingine nchini.

Ni matumaini yangu kwamba, Asasi nyingine za Kiserikali kama vile *Zanzibar Investment Promotion Agency* na *the Tanzania Investment Centre* na zile za kibinafsi, zitasaidiana na Serikali kumpata mwekezaji atakayesaidia kuondoa tatizo la uchukuzi kwenye maeneo hayo na mengine nchini.

Ni sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kusaidia wawekezaji katika Sekta ya Uchukuzi hasa katika maeneo ambayo hayawavutii wawekezaji, lakini ni muhimu yapatiwe usafiri yaani *public service obligation.*

Na. 80

**Madhara ya Mamba kwa Wananchi wa Kyela**

**MHE. JONH L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mamba ni mnyama hatari kwa binadamu na ni miongoni mwa wanyama wanaolindwa na sheria mbalimbali za Kimataifa na kwamba ni Kosa la Jinai kumuua Mamba bila kibali cha Serikali:-

(a) Je, kuna faida gani ya kuwa na mnyama kama huyo kwa wananchi wa Kyela ambao mara kwa mara wamekuwa wakishambuliwa na mnyama huyo kwa kuwang'ata miguu au mikono na kuwasababishia vilema na wakati mwingine vifo wakati wanapokwenda mtoni kiasi cha kuwalinda kwa sheria ya Kimataifa?

(b) Kwa kuwa mito yote mikubwa Wilayani Kyela, yaani Mto Songwe, Kiwira, Mbaka na Lufilyo imekuwa na Mamba wengi sana na wananchi wa Kyela pamoja na mifugo yao wanaathirika kutokana na tatizo hilo, je, Serikali ina utaratibu gani wa kumfidia mtu aliyejeruhiwa na Mamba na kubakia kilema kwa mantiki kwamba wanyama hao ni mali ya Serikali na analindwa na sheria zake?

(c) Je, Serikali inaona ugumu gani kuvuna Mamba wanapokuwa wanazaliana kwa wingi kupita kiasi na kuwa kero kubwa kwa wananchi wa maeneo husika?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la mamba, nchi yetu iliwasilisha maombi ya kuongezewa mgao wa kuvuna mamba kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Biashara na Mimea na Wanyama walioko Hatarini kutoweka *(CITES)* na kukubaliwa kwenye Mkutano wa nchi wanachama *(Conforence of the Parties),* uliofanyika Gigiri, Kenya mwaka 2000. Mkutano huo ulikubali ombi la Tanzania kuongezewa mgao wa mamba. Tanzania iliruhusiwa kuvuna mamba 1,600 kwa mwaka. Katika mgao huo, mamba 100 ni kwa ajili ya uwindaji wa kitalii na 1,500 ni kwa ajili ya uwindaji wenye lengo la kudhibiti tatizo la mamba wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na mamba kusababisha usumbufu mbalimbali kwa maisha na mali za wananchi, mnyama huyo ana faida kubwa Kitaifa na Kimataifa kwa kuwa ni moja ya vivutio vya utalii. Mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kama vile ada za uvunaji wa mamba yanaingia katika Mfuko wa Serikali ambapo fedha hizo hutumiwa na Serikali kugharimia shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii nchini zikiwemo zile za wananchi wa Wilaya ya Kyela. Kwa mfano, kati ya mwaka 2000 hadi 2002, Serikali ilijipatia jumla ya shilingi 145,280,000/= kutokana na uvunaji wa mamba 3,632 waliowindwa na watalii pamoja na kampuni mbalimbali zinazoendesha biashara ya nyara.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 hairuhusu Serikali kulipa fidia kwa madhara yatokanayo na wanyama wakali na waharibifu wakiwemo mamba. Vilevile wananchi wanaruhusiwa kuwaua mamba wanapoleta madhara kwa utaratibu maalum unaokubalika kisheria na kwa kuwatumia Maafisa na Askari Wanyamapori walioko karibu na maeneo husika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haioni ugumu kuvuna mamba wanapozaliana kwa wingi kupita kiasi na kuwa kero kwa wananchi ndiyo maana Serikali imeongeza mgao wa uvunaji wa mamba hasa katika maeneo yenye tatizo la mamba wakali na waharibifu.

Aidha, Serikali inatoa mgao wa mamba 1,500 kila mwaka kwa Kampuni binafsi zinazomilikiwa na wananchi ili zisaidie kuwinda mamba wanaosababisha kero kwa wananchi. Kwa kuzingatia hoja ya Mheshimiwa Mwakipesile, baadhi ya Kampuni zitakazochaguliwa kuwinda mamba mwaka huu 2004 zitapewa kibali cha kwenda kuwinda mamba kwenye mito ya Songwe, Kiwira na Lufilyo Wilayani Kyela ili kudhibiti madhara ya mamba kwa wananchi wa Wilaya hiyo.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa katika Ziwa Rukwa mamba ni wengi, nadhani kuliko Maziwa mengine yote katika nchi hii. Je, Makampuni hayo yatasaidia vilevile kadri watakavyovuna huko Kyela watavuna kwenye Ziwa Rukwa ili wananchi wangu waweze kuishi kwa usalama maana wengi wameng'atwa miguu na mikono?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama ninakumbuka vizuri ni kwamba, mwaka 2003 kulikuwa na tatizo kubwa la mamba katika Ziwa Rukwa na baadhi ya makampuni yalikwenda kuwinda katika Ziwa Rukwa.

**SPIKA:** Mamba wa Ukerewe, Mheshimiwa Getrude Mongella. *(Kicheko)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, aliniona nilikuwa nimesimama lakini kwa sababu ya kimo changu hakuniona vizuri. Nashukuru kaniona. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Mamba hawa pamoja na kwamba katika Kisiwa cha Ukala tuna utaalamu wa kuwafuga, lakini wanaongezeka kwa kasi kubwa ya kuhatarisha maisha ya watu. Je, Waziri anaweza kuzingatia utaalamu huu wa Kisiwa cha Ukala ili aweze kusaidia zaidi katika maeneo mengine na papo hapo atusaidie ongezeko kubwa la viboko ambao sasa wanakula watu katika Wilaya ya Ukerewe? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tutazingatia na ningependa nionane na Mheshimiwa Mama Getrude Mongella tuzungumzie suala hili. *(Makofi)*

Na. 81

**Ujenzi wa Soko la Kisasa Kizingo**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Japan kwa muda mrefu imekuwa na mpango kamambe wa kujenga Soko la Kisasa la Samaki huko Kizingo Kikwajuni.

Je, mpango huo bado upo na kama upo umefikia hatua gani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Japan imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia nchi yetu katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ile inayohusu

Sekta ya Uvuvi. Moja ya miradi hiyo ni ule mradi wa Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi *(Fisheries Development Master Plan Programme),* uliokamilika Juni, 2002 . Chini ya mpango huo maeneo15 yalitambuliwa na kupewa kipaumbele ili kuendeleza Sekta ya Uvuvi. Moja ya maeneo hayo ni ujenzi wa Soko la Kisasa la Kirumba, Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi ambayo yaliwasilishwa kwa Serikali ya Japan ni kwa ajili ya msaada wa ujenzi wa Soko la Samaki la Kirumba Mwanza na Kilimani, Zanzibar. Hata hivyo, Serikai ya Japan ilikubali maombi ya ujenzi wa Soko la Kirumba Mwanza ambapo mpaka sasa maandalizi ya awali ya kutekeleza mradi huo yamekwishafanyika na mapendekezo yake kuwasilishwa kwa Serikali ya Japan. Ikiwa Bunge la Japan litaridhia, mradi wa ujenzi wa Soko la Samaki la Kirumba utaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maombi ya ujenzi wa Soko la Kilimani yameshawasilishwa kwa Serikali ya Japan, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zitaendelea kufuatilia matokeo ya maombi hayo kupitia Wizara husika. *(Makofi)*

Na. 82

**Matatizo ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ina idadi kubwa ya wanafunzi, Walimu na jamii ya shule kwa kiasi ambacho idadi yao inafikia zaidi ya 600; na kwa kuwa Chuo cha Ualimu Bustani nacho idadi yao ni zaidi ya 300 na kwa pamoja shule hiyo na Chuo hicho vina magari ambayo ni mabovu; na kwa kuwa wanafunzi na wanachuo wa Taasisi hizo hupata shida sana itokeapo dharura ya wagonjwa ambao hulazimika kubebwa na wenzao kufikishwa hadi hospitalini:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kutengeneza magari hayo ili yatumike kuondoa matatizo hayo?

(b) Je, kwa nini Serikali hupendelea kulimbikiza matatizo badala ya kuchukua hatua za haraka kuyaondoa ili kuboresha hali ya Vyuo na shule hizo za sekondari?

(c) Je, upungufu wa walimu uliopo katika shule za sekondari ya wasichana Kondoa, Kwapakacha, Bereko, Pahi na Intella ni kiasi gani kwa kila shule na hatua zilizochukuliwa kuondoa tatizo hilo ni zipi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara inalitambua tatizo la usafiri kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa na Chuo cha Ualimu cha Bustani. Katika kushughulikia tatizo hilo, Desemba, 2002, Wizara iliipatia shule ya Sekondari ya Kondoa shilingi milioni nne kwa ajili ya matengenezo ya gari la shule. Hata leo asubuhi tumewasiliana na *Headmaster* wa shule hiyo, lori la shule hiyo aina ya Tata linafanya kazi. Aidha, Wizara imekipatia Chuo cha Ualimu cha Bustani gari jipya katika mwaka huu wa fedha. Wizara inaendelea kuyahudumia magari hayo kwa kuyapatia mafuta na kuyafanyia matengenezo ya utunzaji.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, nia ya Serikali ni kutatua matatizo ya wananchi mara tu yanapojitokeza na siyo kuyalimbikiza. Lakini wakati mwingine inashindikana kufanya hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, hali ya walimu katika Shule za Sekondari za Kondoa, Kwapakacha, Bereko, Pahi, Intella na Mando ni kama ifuatavyo: Jumla ya walimu wanaohitajika katika shule hizo ni

118. Mwaka 2001 shule hizo zilikuwa na jumla ya walimu 63 na upungufu ulikuwa walimu 55. Mwaka 2002/2003 na mwaka 2003/2004 wamepangwa katika shule hizo jumla ya walimu 36. Kwa hiyo, pengo limepungua kutoka 55 hadi 12 na tunaendelea na juhudi ya kuajiri walimu mpaka wawepo walimu wa kutosha.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa majibu mazuri katika swali langu la msingi.

(a) Kwa kuwa tatizo kubwa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa ni maji na makisio yaliyofanyika ili kutatua tatizo hili la maji ni kununua pampu kupeleka katika shule hiyo ni kama shilingi milioni 8 hivi. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuchangia hivyo ili tuondoe tatizo hili la maji katika shule hii yenye wanafunzi wasiopungua 600?

(b) Kwa kuwa walimu wapya wanaoajiriwa wanakaa mwaka mzima na miezi hata 6 bila kupata mishahara na kadhalika. Je, Serikali inaweza ikaeleza nini tatizo na watalitatua tatizo hili lini ili walimu wawe wanapata mishahara kwa haraka iwezekanavyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la maji, namshukuru kwa kunitaarifu. Ni jambo ambalo tunahitaji tushirikiane na wenzetu wa Idara ya Maji kupitia Wizara yao. Lakini tutaliangalia tatizo hili lina ukubwa kiasi gani kwa sababu pengine tunaweza tukapata mafungu tutakapokuwa tumejua kwa usahihi makisio ya kufikisha maji katika shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa. Nakubaliana naye kwamba, maji ni mahitaji muhimu sana katika shule ya sekondari hasa inapokuwa ya bweni na ina wanafunzi wengi kiasi cha wanafunzi 600.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, mishahara ya walimu kuchelewa, tunajaribu kuondoa tatizo hili kwa kuhakikisha kwamba, walimu wapya wanaoajiriwa wanajaza fomu zao zote zinazohitajika mapema. Jambo hili linapotokea kuchelewa wakati mwingine siyo Wizara au Hazina wanaochelewesha, isipokuwa ni *particulars* fulani fulani zinazotakiwa zijazwe pale wanaporipoti kazini. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa wasimamiaji wa maeneo hayo hasa *Headmasters* wa shule zetu kwamba, mara walimu wanaporipoti pale, wakamilishe taarifa zote zinazohitajika ili waweze kuingizwa katika orodha ya watumishi wa Serikali na wawemo katika orodha ya mishahara.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kama ifuatavyo: Wilaya ya Kondoa ni mojawapo ya Wilaya ambazo zinao Mradi wa Benki ya Dunia wa Maji na mradi huo wameanza kuutekeleza mwaka huu. Namshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na viongozi wenzake katika Wilaya, waliweke jambo hili katika mojawapo ya vipaumbele vya Wilaya yao. *(Makofi)*

Na. 83

**Shule za Sekondari za Serikali Jimboni Mkinga**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Mkinga halina shule ya Sekondari ya Serikali hata moja; na kwa kuwa hata zile za wananchi zilizopo yaani Maramba, Lanzoni, Zingibari na inayoendelea kujengwa Kata ya Kigongoi zina ukosefu wa mabweni, maabara, vitendea kazi muhimu, nyumba za walimu na upungufu wa walimu; na kwa kuwa mpango wa kuboresha Elimu ya Msingi *(PEDP)* unatarajiwa kutoa mafanikio mema na hasa idadi kubwa zaidi ya wanaofaulu vizuri darasa la saba:-

( a) Je, huu si wakati muafaka kwa Serikali kujenga angalau Shule za Sekondari mbili Jimboni Mkinga?

(b) Je, Serikali isingefikiria kuzijumuisha Shule za Sekondari za wananchi za Maramba, Zingibari, Lanzoni na Kigongoi miongoni mwa shule ambazo zitafaidika chini ya

Mpango wa Maendeleo wa Shule za Sekondari ambao naamini utaanzishwa hivi karibuni?

(c) Je, ni misaada ya namna gani ambayo Serikali inaweza kutoa kwa wananchi wenye azma ya kujenga au kuendeleza Shule za Sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona ni busara zaidi kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Mkinga kuziboresha na kuzipanua shule nne za sekondari za wananchi zilizopo Jimboni Mkinga ambazo kwa sasa zina upungufu mkubwa wa mabweni , maabara, nyumba za walimu na vitendea kazi muhimu badala ya kujenga shule nyingine mpya. Shule hizo zikiimarishwa na zikaweza kuongeza wanafunzi hadi mikondo minne, yenye wanafunzi 40 kila mkondo, zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 640 wa Kidato cha kwanza kila mwaka. Kwa hiyo, jumla zinaweza kuwa wanafunzi 2,560 yaani 640 x 4 kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne 2,560.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 - 2009 wa miaka 5 unaotarajiwa kuanza kutekelezwa baadaye mwaka huu. Mpango huu utakapoanza kutekelezwa, shule zote za sekondari zilizopo pamoja na hizo za Maramba, Zingibari, Lanzoni na Kigongoi, zitanufaika katika maeneo mbalimbali ya taaluma na huduma muhimu kama vile kupewa ruzuku ya uendeshaji wa shule ili kuondoa kabisa uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa hutoa msaada wa utaalamu wa ramani za majengo, huduma za ukaguzi, huduma ya usajili wa shule na huduma ya mitihani yake Kitaifa. Aidha, Serikali ikiombwa huzipokea shule hizo ziwe za Serikali kama vile ambavyo imekwishazipokea shule za Zingibari, Lanzoni na Maramba na zikifikia hatua hiyo, Serikali hubeba gharama zote za uendeshaji wa shule. Katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004 - 2009 utakaonza kutekelezwa baadaye mwaka huu, inatarajiwa Serikali itakuwa inatoa kwa wanaojenga shule za sekondari, ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya uendeshaji wa shule kama vile zinavyotolewa katika ngazi ya elimu ya msingi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawilli ya nyongeza.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, wananchi wetu katika Jimbo la Mkinga wamehamasika sana na wanatarajia kujenga shule za sekondari karibu kila Kata kama wanavyohimizwa. Je, kwa msingi huu Serikali itakuwa tayari kusaidia vipi?

(b) Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba Wilaya ya Muheza ni moja ya Wilaya ambayo ilichangia sana katika kutoa walimu na wataalamu wengine mbalimbali katika nchi hii katika wakati wa ukoloni na hata baada ya uhuru kwa miaka mingi iliyoendelea, lakini kwa bahati mbaya Serikali iliitelekeza kabisa Wilaya ya Muheza na mpaka leo hakuna hata shule moja ya sekondari ya Serikali. Je, kwa msingi huu Serikali haiwezi kutoa kipaumbele maalum?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kusikia kwamba katika Wilaya ya Muheza wameazimia kujenga shule za sekondari katika kila Kata. Sasa Serikali tutasaidiaje? Kama nilivyosema katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, tunataka kufikisha uwezo katika nchi yetu wa kupeleka angalau asilimia 50 ya watoto wetu wanaomaliza darasa la saba katika shule za sekondari. Kwa hiyo, ni dhahiri kila shule inayojengwa na wananchi kwa lengo hilo la kuiwezesha Wilaya au Kata ifikie lengo hilo wataweza kupata ile ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya uendeshaji. Kwa hiyo, nawaomba waendelee kwa juhudi zote na mipango hiyo. *(Makofi)*

Kuhusu mchango wa Wilaya ya Muheza katika elimu miaka iliyopita, napenda nikubaliane naye kabisa kwamba, ni kweli miongoni mwa Wilaya zilizotoa walimu wa kwanza Wilaya ya Muheza imo. Mimi mwenyewe wakati nikisoma katika shule ya Sekondari kule Malangali, *Headmaster* wetu Mwalimu George Mgondo, alikuwa anatoka katika Wilaya ya Muheza. Mpaka hivi sasa ni mwalimu mstaafu anayeishi nje kidogo tu ya Wilaya ya Muheza na nilipoteuliwa kuwa Waziri aliniandikia barua kupitia kwa Mbunge wake ya kunipongeza kwamba mwanafunzi wake nimekuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Kwa hiyo, analosema Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ni la kweli kabisa na mimi mwenyewe nimewaona walimu hao. Lakini napenda ieleweke kwamba, Wilaya ya Muheza siyo kwamba haina shule za sekondari za Serikali, hizi shule za Zingibari, Lanzoni na Maramba, ambazo zimejengwa na wananchi sasa hivi zimekabidhiwa zinaendeshwa na Serikali, kwa hiyo Serikali inabeba gharama zote. *(Makofi)*

Lakini napenda nimfahamishe pia kwamba, katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, imependekezwa ndani ya mpango ule kwamba katika Makao Makuu ya kila Wilaya, ijengwe shule ya sekondari ya Serikali ambayo iende mpaka kidato cha sita ili iwe inapokea wanafunzi kutoka shule zingine zilizoko katika Wilaya ile. *(Makofi)*

Na. 84

**Huduma ya Matibabu kwa Wazee na Watoto**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishatoa ahadi yenye matumaini kwa wananchi kwamba, huduma ya matibabu kwa wazee na watoto kwenye Hospitali zote za Serikali itakuwa bure lakini inaelekea haizingatiwi na watoa huduma hizo, hasa wazee wa Mjini Morogoro:-

(a) Je, Serikali imebadili msimamo wa ahadi hiyo?

(b) Je, endapo hakuna badiliko, yanaweza kutolewa maelekezo ya ziada kwa wananchi na watoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kukemea wote wasiowajibika kutekeleza ipasavyo kauli za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Thobias Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara yangu, imebuni Sera ya Uchangiaji Huduma za Afya kwa madhumuni ya kuongeza kipato cha vituo vya kutolea huduma za afya ili ziongeze ubora wa huduma zao. Kwa mujibu wa sera hiyo, akinamama wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka 5, wazee walio na umri wa miaka 60 na zaidi na wasio na uwezo na wagonjwa wenye magonjwa sugu kama Ukoma, Kifua Kikuu, UKIMWI na magonjwa ya mlipuko, wamesamehewa kuchangia huduma za afya na hivyo kupata matibabu bila malipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijabadili sera hii na msimamo wa Wizara ni kwamba, makundi ya watu niliyoyataja hapo awali yataendelea kupata msamaha wa kuchangia matibabu.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine tena kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaagiza viongozi wa huduma za afya nchini, kufuata sera ya uchangiaji kikamilifu.

Aidha, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali imeweka mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa Afya chini ya Bodi za Afya za Wilaya, Mikoa na Hospitali za Rufaa, ili ziweze kukabiliana na matatizo kama haya. Hivyo, nachukua fursa hii kuzikumbusha Bodi husika kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale wote wanaokiuka maamuzi halali ya Serikali.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wapo wananchi wasio na uwezo wa kumudu matibabu haya ya uchangiaji na ambao wangeweza kujumuishwa katika kundi hili. Je, Serikali inaweza ikatazama upya uwezekano wa kuwasogezea utaratibu huu ili wajue kuwa Serikali yao tukufu inawajali pia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wananchi ambao hawako katika makundi niliyoyataja na vile vile hawana uwezo wa kujilipia matibabu. Utaratibu upo kila hospitali, kila kituo kinachotoa huduma za afya kinatakiwa kiwe na utaratibu wa kutoa misamaha kwa wale ambao watathibitika kwamba, hawana uwezo wa kujilipia matibabu.

Na. 85

**Sabuni za Kunenepesha**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kwamba zipo sabuni zilizoingizwa hapa nchini kutoka Uchina ambazo zina uwezo wa kunenepesha viungo kama vile maziwa, makalio na kadhalika na pia kupunguza matumbo makubwa na kuyafanya madogo *(flat)*; na kwa kuwa sabuni hizo zimepata soko zuri kutoka kwa akina mama wengi:-

(a) Je, Serikali inalifahamu suala hilo?

(b) Je, ni matatizo gani ya kiafya yanayoweza kuwapata watumiaji wa sabuni hizo?

(c) Je, ni sababu zipi zinazowafanya wanawake kupenda kubadilisha maumbile yao mazuri waliyopewa na Mwenyezi Mungu na je, Serikali itabadilishaje tabia hiyo miongoni mwa wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la sabuni zinazodhaniwa kuwa zinanenepesha lilijitokeza kwenye vyombo vya habari wiki chache zilizopita. Baada ya kupata taarifa hizo, Wizara yangu, kwa kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TEDA)*, ilituma timu ya wataalam kufuatilia sabuni hizo.

Mheshimiwa Spika, hakuna ushahidi wowote uliopatikana kuhusu kuwepo kwa sabuni zinazodaiwa kunenepesha sehemu za viungo vya wanawake kama matiti na kadhalika. Endapo Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa za uhakika kuhusu suala hili tunamwomba atupatie ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatukupata ushahidi wa kuwepo kwa sabuni hizo, Wizara yangu haiwezi kufahamu madhara yanayoweza kuletwa na sabuni hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la uzuri wa binadamu hususan mwanamke ni hisia ya mtu binafsi na jamii inayomzunguka. Mathalan katika nchi za Ulaya jamii inaona mwanamke mwembamba

ndio mzuri na ndio wanaotumika kwa matangazo ya biashara, kucheza sinema na kadhalika. Jambo hili hupelekea wasichana wadogo kujinyima chakula kwa kiwango kikubwa mpaka wengine kupata madhara ya kiafya mfano Ugonjwa wa *Anorexia Nervosa.*

Katika jamii nyingine wanawake wanene ndio huonekana wazuri wakati unene uliokithiri pia huleta madhara ya kiafya mfano shinikizo la damu, kisukari na magonjwa ya moyo. Hivyo hivyo kwa jamii zinazoona wanawake weupe ndio wazuri. Kwa hivyo, Serikali inatoa wito kwa makundi yote ya jamii hususan wanawake na vyombo vya habari, kuelimisha jamii husika kupenda maumbo waliyopewa na Mwenyezi Mungu badala ya kutumia njia zisizofaa za kubadilisha maumbo yao, jambo ambalo mara nyingi huambatana pia na madhara ya kiafya. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inapinga kwa nguvu zake zote uharibifu wa mazingira na hata inafikiria kutayarisha Muswada juu ya mazingira. Je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka kipengele katika Muswada huu kinachokataza wananchi kuharibu mazingira ya miili yao kama vile kutumia mikorogo na vinginevyo au hiyo itakuwa ni kuvunja haki za binadamu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuzuia madawa yanayoathiri wanadamu upo. Utaratibu huo ni kupitia Shirika letu la *Tanzania Food and Drug Authority* kupita kukagua katika maeneo yanayouzwa dawa ili kuhakikisha kwamba, dawa zenye madhara zinaondolewa kutoka kwenye soko. Kwa hiyo basi, sioni umuhimu wa kuweka suala kama hilo katika Sheria ya Mazingira. Ni vitu viwili tofauti. Pamoja na kwamba kuna msanii anasema "Mwanamke Mazingira". Lakini ukweli ni kwamba, sheria hii inahusu zaidi matibabu na iko katika mpango wetu wa *Tanzania Food and Drug Authority* kuweza kuhakikisha wanaondoa dawa zenye madhara kutoka kwenye soko la nchi yetu.

Na. 86

**Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa kukusanya kodi ni jambo muhimu katika harakati za kuondoa umaskini; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua za makusudi za kuboresha ukusanyaji wa mapato:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipi kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuanzia mwaka 1990 hadi sasa mapato ya Serikali kila mwaka yamekuwa yakiongozeka namna gani?

(b) Je, kila sekta ya uchumi imekuwa ikichangia asilimia ngapi ya mapato kutoka mwaka 1990 hadi swali hili linapojibiwa?

(c) Je, kuanzia mwaka 1990 hadi sasa Serikali inakusanya asilimia ngapi ya Pato la Taifa *(Gross Domestic Product at Market Prices)* kwa kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ni moja kati ya shughuli kuu za Serikali. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha mfumo mzima wa ukusanyaji na taratibu zake ili kuhakikisha kuwa mapato mengi zaidi yanakusanywa. Ili kutekeleza azma hii, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* mwaka 1996 na kuikabidhi shughuli zote za kuratibu na kudhibiti ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuitumia *TRA,* Serikali imeanzisha taratibu kadhaa katika kuboresha usimamizi na ukusanyaji wa mapato. Taratibu hizo ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* kutoa namba maalum kwa walipa kodi *(TIN),* kuanzisha Idara ya Walipa Kodi Wakubwa, kuweka mfumo mpya wa kukusanya kodi kwenye mafuta ya petroli, udhibiti wa magendo kwa kutumia boti ziendazo kwa mwendo wa kasi *(Patrol Boats),* utumiaji wa Ankara za Elektroniki *(Electric Cash Registers)*, Hati za Hazina *(Treasury Voucher System)* kwa misamaha ya kodi inayotolewa kwa Watumishi wa Umma, Mashirika Yasiyo ya Serikali *(NGOs)* na Taasisi zote za kidini, kuondoa sheria za kodi zenye kero, kupunguza viwango vya kodi mbalimbali na uandikishaji wa kisasa wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, kasi ya ukusanyaji wa mapato imeongezeka mwaka hadi mwaka. Kati ya mwaka 1996/1997 na 2002/2003, mapato yaliongezeka kutoka shilingi 515.144 bilioni hadi shilingi 1,144.438 bilioni. Kwa mwaka 2002/2003 mchango wa kila Idara katika makusanyo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Kodi ya Mapato shilingi bilioni 312,117, Kodi ya Ongezeko la Thamani shilingi bilioni 312,946 na Ushuru wa Forodha shilingi bilioni 519,375

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imechukua hatua za kuboresha Utendaji ndani ya *TRA* kwa upande wa watumishi na teknolojia. Kwa upande wa watumishi hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuboresha ujuzi na viwango vya utaalamu, kuinua viwango vya mafao ya wafanyakazi na mazingira ya kufanyia kazi, kuimarisha udhibiti wa usimamizi na nidhamu na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati Maalum inayoratibu masuala hayo na kuwasilisha taarifa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa teknolojia ya mifumo ya kisasa ya kompyuta katika sehemu tofauti za Idara za Mamlaka, imeanzishwa kwa ajili ya malipo mbalimbali na uwekaji wa kumbukumbu za mapato na walipa kodi. Aidha, mitambo ya *Closed Circuit Television* imewekwa ili kudhibiti shughuli za utendaji katika ukaguzi wa mizigo na utozaji wa ushuru katika Forodha ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Dar es Salaam.

Mheshimwa Spika, *TRA* pia imeanzisha Mpango Mkuu wa Miaka Mitano. Mpango huu unaelezea dira, dhamira, madhumuni na mikakati itakayowezesha *TRA* kuwa chombo cha kisasa cha usimamizi wa kodi ifikapo mwaka 2008. Utekelezaji wa mpango huu kikamilifu utaboresha zaidi ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, sekta zote za uchumi zimekuwa zikichangia ingawa kwa viwango tofauti katika mapato ya Serikali. Sekta ya viwanda na biashara ikijumuisha uagizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, imekuwa na mchango mkubwa zaidi katika mapato ya Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, uwiano kati ya ukusanyaji wa kodi na Pato la Taifa umekuwa ukibadilika hasa katika miaka ya 1990 - 1995 kutokana na marekebisho ya mara kwa mara ya takwimu za Pato la Taifa wakati huo. Katika kipindi hicho yaani 1990 - 1995 mapato ya kodi yalifikia wastani wa asilimia 11.7 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha 1996 - 2004, uwiano kati ya makusanyo ya mapato na Pato la Taifa uliimarika na hivi sasa ukusanyaji umefikia asilimia 13.2 ya Pato la Taifa, baada ya kusuasua kwenye wastani wa asilimia 11 kati ya 1996 na 2002.

Mheshimiwa Spika, uwiano kati ya makusanyo ya kodi na Pato la Taifa ulitegemewa uwe mkubwa zaidi ya kiwango cha sasa iwapo sekta zote zingechangia katika kulipa kodi. Sehemu kubwa ya uchumi wetu inatokana na kilimo, ikifuatiwa na sekta isiyo rasmi. Sekta hizi mbili zina mchango mdogo kwenye makusanyo ya kodi, hivyo uwiano wa jumla kati ya makusanyo ya kodi na Pato la Taifa unakuwa mdogo. Vinginevyo, ukusanyaji wa mapato ya kodi umekuwa unaongezeka mwaka hadi mwaka na sasa tunakusanya shilingi 108 bilioni kwa mwezi, ambazo zinagharamia asilimia karibu 55 ya matumizi yote ya Serikali.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kumekuwepo na utaratibu wa baadhi ya Makampuni kupata *Tax Holiday* na baada ya muda kubadilisha majina kwa nia ya kuendelea kupata *Tax Holiday* mpya. Kwa mfano, *Sheraton Hotel* walibadilisha jina wakajiita *Royal Palm Hotel.*

**SPIKA:** Hebu uliza swali moja acha maelezo.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** *Sheraton Hotel* walipojibadilisha jina wakajiita *Royal Palm Hotel* walipata kibali kipya cha *Tax Holiday* au waliendelea lakini kibali ni cha zamani? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa chombo hiki ndicho pekee chenye uwezo wa kuruhusu kodi yoyote ikusanywe hata ikiitwa ada; na kwa kuwa *TRA* hivi sasa wanakusanya shilingi 10,000 kama sehemu ya ada ya kupata namba mpya za magari; je, kwa nini *TRA* wanajigeuza Bunge dogo na kunyakua madaraka ya Bunge ambacho ndicho chombo pekee cha kutoa kibali cha kukusanya kodi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, *Sheraton Hotel* ilipobadilika kuwa *Royal Palm Hotel,* taratibu zote zilifuatwa na hapakuwa na *Tax Holiday*. Kodi zote za Serikali na utaratibu wote wa uwekezaji katika hoteli ile ulifuatwa.

Pili, ada ya shilingi 10,000 kwa ajili ya usajili wa magari inatokana na kwa kuwa utaratibu huu ni mpya. Katika nchi nyingine nyingi ambazo zina utaratibu huu wa namba kwa mfano, Ujerumani wana kitu kinaitwa *TUV,* ambapo kila mwaka inabidi upeleke gereji gari lako likaguliwe na litakapokaguliwa linapata *wetness* ya kuwa barabarani. Kwa hiyo, gharama hii ni kwa ajili ya *process* ya *registration* ya magari. Unahitaji *computer,* karatasi na teknolojia kwa ajili ya shughuli hiyo. Kwa hiyo, ada hii ni kwa ajili ya kusajili gari sio kodi mpya ambayo ilitakiwa ipite kwenye Bunge. Ni kodi ambayo ina-*facilitate* zoezi zima la *registration.*

Na. 87

**Mfuko wa *PPF***

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa *PPF* unawekeza michango ya wanachama wake kwa lengo la kukuza raslimali ya mfuko na hivyo kuweza kulipa mafao bora zaidi hasa wanachama na kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa Taifa katika vitega uchumi vya raslimali zinazoriba *(Fixed Income Assets)* hisa za Kampuni *(equities)* na majengo ya kupangisha *(Real Estates):-*

(a) Je, ni kwa kiwango gani mfuko huo umeboreka zaidi kwa njia hizo?

(b) Je, kuna tofauti gani ya mapato kati ya mwaka na mwaka?

(c) Licha ya kupanga, je, mtu anaweza kujengewa au kuuziwa nyumba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, fedha za wanachama katika Mfuko wa *PPF* huwekezwa katika maeneo matatu; raslimali zenye riba maalum inayojulikana *(Fixed Income Assets)* hisa za Makampuni *(equities)* na majengo ya kupangisha *(properties)*. Sababu kubwa ya kuwekeza katika maeneo hayo ni kulinda fedha za wanachama zisipotee. Uwekezaji hufanywa kwa taratibu na kanuni zinazohakikisha kuwa fedha

zinatunzwa ipasavyo na kupatikana faida ambayo hatimaye hujumuishwa na michango ya mwanachama wakati anapofikia umri wa kulipwa mafao yake. Hali hii ndivyo ilivyo katika sekta nzima ya Pensheni ya Jamii duniani kote.

Mfuko wa *PPF* umewekeza fedha za wanachama kwa kutumia Sera ya Mfuko ya Uwekezaji *(Investment Policy)* iliyoridhiwa na kupitishwa na Bodi ya Wadhamini *(Board of Trustees).* Kwa sasa viwango vya uwekezaji katika sera hiyo ni asilimia 55 kwa raslimali za riba maalum inayojulikana kama *Fixed Income Assets,* asilimia 40 kwa majengo ya kupangisha na asilimia 5 kwenye hisa za Makampuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *PPF* umekuwa ukiboreka mwaka hadi mwaka kutokana na faida itokanayo na uwekezaji nilioueleza pamoja na mapato mengine kama vile michango ya wanachama. Kati ya mwaka 1999 na 2000, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 10 kutoka shilingi bilioni 83.7 hadi shilingi 91.9 bilioni. Kati ya mwaka 2000 na 2001 ongezeko lilikuwa ni asilimia 17 ambapo thamani ya Mfuko ilikuwa ni shilingi bilioni 107.7. Kufikia mwaka 2002 thamani ya Mfuko ilikuwa ni shilingi bilioni 128.0 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2001.

(b) Mheshimiwa Spika, mapato ya mwaka hadi mwaka kutokana na uwekezaji katika kipindi cha mwaka 1997 - 2002 yalikuwa kama ifuatavyo: Mapato yatokanayo na uwekezaji yalipungua kwa asilimia 1.5 kutoka shilingi bilioni 5.84 mwaka 1997 na kufikia shilingi bilioni 5.75 mwaka 1998. Hii ilitokana na kushuka kwa faida *(Interest Rates)* zitolewazo kwenye dhamana za Serikali na pia kutokana na kupungua kwa kiwango cha uwekezaji wa dhamana hizo za Serikali. Aidha, mapato hayo yaliongezeka kidogo kwa asilimia 0.2 kutoka shilingi bilioni 5.75 mwaka 1998 hadi kufikia shilingi bilioni 5.76 mwaka 1999. Hii ilitokana na ongezeko la uwekezaji wa dhamana za Serikali ambazo zilipelekea pia ongezeko la faida zotolewazo na dhamana hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 mapato hayo yaliongezeka kwa asilimia 18 kufikia shilingi bilioni 6.79. Pamoja na kwamba kulikuwa na kupungua kwa viwango vya fedha za Mabenki lakini mapato yatokanayo na pango za nyumba yalichangia kuongezeka kwa mapato hayo. Ongezeko kwa mwaka 2001 ilikuwa ni asilimia 5 kufikia shilingi bilioni 7.17. Ongezeko la pato litokanalo na pango pamoja na hisa za Kampuni lilifidia upungufu uliosababishwa na kushuka kwa viwango vya faida za Mabenki pamoja na dhamana za Serikali. Kwa mwaka 2002 mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kwa asilimia moja tu na hii ilitokana na kupungua sana kwa riba zitokanazo na Mabenki pamoja na dhamana za Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, licha ya kupangisha majengo na nyumba zake, Mfuko wa *PPF* umeanzisha mpango wa ujenzi kwa nyumba za kudumu za bei nafuu kwa ajili ya kuwauzia wanachama wake kwa mkopo. Kwa kuanzia, Mfuko umepata maeneo ya kujenga nyumba kama hizo Kibaha na Mwanza. Nyumba zitakazojengwa Kibaha ni kwa ajili ya Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Tayari Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi *(UCLAS),* kimekwishapewa kazi ya kupima viwanja katika maeneo husika. Baada ya kazi hiyo kukamilika, hatua itayaofuata ni kuwalipa fidia wananchi waishio katika maeneo hayo. Inatarajiwa kuwa shughuli hizi mbili zitakamilika hadi kufikia mwisho wa mwaka huu 2004 na ujenzi kuanza baada ya hapo.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina masuala mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kulingana na zile taarifa alizozitoa kuwa katika mfumo huu au hizi hatua tatu alizozitaja za kuongeza mapato, je, ni hatua ipi ambayo wananchi wanaipendelea sana ambayo haiwasumbui na Serikali inapata tija ndani yake?

Pili, je, mifuko mingine inao utaratibu kama huu wa *PPF?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, nilieleza kwamba kuna njia tatu ambapo Mfuko wa *PPF* unawekeza. Moja ilikuwa ni raslimali zenye riba maalum na Hisa za Makampuni, pamoja na majengo ya kupangisha .

Mheshimiwa Spika, njia inayopendelewa zaidi na wananchi kwa sababu wananchi hawahusishwi moja kwa moja katika kutoa maamuzi ni Mfuko wa *PPF* na Bodi ya Wadhamini *(Board of Trustees)* ambao ndio wanatoa maamuzi kwa niaba ya wanachama kwa nia ya kulinda mali iliyopo pale isipotee na iweze kuongezeka kulinda mfuko uongezeke kama nilivyoeleza. Kwa hiyo njia zote hizi zinatumika. Lakini Bodi ya Wadhamini huwa inaangalia ni ipi ambayo haitaleta hasara na hatimaye fedha za wanachama kupotea.

Mheshimiwa Spika, Makampuni yote ya Hifadhi za Jamii duniani kote yanafanya shughuli kama inavyofanya *PPF*. Kinachotakiwa hapa ni uangalifu wa kuhakikisha kwamba, fedha za wanachama zinalindwa kwa kiwango cha hali ya juu na kwamba hazipotei.

Na. 88

**Matengenezo ya Barabara ya Mbeya-Rungwa**

**MHE NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitangaza kuwa kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya matengenezo maalumu na ya kawaida kwa barabara ya Mbeya-Rungwa-Itigi:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa barabara yote?

(b) Je, ni kiasi gani kimetumika hadi sasa na ni maeneo gani yaliyotengenezwa?

(c) Je, mpango wa kuweka lami kwenye barabara kati ya Mbeya-Chunya-Makongolosi ambayo ndiyo mwanzo wa kuweka lami barabara yote, utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbeya hadi Itigi ni barabara muhimu inayounganisha Mikoa ya Mbeya na Singida na inahudumiwa na Mikoa hiyo miwili. Kilometa 295 za barabara hii zipo upande wa Mkoa wa Mbeya kuanzia Mbeya hadi Rungwa na kilomita 196 kutoka Rungwa hadi Itigi zipo Mkoa wa Singida.

Katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, kiasi cha shilingi 640.34 milioni kimetengwa kwa barabara hii ambapo shilingi milioni 389.03 zimetengwa Mkoa wa Mbeya na shilingi milioni 251.31 zimetengwa Mkoa wa Singida.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotumika hadi sasa ni kama ifuatavyo: Katika Mkoa wa Mbeya jumla ya shilingi milioni 36.85 zimetumika. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 16.9 zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuanzia *Rift Valley* hadi Maji Mazuri na shilingi milioni 20 zimetumika katika kuboresha eneo la Mamba "A" lililokuwa limejaa mchanga.

Katika Mkoa wa Singida jumla ya shilingi milioni 204.52 zimetumika. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 8.5 zimetumika kwa matengenezo ya kawaida kati ya Mgandu na Itigi (km. 30) na shilingi milioni 159.2 zimetumika kwa matengenezo ya muda maalum kati ya Itagata na Mlongoji (km. 35).

Aidha, kilomita 30 kati ya Rungwa na Kiyombo zitatengenezwa kwa gharama ya shilingi 809.74 milioni chini ya mradi wa ukarabati wa barabara zilizoathiriwa na mvua za *El-Nino.* Kati ya fedha hizo, shilingi 722.45 milioni ni fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na shilingi 84.29 milioni ni fedha za Tanzania. Mkataba wa kazi hii umesainiwa tarehe 8 Januari, 2004 kati ya *TANROADS* na Mkandarasi *M/S Badr East Africa* na kazi hii inatarajiwa kuanza wakati wowote. Zabuni kwa ajili ya matengenezo mengine ya kawaida pamoja na ukarabati wa daraja la Doroto tayari zimetangazwa na kazi zitaanza robo ya tatu ya mwaka 2003/2004. Kazi hizi zitafanyika kati ya Itagata na Ukimbu na zinakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi 75 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Mbeya - Itigi kwa kuunganisha Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kanda ya Kati na ya Kanda ya Ziwa, imepanga kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ili kuweza kutimiza lengo hili, Serikali imefanya na kukamilisha upembuzi yakinifu wa sehemu ya kwanza ya barabara hii kwa kuanzia Mbeya - Chunya hadi Makongolosi mwaka 2002/2003. Mnamo tarehe 22 Januari, 2004, Serikali imesaini mkataba na Kampuni ya *BCEOM* ya Ufaransa ikishirikiana na *M-Konsult* ya Tanzania, kufanya usanifu wa sehemu ya kwanza ya barabara hii. Kazi za usanifu zitakamilika Februari, 2005. Baada ya usanifu kukamilika, taratibu za kumpata Mkandarasi na kuanza ujenzi ndipo zitakapoanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Kwa kuwa fedha za matengenezo ya kawaida zilizotengwa kwa upande wa Mkoa wa Mbeya ni kiasi kidogo tu mpaka sasa kimeshatumika. Je, kiasi kingine kilichobakia ni maeneo gani ambayo yatafanyiwa matengenezo kati ya Chunya na Rungwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, fedha zilizopangwa kwa matengenezo ya kawaida ni fedha ndogo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na zimeshatumika. Lakini akiangalia katika majibu yangu, kuna fedha nyingi sana ambazo tumezipanga kwa matengenezo maalum ili tufikie kiwango cha lami. Kwa hiyo, ndiyo maana tumepunguza fedha za matumizi ya kawaida.

Ni maeneo gani sasa kwa fedha zingine itabidi tutafute fedha ili kujua ni maeneo gani muhimu. Kwa kawaida haya huwa yanapangwa na *Regional Manager,* ambaye yeye ndiyo anakagua hiyo barabara kila wakati.

Na. 89

**Kuwahamisha Watu Waliojenga Kwenye Hifadhi za Barabara**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwahamisha watu waliojenga kwenye eneo la hifadhi ya barabara *(Road Reserve)* na kuonyesha mifano mizuri ya kujenga barabara zinazofaa:-

(a) Je, uhamisho na ubomoaji wa nyumba za barabara ya Kilwa ulikuwa kwa lengo la ujenzi wa barabara nzuri na pana kwa ajili ya msongamano wa magari au ulikuwa kwa lengo gani?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na tabia ya kudharau Kanda ya Kusini kiasi ambacho hata njia ya kuelekea huko haifahamiki, je, ni lini Serikali itaipanua barabara hiyo kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uhamisho wa mali zilizokuwepo ndani ya Hifadhi ya Barabara ya Kilwa una lengo la kujenga upya na upanuaji wa barabara iliyopo kwa kiwango cha lami. Upanuzi huo

unatokana na mahitaji yanayosababishwa na msongamano mkubwa wa magari na pia kutenganisha barabara za waenda kwa miguu na baiskeli na ile ya magari. Mpango wa utekelezaji wa mradi huu umeonyeshwa wazi kupitia Bajeti ya mwaka 2003/2004 ambapo shilingi 778 milioni zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Barabara ya mwaka 1969 na 1967 ambazo zinatokana na sheria za zamani za miaka ya 1954 na 1930, barabara husika imetajwa. Aidha, kwa kupitia Bajeti zote za miaka ya nyuma, barabara hizo zimekuwa zinatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za changarawe na lami. Barabara za lami ni pamoja na Dar es Salaam - Kibiti (km. 145), Kibiti - Ikwiriri (km. 30), Ikwiriri - Ndundu (km. 14) ikijumuisha daraja la Mkapa. Masaninga - Nangurukulu - Kilwa Masoko (km. 50), Lindi - Mingoyo (km. 25), Mingoyo - Mtwara (km. 92) na Mingoyo - Masasi (km. 103)

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia mradi maalum wa barabara kuu, Serikali sasa inajenga kwa kiwango cha lami sehemu zote zilizosalia zisizokuwa na lami zenye urefu wa kilomita 213 kati ya Somanga - Masaninga na Nangurukulu - Lindi - Mingoyo. Sehemu mbili nyingine kati ya Kimanzichana na Kibiti (km. 60) pamoja na Ndundu - Somanga (km.55) zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa lengo la kukamilisha barabara yote kwa kiwango cha lami ifikapo mwaka 2006. Aidha, katika juhudi za Serikali za kuunganisha kanda za usafirishaji, barabara ya Masasi - Songea - *Mbamba Bay* (km. 649) imefanyiwa upembuzi yakinifu ambao umekamilika Desemba, 2003 chini ya msaada kutoka Serikali ya Kuwait.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo niliyotoa ni dhahiri Serikali hata siku moja haijawa na tabia ya kudharau Kanda ya Kusini na siyo kweli kuwa njia ya kuelekea Kusini haifahamiki. Aidha, siyo Ukanda wa Kusini wa barabara pekee ambao umechelewa kujengwa kupitia kiwango cha lami bali sehemu nyingi za nchi zinahusika ikiwemo barabara anakotoka Mheshimiwa Mabina yaani Geita kama inavyojionyesha kwenye vitabu vya bajeti kwa miaka ya nyuma na wakati huu. Hii yote imetokana na sababu zinazoeleweka na uwezo mdogo wa kiuchumi wa nchi yetu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa swali lenyewe limekuwa la mwisho na nimesema kwamba Kusini inakuwa ya mwisho na nafikiri hata Bunge lenyewe limeshaiweka sehemu hiyo kuwa ya mwisho. Je, Serikali kama imeamua kupanua ile barabara ya Kilwa, Wananchi wanaoishi kando kando ya Ziwa wanaweza wakafidiwa? Kwa sababu tangu walivyopanua ile barabara mpaka sasa hivi hawajafidiwa chochote.

(b) Kwa kuwa kumekuwa na utaratibu wa Wananchi wa Kusini (Wamachinga) kutembea kwa miguu na barabara yao imekuwa ni finyu. Je, barabara itakapopanuliwa hao Wamachinga wanaweza kurudishwa nyumbani kama alivyorudishwa Matonya? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hitimisha majibu yako.

**MJUMBE FULANI:** Anatafuta msaada.

**SPIKA:** Unatafuta msaada? Umeupata. Mheshimiwa Waziri mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu letu la msingi tumeeleza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kutengeneza barabara yote ya kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara na tumeeleza kwamba, hatua za kutengeneza barabara zote kwa kiwango cha lami bado hazijafikiwa na tukatoa mfano hata kwa barabara ambayo Mheshimiwa Mabina anatoka nayo ni barabara ya kutoka Usagara - Geita hadi Biharamulo, nayo haijatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *compensation* za watu waliobomolewa nyumba, sheria iliyopitishwa na Bunge hili, Sheria Namba 67 ya mwaka 1967 ambayo ilikuwa *gazetted* tarehe 5 Mei, 1967 ambayo imeanza kutumika tangu mwaka 1930 ikafanyiwa *amendment* mwaka 1938 na ikafanyiwa *amendment* nyingine mwaka 1954, inazungumzia upana wa barabara. Kwa hiyo, kwa sheria hiyo kama mtu anajenga

barabarani awe kwenye barabara ya Kusini, awe kwenye barabara ya Geita au awe kwenye barabara ya Mkoa wowote ni lazima nyumba yake ibomolewe ili aache nafasi ya kujenga barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Wananchi waliobomolewa nyumba hizo katika barabara ya Kusini hakuna *compensation* yoyote itakayotolewa. Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2003/2004, imetenga Shilingi bilioni moja ambazo ujenzi wake utaanza mwaka huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Tunaendelea.

Matangazo ya vikao vya Kamati kwa siku ya leo ni kama ifuatavyo: Kamati ya Uongozi imepangiwa kukutana saa 7.00 baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi. Kamati nyingine ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Mgombelo, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.00 vile vile katika ukumbi Namba 428 *wing C* ghorofa ya nne kwa ajili ya kukutana na Bodi ya Usafiri Dar es Salaam *(UDA)*. Kamati nyingine ni ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anna Makinda Mwenyekiti wake, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 219 ghorofa ya pili. Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane na Wabunge wa Afrika Mashariki katika chumba namba 231 ghorofa ya pili saa 10.00 jioni.

Kamati ya mwisho iliyopangiwa kukutana leo ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Lubeleje, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 9.00 mchana katika ukumbi namba 133 ghorofa ya kwanza. Hiyo ndiyo mikutano ya Kamati.

Pili, napenda kutoa taarifa rasmi Bungeni kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalihutubia Bunge hili kesho kutwa tarehe 12 Februari, 2004 katika kikao chake cha asubuhi. Kamati ya Uongozi inakaa leo kukamilisha ratiba yake, lakini kuna gazeti moja lilitoa taarifa za kupotosha kwamba, Rais aomba kuhutubia Bunge. Rais haombi kuhutubia Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Rais haombi kwa sababu kifungu cha 91(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinasema hivi: "Rais atalihutubia Bunge jipya katika mkutano wake wa kwanza na kulifungua rasmi Bunge hilo." Bila kuathiri masharti ya ibara hiyo niliyoisoma kifungu kidogo cha (2) kinasema: "Rais aweza wakati wowote kulihutubia Bunge." Anachohitaji ni kumuarifu Spika tu kwamba yuko tayari kuhutubia Bunge halafu anapangiwa siku ya kufanya hivyo, haombi. Ninaamini watarekebisha mambo yao. *(Makofi)*

Kuhusu *Order Paper* ya leo ni kwamba, tumepanga mjadala wa jumla uendelee mpaka saa 7.00, halafu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, ataanza kujibu katika kipindi cha mchana tutakaporejea saa 11.00.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa wa Mwaka 2004 *(The Transfer of Prisoners Bill, 2004).*

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988 wa Mwaka 2004 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges (Amendment) Bill, 2004).*

Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wa mwaka 2004 *(The Government Students' Loan's Board, Bill 2004).*

Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa Mwaka 2004 *(The Diary Industry, Bill 2004).*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada hiyo imesomwa mara ya kwanza, ukiondoa mmoja mingine iliyobaki itajadiliwa katika mkutano ujao. Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, umepangwa kujadiliwa katika mkutano huu huu unaoendelea, utawekwa kwenye *Order Paper* katika wakati muafaka na leo hii nitaupeleka kwenye Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ili uweze kuchambuliwa.

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko katika Sheria ya Ardhi wa Mwaka 2003 (*The Land (Amendment) Bill, 2003)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie Muswada wa Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, aliyeteuliwa kurudi tena Bungeni kwa sababu mwaka 1995 mpaka 2000 tulikuwa naye. Ninampongeza kwa kurudi tena Bungeni. Pia, niwapongeze wale walioteuliwa kwenda katika Bunge la Afrika, wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Muswada huu wa Ardhi kuwawezesha wenye haki ya ardhi kupewa hati na mikopo, tatizo langu ni dogo tu. Nia ni kuondoa umaskini, lakini umaskini huu unajulikana ni kwamba tulikuwa tunashindwa namna ya kupewa mitaji, ni hilo tu.

Mheshimiwa Spika, ninasumbuliwa na eneo linalosema: "Akishakuwa na hati ya ardhi yake akipewa mkopo baadaye akishindwa kulipa ardhi ile iuzwe." Maana yake nini? Naomba marekebisho hapa, kwamba mtu apewe mkopo kutokana na hati ya ardhi aliyonayo kupitia kijijiji halafu turudishe sheria ya ushirika na nguvukazi, mikopo ile ifanye kazi ya kilimo, dhamira yake iwe ni kukopesha kwa ajili ya kilimo au mazao yatakayotokana na kilimo yalipe deni, ardhi yake ikingwe kwa msingi huo. Hili mliloliweka kwamba wanaweza wakauza na ardhi hiyo, mtaongeza umaskini kweli kweli kwa sababu umaskini huu tulionao tumekingwa kwa kuwa na ardhi, sasa tukiruhusu wauze na ardhi yake hawa watakuwa watumwa kweli kweli. Ni utumwa ule wa ukoloni mamboleo ndiyo utakaorudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna mfano mdogo tu katika Jimbo la Mikumi. Kazi tunayoifanya kwenye ardhi hii tumekubaliana na wawekezaji. Mikopo inatolewa na wawekezaji na siyo Serikali. Mtu anakopeshwa mbegu, analimiwa, anapandiwa, anasimamiwa kupalilia halafu analipa ule mkopo kwa kupitia mazao atakayoyauza. Sheria ingetosha kusimamia hapo tu, isiteremke huku kuuza ardhi endapo atashindwa kulipa, halafu baadaye akiuza ardhi atabaki na nini? Serikali mtuambie sasa ni nani huyu atakayekuwa ananunua ardhi za watu? Yaani ukishindwa kulipa anakuja ananunua ardhi yako, ni nani mliyekubaliana naye? Mtuambie maana yasije yakazuka mambo ya Zimbabwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Zimbabwe wanahangaika na *plan* hii tuliyonayo, wamenyang'anya ardhi ya wawekezaji wakubwa wanawapa wadogo. Sasa na sisi tunataka mkubwa mmoja aje na hela zake kwa kipindi cha miaka mitano au kumi anawinda ardhi za Serikali za watu/za Vijiji baadaye anazinunua zote inabakia sisi hatuna ardhi, huyo mwekezaji anakuwa na ardhi kubwa. Tutaleta matatizo ya Zimbabwe hapa. Hii tunayosema tunawaenzi Viongozi wetu, tunafuata nyayo zao, kuuza ardhi hii ndiyo kufuata nyayo zao? Kweli tunafuata nyayo zao kwa msingi huu mpya! Hapa hatuwaenzi wala hatufuati nyayo zao, tunaanza kuwauza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano wa ardhi ya vijiji vya wafugaji. Nampongeza sana Mheshimiwa Lekule Laizer, jana amezungumzia sana hili pamoja na Mheshimiwa Losurutia pale kwamba, hivi hao nao mtawapakiaje, maana ni eneo kubwa la hekta 4,000 wanakwenda kuchunga pamoja.

Mtakwenda kupima kule msituni kwamba wewe lima hapa na hati yako ni hii, eneo lako liishie hapa, je, baadaye ukishindwa kulisha na ng'ombe wakifa uuze pori? Mtafanyaje na hii? Tunaomba majibu mazuri hapa. Mnaanza kusumbua, haya ni matatizo, tunaelekea kwenye uchaguzi bado mwaka mmoja tunaletewa sheria za balaa balaa namna hii, haturudi humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali itusaidie kwamba maeneo ya wafugaji kwa mfano kwangu pale Kidui, Twatwatwa na Filisi wanieleze maeneo yale mnayafanyaje, yanakuwa yanamilikiwa na Kijiji au mtu mmoja mmoja? Huyo mtu anaweza akauza pori lile katikati pale karibu na mabwawa ya kunywesha maji ng'ombe na mabwawa yatakuwa ya nani sasa maana mle sisi tume-*invest* mabwawa tayari, ng'ombe wanakwenda pale wanakunywa maji. Hizo ni hekta 4,000 kwa mfano ninazosema, wanalisha kwa pamoja. Ushauri wangu hapa zaidi ni kwamba, niombe basi Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Fedha, wasaidiane namna ya kusimamia hii mikopo kwa sababu kinachotakiwa hapa ni kumwezesha huyu mkulima apate mkopo na alime. Sasa hivi naishukuru sana Wizara ya Ushirika na Masoko kwani tumeanza kulima pamba. Tumelima sana pamba Kilosa na mwaka huu tunategemea kuvuna pamba nyingi. Sasa, tunachosema kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Kilimo na Chakula watusaidie kupeleka wataalam ili wapande vizuri ile pamba. Wizara ya Ushirika na Masoko watusaidie kutafuta soko la pamba ile itakapokuwa tayari imevunwa ipate soko. Wizara ya Fedha, Wizara ya Ushirika na Masoko pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa pamoja wangoje wakati tutakapouza, mikopo yao wakate kwenye fedha za mauzo. Tuwaombe wataalam waende vijijini na siyo kukaa tu maofisini. Hii hati ya ardhi mimi nakubali niimiliki, lakini kusema nitapoteza hati yangu kwa sababu eti nimepewa mkopo na bahati mbaya mvua hazikunyesha, mazao sikuvuna, baada ya siku 30 mnazozungumza anakuja mtu anasema nilikukopesha ardhi hii sasa iuzwe iwe ya kwangu, tutapata matatizo kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, wewe una uzoefu. Huko vijijini kwetu, hata kule kwako Ukerewe, hivi kweli kuna wataalam watakaozungumzia mambo ya pesa na ardhi mpaka mtu aokoe ile ardhi, wapo? Nina wasiwasi kwamba hawapo. Hawa wavuvi wenzetu pale kweli wanaweza kusimamia mambo ya pesa? Hata wavuvi sasa inabidi tuwazungumzie maana maeneo ya uvuaji yatapotezwa, kwamba eneo hili limeuzwa uliliwekea rehani sasa hatuvui tena, si ndiyo maana yake? Katika maeneo ya madini hali kadhalika, kwamba maeneo hayo pamoja na nyumba yako uliikopea mkopo sasa ondoka hapa tunafuatilia madini yaliyoko chini. Chonde kama walivyosema wenzangu kwamba, suala la ardhi tukilizungumza juu juu hivi bila kuliangalia litatuletea matatizo. Kilimo ni ajira iliyobaki kwa Wananchi. Tunasema asilimia 85 wanaajiriwa na kilimo, leo tunataka kunyakua ardhi hii, ajira ya asilimia 85 iende kwenye mikopo isimamiwe na ardhi na watu hawa hawajasomea mambo ya fedha, ni matatizo kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, Serikali huko nyuma ilitoa mikopo kwa mashamba makubwa kwa wakulima wakubwa, hawa wakachukua fedha tu wakaenda kufanyia biashara Mijini. Kwangu pale kuna mashamba kama Shamba la Mauzi, Shamba la Ulaya, Shamba la Mwenda na Shamba la Ruembe. Mashamba haya Waziri wa Ardhi ameshayafikia, mashamba haya Waziri wa Kilimo ameshayaona, matatizo yake mpaka leo yanaonekana ni mashamba ya hao wakubwa. Tunachoomba ni kwamba, wakulima wadogo wadogo kupitia vijijini, vijiji ndiyo vimiliki hiyo sehemu ili waweze kulima pamba hii niliyoisema na wapewe mikopo wale wanyang'anywe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, alifika alifika kwetu mwaka 1998, Waziri wa Kilimo na Chakula alifika mwaka 2000, naomba tufike mahali haya mashamba wapewe wakulima wadogo wadogo. Shamba la Ruembe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali analifahamu, kesi iko kwake toka mwaka 1997, anazungumza kwamba, bado anatazama sheria kutokana na utaratibu wa sheria ambapo kesi ikishakuwa Mahakamani ni juu ya wenye sheria.

Mheshimiwa Waziri, jana ulisifiwa sana na Mheshimiwa Bendera kwamba, ulikwenda kwenye Jimbo lake na umetatua hili tatizo. Ni kwa nini pale Ruembe usitatue tatizo la hili shamba? Sheria ni hizo hizo ulizozitumia pale kwa Mheshimiwa Bendera, hebu zitumike na kwangu pale kwenye Shamba la Ruembe. Toka mwaka 2003 nilizungumza, tuliwasiliana vizuri ukasema shemeji nisubiri kidogo. Ni kweli mimi ni shemeji yako, sasa shemeji si urudi basi, dada yako atakula nini? Hebu tulitazame hili Shamba la Ruembe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tutakapokuwa tunampa hati mwenye shamba ningeomba Kijiji kihusike kikamilifu, yaani wawe na nafasi yao ya kusaini, kwa sababu sasa hivi hatuna ardhi ya mtu, ardhi yote iko

chini ya Serikali ya Kijiji kwa mujibu wa sheria, ardhi yote ni ya Rais. Sasa, kijiji kama kijiji, kama hakitawekewa kipengele cha kusimamia ardhi hiyo na katika hati hiyo kijiji kama hakitasaini kwamba eneo hilo tunalifahamu na ni la fulani na tutalisimamia afanye kazi ya kulima tu na kulipa deni, watu watauziana mashambani huko huko ardhi yote itakwisha. Serikali za Vijiji ndiyo zenye mamlaka ya kusimamia hizi ardhi. Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alizungumza kwamba, hakuna ardhi iliyo tupu. Kila ardhi imepakana kati ya Kijiji na Kijiji, Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa, sasa tusije tukaona milima imeuzwa. Tutakuja kukuta hata ile milima ya Uluguru imeuzwa. Watu wako milimani kwa sababu sasa ukipata hati tu ya ardhi unakwenda kwenye mkopo, watu watauziana milima huko. Tunaomba Vijiji vihusike kikamilifu katika suala la hati na ardhi.

Mheshimiwa Spika, bila kusema naunga mkono hoja itakuwa si kweli. Naunga mkono hoja, lakini napenda kusema kwamba, haya niliyoyazungumza yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na timu yake na pia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pongezi hizi ziende pamoja na kuzingatia haya niliyoyasema. Mambo mazito hapa ni kwamba, kwa mfano, sasa hivi tunazungumzia *Anti-Dumping,* tumesema tupunguze namna ya kuagiza *material* kutoka nje, *material* yote tulime humu. Sasa kama ardhi itauzwa ovyo ovyo hivi na kushikwa na mtu hiyo *Anti-Dumping* itakuwa kubwa kweli kweli. Kwa mfano, sasa viwanda vinavyotengeneza unga wa ngano tunasema viwezeshwe na Wizara ya Kilimo kwa maana ya mikopo hii hii na ardhi hii, walime ngano, viwanda vibadilike visage ngano ya hapa ndani. Viwanda vinavyotengeneza sukari vilime miwa, miwa isagwe ya hapa ndani tutengeneze sukari. Mafuta hali kadhalika pamoja na nguo. Sasa kama tutaiacha ardhi iondoke, hayo yote yatakuwa hakuna cha *Anti-Dumping* wala nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nisingependa kengele ya pili inigongee. Nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii uliyonipa. Napenda kuanza kuwapongeza Wabunge wote ambao tumewachagua kwenye Bunge hili kwa ajili ya kutuwakilisha katika Bunge la Afrika na wengine kwa ajili ya kutuwakilisha katika Bung la *SADC.* Lakini vile vile, napenda kutanguliza kheri ya mwaka mpya kwa wote kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika kikao hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi wangu kwa sababu Serikali ipo hapa na inasikia, napenda kurejea kukumbusha tu kwamba, mwaka huu kule kwetu kuna njaa. Napenda nitumie nafasi hii kabla sijaingia kwenye mchango kuiambia Serikali mwaka huu tuna njaa na ni kweli sisi hatuna mazoea ya kuomba omba chakula, lakini mwaka huu tuna njaa, tena njaa kweli. Kwa hiyo, naomba Serikali isikie, ichukue hatua za haraka na kutahadharisha kabisa kwamba, kwa hali ilivyo, kwa jinsi mvua inavyonyesha hata mwakani kutakuwepo na njaa vile vile katika maeneo yote ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi.

Hii Sheria ya Ardhi nashukuru imekuja kama Serikali ambavyo imeileta. Kwa muda mrefu wakati ule tukiwa katika mfumo wa ujamaa, tulikuwa tukisema ili tuendelee tunahitaji vitu vinne ambavyo ni ardhi, siasa safi, uongozi bora na watu. Katika kuzungumzia Sheria hii ya Marekebisho ya Ardhi ya sasa, naamini sasa ni wakati muafaka Watanzania tukachukua hatua ya kutumia ardhi yetu. Ningependa kuiambia Serikali kwamba, nayo ichukue hatua ya kuwawezesha Watanzania hawa ambao tunasema ili waendelee wanahitaji kuwa na ardhi, waitumie ardhi katika kujiondolea umaskini. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, Serikali itumie Muswada huu wa marekebisho kwa kuitumia ardhi, lakini kwa kuwalenga Wananchi wa Tanzania wenyewe hasa wakulima wadogo wadogo vijijini ambao walikuwa hawana namna nyingine ya kukopeshwa katika kujiendeleza na kilimo chao. *(Makofi)*

Katika dira ya kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025 inalenga kuwaondolea Watanzania umaskini na lengo kubwa ni kuinua hali ya kilimo. Mimi nilikuwa nataka kutoa rai kwa kutumia sheria hii ya ardhi, Serikali iwape dhamana wananchi kuitumia ardhi kwa ajili ya kujikopeshea pembejeo, kwa ajili ya kujikopeshea matumizi ya kuondokana na kutumia jembe la mkono. Ili tufike katika lengo la mwaka 2025 kama bado tunalima kwa jembe la mkono, bado hatutafikia azma ya kuondoa/kufukuza umaskini ifikapo mwaka 2025.

Ninapendekeza kuwa sheria ya marekebisho wakulima wetu waweze kukopeshwa zana mbalimbali za kilimo kama majembe ya kukokotwa na wanyama, au matrekta madogo madogo *(power tillers)* waweze kukopeshwa mbolea na pembejeo mbalimbali kwa wale wakulima ambao wanatumia zaidi mbolea. Kwa mfano maeneo ambayo tunatoka sisi Kanda ya Magharibi wakulima wengi wanatumia mbolea hasa kwa kilimo cha tumbaku, lakini wanakopeshwa mbolea hii na makampuni yanayonunua tumbaku. Kwa sababu umekopeshwa na makampuni yanayonunua tumbaku ni lazima hata kuuza, uuze kwa masharti yale yale na riba yake ni kubwa, unauza pale pale kuliko kuzingatia soko huria. Kwa hiyo, mimi nadhani kwa sheria hii wakulima wetu sasa waitumie na Serikali iwarahisishie kupata mikopo hiyo, ili waweze kufaidika na kuinua kilimo chao kwa ajili ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nilitaka kulisema katika maboresho ya sheria hii ni kwamba wasiwasi wangu mkubwa ni katika maeneo ambayo vijiji vimefuatana na wakulima pamoja na wafugaji. Miaka nenda miaka rudi wafugaji na wakulima wamekuwa wakishirikiana vizuri tu bila matatizo hasa katika maeneo yetu, yanatokea matatizo ya hapa na pale yanatatulika. Lakini mimi napata wasiwasi mkubwa kama tutapitisha sheria hii ipite na wapo wajanja wanaweza wakatumia nafasi hii ya kuchukua maeneo yanayotumiwa na wafugaji na yakawekwa katika rehani. Kwa kawaida mifugo huwa tunachungia mahali popote. Kuna mabonde ambayo ni mazuri kwa kuchunga na kuna mabonde ambayo kuna malambo. Mimi jana nilisikitika baadhi ya Wabunge, ambao wanatulaumu sana sisi Wasukuma na Wamasai. Siyo vizuri kulaumiana kiasi hicho, kila kitu kibaya mnasema Wasukuma, kila kitu kibaya Wasukuma wamefanya hivi, Wamasai wamefanya hivi, hapana! Ni jinsi ambavyo utaratibu ulivyokuwa. Mahali ambapo huna malambo na una mifugo, una ng'ombe mkulima au mfugaji wa mifugo hawezi akakubali ng'ombe afe wakati anasikia mahali pengine kuna malambo au maji au majani. *(Makofi)*

Sasa kwa sheria hii mimi nilikuwa naomba iwekwe bayana kabisa mahali ambapo pamewekwa sehemu ya kuchungia mifugo, kuna malambo, pasitumiwe kama dhamana, pasitumiwe kuwekeza au kufanya hatua yoyote isije ikatokea tafrani kati ya wafugaji, isije ikatokea tafrani kati ya mwekezaji yule aliyechukua eneo hilo, kuwafanya wenye mifugo waweze kuhangaika mahali pa kuchungia, mahali pa kunyweshea na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli ardhi ni yetu sisi wote, Mwenyezi Mungu alitujalia akatupa sisi wote lakini vile vile ni kweli amewapa na viumbe nao wana haki na ardhi hii. Hivyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aliseme bayana na ingewezekana aweke katika kanuni, inaweza ikawa ni tabu kuweka katika sheria basi aweke katika kanuni kukataza maeneo ambayo ni ya malisho, maeneo ambayo ni ya kuchungia, maeneo ambayo ni ya malambo yasiwekewe dhamana kabisa na yasikopeshwe wala yasije yakauzwa kwa sababu ya faida ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nilikuwa nataka kuzungumza katika Muswada ni thamani ya ardhi. Hapa tunazungumza thamani ya ardhi kwa kijumla. Lakini ardhi hii imekuwa inabadilikabadilika kutokana na sehemu ulipo. Unaweza ukathamanisha thamani ya ardhi ya Dodoma ikawa ni tofauti sana na thamani ya ardhi ya Dar es Salaam au ya Mtwara au ya Mwanza na kadhalika. Lakini mimi nilikuwa nasema, hilo halitoshi, ni wakati muafaka sasa umefika thamani ya ardhi tuithamanishe na thamani ya ardhi iliyopo hata chini kwa maana ya sehemu ambayo kuna madini. Tunathamanisha thamani ya ardhi kwa sababu tunaangalia tu eneo la juu, eneo la miti, eneo lenye nyumba, lakini ebu tufikie mahali ambapo tunazungumzia thamani ya ardhi hata ya mtu anayekalia madini pale chini. Hii imfanye awe na haki ya kuingia ubia na yule anayekuja kuwekeza, kuvuna yale mazao ambayo yako chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi tutawakomboa wananchi wetu ambao mara nyingi wanakuja kupewa *compensation* ndogo sana kwa kuthamanishwa na thamani ya kile kilichoko juu ya ardhi peke yake bila kuzingatia thamani ya mali iliyopo chini ya ardhi kwa maana ya madini. Mimi nilikuwa natoa pendekezo katika marekebisho haya, basi tukubaliane thamani ya ardhi vile vile na madini yaliyoko nchini yawe ni dhamana, yamwezeshe mmilikaji wa eneo hilo aweze kuingia ubia, aweze kuingia hatua ambayo itamfanya na yeye awe na sauti katika maeneo ambapo kutakuwa na migodi na kuchimba madini ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka kulijua katika marekebisho ya Muswada huu ni namna gani tafsiri ipo katika kuthamini ardhi hii. Je, inafuata kama vile ambavyo inavyothaminiwa

nyumba kwa maana ya uhai wa dhamana yenyewe? Au uhai unafuata *write up* ambayo ameipeleka mkopaji? Maana yangu ni kwamba huyu anayemiliki ardhi kwa sababu ya kukopa anaruhusiwa kumiliki kwa miaka 33, miaka 90 au ni muda gani, au ana miliki kwa jinsi ambavyo ameandika mchanganuo? Mimi nilikuwa napendekeza kwa sababu haki miliki kwa muda mrefu wa miaka hiyo ya 33 nakadhalika, kunaweza kuwa na mabadiliko makubwa ya kuhitaji ardhi hiyo. Mimi nilikuwa napendekeza ardhi imilikishwe kwa kufuata mchanganuo ulivyoandikwa. Ukifuata mchanganuo ulivyoandikwa na kwa kuzingatia Serikali zetu za vijiji kwa kuzingatia matumizi ya ardhi, basi itakuwa ni rahisi hata kuikomboa ardhi hiyo kwa kutumia namna ambavyo mchanganuo jinsi ambavyo umeandikwa kuombea pesa zile. Mimi sina matatizo ya namna pesa ambazo zingeweza kutumika kwa sababu anapokopa anachukua kama dhamana.

Kwa hiyo, hiyo dhamana anaweza akatumia chochote, siyo lazima atafanya pale pale anaweza akachukua dhamana akaenda kufanya kitu kingine mahali popote pengine. Hilo sina tatizo. Lakini tatizo langu ni muda wa maisha ya ardhi ambayo imethamanishwa.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa napendekeza katika kanuni atakazoandika bwana Waziri suala la wakopeshaji wale wanaokopesha liwe suala la muhimu sana. Aangalie mabenki ya kizalendo ya hapa nchini, ndiyo yawakopeshe wananchi wetu. Kwa nini? Kwa sababu tukikukubali tu kila benki iende kuwakopesha wananchi, hapo ndipo utakuwa mwanzo wa kuuza ardhi ya wananchi wa Tanzania wanavikijiji ambao uwezo ni mdogo sana. Haya mabenki makubwa makubwa sana ya kimataifa inawezekana yakapata mwanya wa kuingia mpaka kule. Mimi napendekeza benki ambayo itumike ni benki ambayo ina mkono wa Serikali. Kwa maana hiyo, ningependekeza kama siyo *CRDB* basi *NMB* na benki zingine ambazo Serikali inaweza kuanzisha kwa ajili ya kuinusuru nchi hii isije ikauzwa kinyemela kwenda kwenye mabenki makubwa ambayo yana uwezo wa kimtaji, wa kiteknolojia na utalaam mbalimbali.

Lakini vile vile ningeomba Serikali iangalie riba ya mabenki hayo kwa sababu miaka ya nyuma kumekuwa na benki ambazo zilikuwa zinakopesha wafanyabiashara wanaweka thamani za nyumba, lakini mara nyingi kwa sababu riba ni kubwa kulingana na biashara waliokuwa wakifanya wanashindwa kulipa matokeo yake nyumba inauzwa. Sasa nyumba si kitu kikubwa kama ardhi. Ardhi ikienda hapo ni kilio cha jamii nzima, ardhi ikienda ni kilio cha watoto, ni kilio cha wajukuu, ni kilio cha kijiji kizima. Mimi nilikuwa naomba Serikali izingatie sana riba ambayo itatozwa na mabenki kwa wakulima wetu ili iwe ni riba inayokopesheka, lakini iwe ni riba inayolipika vile vile. Haiwezekani ukawa ni mkopo tu lakini ukawa ni kiini macho cha kuhatarisha ardhi ikachukuliwa na watu wa nje kwa sababu wanakijiji watashindwa kulipa riba ambayo imewekwa na mabenki hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nilikuwa napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri tafsiri hii ambayo inakuwepo kwa kiswahili na kwa sababu jambo hili linahusu wanakijiji, wananchi wa kawaida ipelekwe haraka sana, ili wanakijiji na wananchi ambao wana hamu ya kupata mkopo, wana hamu ya kukopeshwa, wana haja ya kujiendeleza kujiondolea umaskini iweze kutafsiriwa na mimi ningependekeza wangeipeleka ngazi ya tarafa, ngazi ya kata na kama itawezekana basi wapeleke ngazi ya kila kijiji kwani sasa hivi tunao Watendaji wa Vijiji, tunao Maafisa Maendeleo wa Jamii katika vijiji mbalimbali ambao wataweza kusoma na kuwaelewesha wananchi wetu namna nzuri ambayo wanaweza kukopa kwa kutumia raslimali hii ya ardhi kwa manufaa ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie katika Muswada wa sheria wa kufanya mabadiliko katika sheria ya ardhi *(Land Amendment Bill 2004).* Pili, nikutakie wewe heri ya mwaka mpya pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri na Wabunge wenzangu niwatakie heri na fanaka ya mwaka huu 2004. *(Makofi)*

Tatu, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge na pia niwapongeza Waheshimiwa tuliowachagua kutuwakilisha katika Bunge la Afrika na mwisho nimpongeze Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuweza kuchaguliwa kutuwakilisha katika *SADC Parliamentary Forum. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda kuchukua nafasi hii pia kuchangia katika Muswada uliko mbele yetu. Mengi mazuri yameongelewa na Wabunge wenzangu kuhusu dhamana ya ardhi katika kuwapatia nafasi yetu wananchi ya kupata mikopo na kuondokana na umaskini. Naheshimu sana na kuthamini michango yao na sitapenda kurudia mengi ambayo wameongea. Mimi ninayo matatu ya msingi.

La kwanza, ni sheria hii ya sasa kuangalia nyuma katika mapungufu ambayo yamekuwepo katika matumizi ya ardhi. Kumekuwepo na migogoro mingi ya wafugaji na wakulima kwa sababu ardhi yetu haikuwa na *land use plan.* Kwa hiyo, tunapoingia sasa mahali ambapo ardhi sasa inakuwa na dhamana ya kupatia chochote nafikiri wimbi la migogoro hii itashamiri zaidi. Kwa hiyo, kabla sheria hii haijaanza kutumika Waziri angeangalia nyuma kwamba kwa nini pamekuwepo na migogoro kati ya wafugaji na wakulima? Kumekuwepo na migogoro kati ya vijiji na vijiji. Kijiji kimoja na kijiji kingine kinapambana juu ya mpaka kwa sababu Serikali ilisimamisha upimaji wa vijiji na idadi ya watu imeongezeka. Kama idadi ya watu imeongezeka maana yake na mahitaji ya ardhi yameongezeka. Kwa hiyo, watu wamekuwa wakihama kijiji kimoja kwenda kijiji kingine na hatimaye imeleta migogoro kati yetu sisi. Hilo nalo lingeangaliwa maana sasa tunaingia katika hali ya kutumia ardhi kama sehemu ya kupatia mikopo na watu ambao watakuwa wanatoa hati miliki ni uongozi wa Serikali za vijiji. Kwa hiyo, lazima hilo likaangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nichukue sehemu moja ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu katika enzi hizi kule katika vijiji wananchi wangekuwa hawawezi kupata ardhi kwa ajili ya kuweza kupatia mkopo huko vijijini kwa sababu mabenki yalikuwa hayakubali dhamana ya ardhi au hata ya nyumba. Lakini sasa kwa Muswada huu kuletwa nafikiri itawapa wananchi wetu vijijini nafasi ya kuweza kukopa wale ambao wana uwezo. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri aangalie huko nyuma ili wakati huu sheria itakapoanza kutumika haya mapungufu yakaondolewa.

Sisi tunaamini maisha ya mwanadamu yanategemea ardhi, maisha ya mifugo ya yanategemea ardhi, maisha ya ndege yanategemea ardhi. Kwa hiyo, hii sheria ikaangalie uwiano mzuri isije ikasahau kwamba ardhi ambayo inakwenda kuwekezwa vile vile inatumika kwa matumizi ya mifugo.

Nitatoa mfano mdogo kuhusu umuhimu wa mifugo. Bwana mmoja aliozeshwa akapata watoto wawili, siku moja balaa ikaingia, mtoto wake akapata akafa ghafla wakati anacheza na wenzake. Sasa baba zake walipokuja kumhani wamemaliza kuzika wakamwuliza mtoto amekufaje? Akaeleza, mtoto alikuwa anacheza na wenzake ghafla ameanguka amekufa. Yule baba mkwe akamwuliza mkwewe, hapa ndani kwako unafuga kuku? Akasema hapana. Unafuga mbuzi, akasema hapana. Unafuga kondoo Vile vile akasema hapana. Akaendelea unafuga mbwa, akasema hapana. Unafuga paka aakasema hapana. Akamwambia, "Mwanangu umeua mtoto wako mwenyewe. Kifo kingeangukia wapi kwa sababu hata kuku huna, hata paka huna?" Kwa hiyo, wakati huu tunapoongelea ardhi tusije tukasahau nafasi ya wafugaji kwa sababu ufugaji nao una nafasi katika maisha ya Watanzania, kwa sababu bila ardhi hata mifugo haiwezi kupata malisho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, ambayo ningependa kuchangia ni sehemu ya huu Muswada kuwa sehemu ya kupatia mikopo ili kukuza uchumi wa wananchi wetu na kuwasaidia kuondokana na umaskini. Inakuwa ni kianzio cha maisha. Sawa sawa na mtu anakwenda kwenye klabu ya pombe kama hana kianzio hana sababu za kuingia. Sasa isije ikawa tunawaingiza Watanzania pale na kianzio na hana cha kumwendeleza. Tutakuwa tunakwenda kuwabamiza, tunawaingiza Watanzania kichwa, kichwa tunawapa nafasi ya kukopa, baadaye wananyang'anywa ardhi, wanakuwa watumwa, tunakuwa vibarua. Kwa hiyo, ili Muswada huu uweze kuwa na maana ya kiuchumi kwa wananchi wetu ni muhimu kukawepo na chombo cha kuwaelimisha wananchi. Muswada hauelekezi ni nani atahusika na kuwaelimisha wananchi, siyo Wizara wala siyo mabenki. Mabenki hayakubali dhamana ya kuwaelimisha wananchi na Wizara haikubali hiyo dhamana, sasa chombo gani kitawaelimisha wananchi? Lazima kitafutwe. Kuna sehemu ambapo wananchi wetu wamekopa fedha wakakimbia nyumba zao, akakimbia mke na watoto mkopo wa fedha tu. Sasa sembuse hii ya ardhi watakimbia wakakosekana. Kwa hiyo, hilo la kwanza likaangaliwe vizuri wananchi wakaelimishwe.

Lakini la tatu, muhimu kuhusu ardhi nafikiri hili litaendana na utaratibu ambao Serikali italeta Bungeni hivi karibuni. Mimi niipongeze Serikali kwa makusudi kabisa kwa kuwa na lengo la kuwapatia

Watanzania vitambulisho ili kujua, nani atakuwa na haki ya kupata ardhi. Hivi sasa katika nchi yetu nina taarifa za kuaminika kule katika sehemu za Matombo, Mkoa wa Morogoro, wanatoka watu nchi za jirani wanakwenda pale wanamnunua mtu na nyumba yake ya nyasi na shamba wanachukua. Watu wametoka nchi za jirani hawana uraia. Lakini kwa sababu Mtanzania huyu ana shida anauza kibanda chake na shamba kwa ajili ya shida kidogo anaondolewa aende akatafute eneo lingine. Sasa Muswada huu usije ukawa umefungua mwanya wa wageni wakaja hapa kwa sababu eti kuna utandawazi. Nadhani utandawazi hauendi mpaka kwenye ardhi, hatuwezi tukaweka ardhi yetu, kama sehemu ya utandawazi. Ardhi ni mali ya Watanzania. Watakaokuwa na haki ya kupata hiyo ardhi lazima wabaki Watanzania wenyewe. Kwa hiyo, suala la uraia ni muhimu sana kama lilivyo suala la vitambulisho.

Kabla Serikali kuleta hapa Bungeni utaratibu wa vitambulisho, mimi nilianza kuunga mkono kwamba ni muhimu Watanzania wakapewe hati za utambulisho, kwamba wao ni raia wa nchi hii, ili wawe na haki zote siyo katika kuchagua Serikali tu inayokuwa madarakani, lakini hata katika kupata huduma za nchi hii. *(Makofi)*

Wako watu wengi wageni wanapata huduma za nchi hii, bila kuwa na uhalali na Watanzania wale wenye uhalali wa huduma ya nchi yao wanazikosa. Sasa tunapitisha Muswada huu kwa maslahi ya Watanzania wenye uraia na haki ya nchi hii, siyo kwa ajili ya wageni ama mtu yoyote mpita njia. Mtu anapita njia anakuta Muswada huu umepita anaona ndiyo nafasi ya kujipatia akafikiri sisi tumelala usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu katika kifungu cha 113 (5) (b) cha Muswada *a deposit of any of the following;*

(i) *A certificate of a granted right of occupancy;*
(ii) *A certificate of customary right of occupancy;*

Hapa ndipo mimi nina sababu kabisa pa kupaongelea. Wale watu wanaomilikishwa ardhi kijadi sasa hivi kuna haki za akina mama, dada zetu katika familia moja kuna watoto wa kike na wa kiume, lakini mara nyingi katika kurithisha hii ardhi ya familia, inatokea inarithishwa kwa vijana wa kiume tu. Sasa wa akina mama walikuwa wamekaa kimya kwa sababu walijua ardhi ile inabaki kwa ajili ya shamba na labda baba alifariki akaacha shamba halina kitu cha maana.

Lakini sasa itakapofikia kwamba ardhi hii ni kwa ajili ya kutafutia fedha ya mkopo, kwa ajili ya kuwekeza wa akina mama lazima watakuwa na haki za kudai. Ningeomba Mheshimiwa akaliangalie kwamba kuna sheria za ndoa sawa sawa. Lakini tunapoongelea habari ya kurithisha mali ya familia ardhi italeta mgogoro hivyo nalo likaangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe la mwisho kuhusu tahadhari ya kuchukua kabla sheria hii kutumiwa. Muswada unasema kwamba Viongozi wa Kijiji na Kata hasa kijiji watahusika na kutoa zile hati miliki. Lakini sasa hivi migogoro mingi ya ardhi iliyoko vijijini inatokana na uwezo mdogo wa viongozi wetu wa vijiji. Tumejiandaa vipi kwa uongozi wa vijiji? Wakati fulani tulikuwa na Mameneja wa vijiji katika utaratibu wetu wa Serikali, sasa hivi hawapo. Hatuna Mameneja wa vijiji. Kwa hiyo, viongozi wengi ambao ni makatibu ambao alikuwa anasema Waziri wa TAMISEMI wamekosa watu wa kuajiri kule wenye uwezo, wengi walioko katika ajira ambayo ndiyo watakaohusika na hizo hati miliki ni watu ambao uwezo wao ni mdogo.

Kwa hiyo, ningeomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI wajenge uwezo wa kutosha wa viongozi wa vijiji kwa sababu ndiyo watakaokuwa na dhamana ya kutoa hati miliki na hawa viongozi wapewe darasa au elimu ili waelewe wanachokifanya. Suala la ardhi ni suala la kitalaam. Sasa hivi huko vijijini wanagawa ardhi ovyo ovyo anaambiwa wewe nimekugawia hapa mpaka kule lete hela, wewe hapa mpaka pale au kule lete hela. Wewe hapa mpaka wapi sijui leta hela. Hali hii italeta mgogoro. Wizara ikalingalie tena kwa makini sana kuhusu viongozi ambao watahusika na hati miliki huko vijijini.

Vile vile ningefikiri Wizara ijiandae kuweka mipaka ya vijiji, tulikuwa tumesimamisha kupima vijiji sasa vipimwe, tuwe na *land use plan,* tunajua sehemu hii ni ya wakulima hii ni wafugaji, hii ni ya makazi ya watu wizara ijiandae kwa hilo.

Pia, kuhusu Watanzania wenyewe na ardhi yao. Watanzania wangapi sasa wana *access* na hii ardhi? Wangapi wana ardhi? Sasa hivi tunapoongea kuna Mtanzania ambaye hana hata ardhi, hakuona umuhimu wa ardhi. Sasa hivi baada ya sheria hii kupitishwa kila mtu atataka kumiliki ardhi kwa shamba au kwa makazi au kwa ufugaji.

Sasa hili nalo linaweza likaleta mgogoro mtu akasema mimi nilizaliwa hapa kama suala lile la Waisrael. Watu wataanza kurudi kutafuta hiyo ardhi maana imekuwa na thamani. Mheshimiwa Waziri aangalie na ajiandae kwamba sheria iweke vipengele vya kuweza kulinda hilo eneo. Nina imani kuwa kama Wizara itachukua hiyo tahadhari, itakuwa imeweza kujenga nafasi nzuri ya hii sheria kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutuletea hii sheria kwa wakati muafaka, wakati huu wananchi wetu tunataka waondokane na umaskini. Mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu ulioko mbele yetu. Kwanza nimpongeze Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa jinsi walivyotuletea Muswada huu mbele yetu ili tuweze kuujadili na kuona umuhimu wake.

Pia nichukue nafasi hii kuwatakia heri ya mwaka mpya Wabunge wote na wananchi wote wa Tanzania na kuwatakia afya njema viongozi ambao wanaumwa.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu juu ya Muswada huu ni hasa kule vijijini. Muswada huu ni mzuri kama wananchi wetu watapewa elimu ya kutosha juu ya kujua umuhimu wa ardhi. Lakini Muswada huu utakuwa hauna maana kama wananchi wetu hawatapata elimu ya kutosha juu ya kujua maana na hali ya ardhi na umuhimu wake.

Nasema hivyo kwa sababu kule vijijini Wabunge wenzangu wengi wamesema kuhusu kule vijijini kwamba inawezekana kabisa madaraka tukawapa wanavijiji au Wenyeviti wa Vijiji kusimamia Muswada huu au sheria hii wasiweze kumudu. Sasa wasiwasi wangu unakuja kwamba wazee wetu zamani walikuwa na maeneo makubwa na walikuwa wanaweza kuoa wanawake wawili watatu mpaka watano kwa kujua kwamba yale maeneo ndiyo watakayoweza kuzalisha na kupata huduma zao.

Sasa wasiwasi nilionao ni kwamba je, ni kweli kwa Muswada huu utasaidia na kweli kutakuwa hakuna ugomvi kati ya familia na familia? Maana yake sasa ni Muswada ambao kila mtu unamgusa kama viongozi wengine walisema hapa kwamba Muswada huu usipoangaliwa utatuletea matatizo. Lakini ni Muswada muhimu na ni mzuri kwa sababu sasa unawapa nafasi wananchi wetu kuweza kujipatia kipato ili kuondoa umaskini wao hasa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni kitu cha msingi, lakini sisi Watanzania zamani tulikuwa hatujajua umuhimu wa ardhi japo tulisema kwamba ardhi ni mali ya Serikali na ni mali ya wananchi ni kweli, lakini sheria hii, ilitakiwa iletwe mapema na kufanya maandalizi ambayo yangeweza kutusaidia. Lakini sasa hivi ni kweli tumechelewa lakini naamini kwamba tukitoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu, wataona umuhimu wa kuwa na ardhi.

Mheshimiwa Spika, labda nizungumze suala lingine ambalo nina wasiwasi nalo pia. Mimi nadhani kungekuwa na kiwango maalum cha kutoa ardhi kwa mtu anayeweza kuhusika kwa sababu nimeona dalili mbaya, kwamba baadhi ya watu wamehodhi ardhi ma - eka kwa ma-eka na hawawezi kuitumia mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni kule kwangu, Waheshimiwa wengi wanatolea mifano maeneo ya kwao, mimi ninaye mtu mmoja ambaye anaitwa Amadoli. Amadoli amehodhi ardhi karibu zaidi ya hekta 5000, toka amechakua ardhi hiyo ni zaidi ya miaka 20 sasa ardhi imekaa haitumiki na wananchi sasa maeneo yale hawaruhusiwi kupita na ardhi imekaa imekuwa msitu.

Leo hii kwa sheria hii tunayopitisha inaweza ikaleta ugomvi mkubwa kama huyu mtu hataangaliwa kama ardhi alipewa kwa nia gani na kama alipewa kwa nia ya kuwekeza basi nadhani hiyo ardhi ingetumika ili atumie. Lakini kama alinunua tu kama mnunuzi wa kawaida mimi nadhani Waziri/Serikali itamke hapa kwamba yule mtu siyo Mtanzania, itakuwaje.

Mimi najua yule mtu siyo Mtanzania, labda inipe maelezo kwamba huyo mtu ni raia na kama ni raia basi pia kiwango alichopewa cha ardhi ni kikubwa mno kwa sababu alinunua ardhi kwa wananchi sijui walifuata taratibu gani, lakini taratibu zote sasa hivi anazo, kwa sababu hati anazo.

Pamoja na kwamba alinunua ardhi kuna baadhi ya wananchi wangu ambao walimwuzia ardhi huyu bwana hawajalipwa mpaka leo na imekaa zaidi ya miaka 20.

Sasa haya ni matatizo yanayojitokeza wakati Muswada huu unapitishwa. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ukweli kwamba huyo mtu ni raia,? Kwa sababu Serikali inasema hatutamilikisha ardhi kwa mgeni. Sasa tujue kama huyo mtu ni raia na kama ni raia, basi tujue na kama sio raia kama alikuwa na nia ya kuwekeza, basi ni kitu gani alichowekeza. Kwa sababu kama ardhi amechukua zaidi ya miaka 25 na bado ardhi hiyo haitumiki, nadhani ni tatizo. Ni vizuri Serikali ingechukua jukumu la kumnyang’anya ardhi huyu bwana ili iwagawie wananchi ambao wako tayari kutumia ardhi hiyo katika kuondoa umaskini wao.

Mheshimiwa Spika, niliposema kiwango cha kumpa mtu ardhi, ijulikane kwa sababu ni vizuri kama atapewa hekta 5,000 au 10,000 tujue kama atatumia kwa kitu gani kwa sababu mtu mwingine anaweza akachukua hekta 20,000 lakini asizitumie kwa chochote. Itakuwa hakuna maana! Au mtu anachukua hekta zaidi ya 5,000 lakini asiwe na uwezo wa kuitumia ardhi hiyo, kutakuwa hakuna maana. Mimi nadhani kuwe na kiwango maalum kwamba mtu atakapopewa ardhi apewe kutokana na uwezo wake yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu suala la taratibu za kibenki. Mimi naamini kwamba kwa Muswada huu sasa na Benki pia wangebadilika. Kwa maana kwamba mtu anapokwenda kukopa Benki, tayari anakuwa na malengo ya kufanya biashara yake au ana malengo ya kulima. Lakini mtu anapokopa Benki utaratibu wake unakuwa ni mrefu kupita kiasi. *Let say* mtu ameomba mkopo leo hii, anakuja kupata mkopo baada ya miezi sita. Kwa hiyo, yale malengo aliyokusudia kuyafanya kwa kutumia ule mkopo yanakuwa yamepotea. Au kama ni mkulima aliyekuwa anasubiri mvua inyeshe, imenyesha na imekwisha, ina maana yule mkulima hawezi tena kulima na kuweza kuzalisha mazao yake. Sasa ni vizuri utaratibu huu uendane na utaratibu wa Benki kubadilika.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba kwa utaratibu huu watu wengi watapenda kwenda kuchukua mikopo Benki na kwa kweli kama utaratibu utakaokuwa unatumika ni huo mrefu, watu wengi wataathirika zaidi. Kwa hiyo, ningeomba huu utaratibu uendane na mabadiliko ya ardhi na sheria ya ardhi iwafikie na Benki wabadilishe utaratibu wao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, muda ule ambao wamesema ni siku 30 mtu asiporudisha mkopo, mimi nadhani watu wengi waumepigia kelele huo muda. Sasa ni vizuri Wabunge wengi tukarudia kusema na kusisitiza kwamba si vizuri. Nadhani huu utaratibu ungekuwa ni ule wa siku 90 au zaidi ikiwezekana kwa sababu mkopo unaweza ukasema unachukua mkopo kwa ajili ya kulima au kwa ajili ya kufanya biashara fulani, hiyo biashara bahati mbaya isifanikishwe vizuri, sasa unapofikia kuchukua ardhi kwa sababu ya kukosa kurudisha ule mkopo kwa muda siku 30 ni ndogo mno, hata ukiambiwa bwana sasa kama ulishindwa kurudisha mkopo kwa mwaka mzima, sijui kama unaweza kurudisha mkopo kwa siku 30.

Kwa hiyo, nilidhani utaratibu ungewekwa kwamba angalau mtu aongezewe muda kwamba bwana kama ulishindwa kufanya hivyo, basi rekebisha biashara zako angalau miezi mitatu kama wenzangu

walivyosema siku 90 ziongezewe ili mtu aweze kupata nafasi ya kuweza kurudisha huo mkopo. Kwa sababu bila hivyo, watu wengi ardhi zao zitauzwa na zitahondiwa na watu ambao watakuwa na uwezo tu wa kipesa na watu wa mabenki.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye utaratibu wa upimaji ardhi, mpaka sasa utaratibu wa upimaji ardhi una matatizo. Waziri anajitahidi sana kufanya marekebisho lakini nadhani bado unahitaji kufanyiwa marekebisho zaidi. Nasema hivyo kwa sababu, mtu kuja kukupimia ardhi yako inaweza kukuchukua hata mwaka mzima bado ardhi yako haijapimwa. Mlolongo wa mambo unakuwa ni mengi mno. Mara hiki bado, mara hiki bado, sasa unaweza ukajikuta hata mwaka mzima unapita ardhi yako haijapimwa. Sasa utakuwa na maana gani ya kuwa na wapimaji au wathamini wa ardhi? Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri hili suala angeliangalia kwenye Wizara yake, anafanya mambo mengi mazuri. Nadhani hili pia angeliangalia japo najua ni mfuatiliaji mkubwa lakini kweli hili pia aliangalie kwa sababu ardhi inavyotakiwa kupimwa ipimwe kwa muda mfupi ili watu waweze kutumia kwa nafasi waliyokusudia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kiwango cha watu kupewa ardhi kubwa na kushindwa kukimudu ni tatizo katika nchi yetu. Wabunge wengi wamepiga kelele na hiyo Serikali nadhani inaelewa na Serikali ina uwezo wa kuweza kunyang'anya mtu kama hawezi kutumia ardhi kama alivyokusudia. Sasa kinachoshangaza ni kwa nini ardhi hiyo mtu akae nayo miaka 20 isitumike? Mimi nadhani, narudia kwa sababu naona ni muhimu hili suala liangaliwe kwa urefu sana. Ni muhimu sana! Si kwamba namwandama tu Bwana Madori, lakini si Madori tu. Kuna maeneo mengine Mashirika yamechukua kwa mfano kule kwangu Mbagala kuna sehemu inaitwa kwa Zakiem au Kibulugwa, kuna maeneo watu wengi wamechukua.

Kwa mfano kuna Kiwanda cha *Cement* kilichukua eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha *Cement.* Eneo lile sasa hivi lina miaka karibu 30, lipo tu halijatumika. Hivi karibuni nilijaribu kuomba ili nilitumie, nadhani kuna utaratibu unakuja Mheshimiwa Waziri atakuja kuupata kwamba hilo eneo kama halitumiki basi naomba nilitumie kwa ajili ya maendeleo ya mambo ya jamii na mambo kadhaa katika eneo langu. Kwa hiyo hilo tuliangalie, kwa sababu mtu anapokuwa anahodhi ardhi kwa muda mrefu, kwa sababu ameshakuwa na hati huwezi ukamnyang'anya mpaka ufuate taratibu za kumnyang'anya. Kwa hiyo, ni vizuri tutumie nguvu ya Serikali na Rais mwenyewe ana uwezo wa kubadilisha matumizi ya ardhi kutokana na mtu kama ameshindwa kutumia ardhi yake.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi ambayo nilikusudia kuyazungumza yameshazungumzwa, lakini nasisitiza kuwa suala la Vijijini, wale wananchi wa Vijijini nadhani ili waweze kufanikishwa na suala hili, wapelekewe elimu ya kutosha kwa sababu bila hivyo tutakuwa tuna matatizo, tutakuwa na ukiritimba ambao hautaleta tija katika marekebisho haya. Kwa kweli suala la elimu nasema ni muhimu kwa wananchi ili wajue umuhimu wa ardhi, maana ya ardhi na nini kinaweza kuwasaidia kwa kutumia ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wenzangu wanne wamezungumza kuhusu mifugo kwamba isije ikaonekana kwamba ardhi inagawiwa tu kwa watu wanaotaka kufanya shughuli zao na je mifugo itakuwa wapi? Mifugo ni moja ya raslimali katika nchi yetu. Wananchi wengi wanapenda kufuga, lakini kama itakuwa hakuna sehemu ya kufugia itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo tunarudia kusema kwa sababu ina umuhimu wake. Wabunge wengi wamesema na mimi nasema kwamba wakati tunagawa ardhi au tunarekebisha suala hili pia tuzingatie kuipa nafasi mifugo wafugaji sehemu ya malisho katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia.

Awali ya yote naomba niseme mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ambao ndio tuliopitia mapendekezo ya Muswada huu na kusomwa mbele ya Bunge lako na Mwenyekiti wetu. Kwa hiyo mimi naunga mkono hoja ya Muswada huu mia kwa mia. Ila nina mambo mawili ya kuongezea. *(Makofi)*

Kwanza, kama tunavyofahamu, nchi yetu ina jumla ya hekta karibuni milioni 48 zinazofaa kwa kilimo na katika hizi hekta karibu milioni sita ndizo zinazolimwa na wakulima wadogo wadogo na wafugaji wadogo wadogo. Wakulima na wafugaji hawa hawana utaalamu wa kutosha na hawana mitaji ya kutosha. Lakini naipongeza Wizara kwa kuweka kitengo cha *Tanzania Investment Centre* ambacho ndicho kitakachosaidia kujaribu kutafuta wawekezaji kuja katika eneo lile lingine kubwa la karibu hekta milioni 40 kuja kuwekeza katika kilimo. Hilo ni jambo zuri, naliunga mkono sana.

Lakini pamoja na kuunga mkono huko, nilikuwa nashauri tu kwamba Wizara ifikirie kitengo hiki shughuli zake na majukumu yake yajumlishe pia namna ya kuweza kuangalia jinsi uendelezaji wa hizo hekta karibu milioni sita ambazo sasa ndizo zinazotumiwa na wakulima. Vile vile naishauri Wizara, wakati *Tanzania Investment Centre* inamilikisha wawekezaji kutoka nje, iwe ina utaratibu wa kuona kwamba maeneo hayo yanayomilikishwa hayamilikishwi katika mikono michache ya watu wachache kwa sababu kitendo hicho kinaweza kupelekea nchi yetu kukosa maeneo ya kilimo na baadaye kusababisha nchi yetu kupata uhaba wa chakula, kama hawa wawekezaji badala ya kulima mahindi, wataamua kulima mazao ya biashara kama vile pilipili. Kwa hiyo, naishauri Wizara kwa maana ya kitengo hiki cha *Tanzania Investment Centre* wawe makini sana wasikiachie bila kuwa na utaratibu wa kuchunguza shughuli zao zinavyokwenda namna gani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuchangia, hili jambo limezungumzika, linahusu mkonge. Inaonekana yako mawazo ya kuitaka Wizara inyang'anye mashamba ya mkonge ambayo hayaendeshwi. Ni mawazo mazuri, lakini kwa maoni yangu wenye mawazo hayo wanachukulia mkonge katika mfumo wake wa zamani. Mfumo wa zamani ulikuwa unaendeshwa na wawekezaji wakubwa, mitaji mikubwa ambao sasa hawapo. Kwa hiyo, nawashauri waondokane na fikra hizo kwa sababu sasa mkonge miliki yake inawahusisha Watanzania wenyewe sio tena watu kutoka nje kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, nina mifano michache ya kutoa. Kwanza tuna shamba la Gomba Mwenga. Hili shamba sasa linaendeshwa na Mtanzania. Lakini vile vile iko Kampuni ya *Katani Limited* ambao wao mwelekezo wao ni kugawanya mashamba yao kwa wakulima wadogo wadogo ili kusudi wazalishe mkonge.

Katika jitihada hiyo sasa wana wakulima wadogo wadogo 2,100 na katika hao, wako wananchi wa kawaida, viongozi wa Kitaifa, viongozi wa kimkoa, viongozi wa kiwilaya, Tarafa, Kata hadi Vijijini. Hiyo kwa maoni yangu mimi, kwa uzoefu wangu mdogo katika mazao ya mkonge, naona ni hatua muhimu sana katika kufufua zao letu la mkonge Tanzania. Kwa ajili hii, nashauri sana kwamba Serikali najua pengine ni Wizara nyingine inayohusika, lakini kupitia kwako Mheshimiwa Waziri wa Arldhi, nashauri Serikali ifikirie kutoa hatimiliki kwa hawa wakulima wadogo wadogo ambao tayari sasa wamekwishapewa mashamba na *Katani Limited* maana tayari zipo hekta 3,200 za mkonge unaolimwa na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, napenda nieleze Bunge lako kwamba kutokana na uzoefu wangu mdogo, nchi ya Brazil, Mexico, nchi ya China sasa ndio wanaongoza katika uzalishaji mkonge duniani na hawa wanatumia mfumo wa wakulima wadogo wadogo. Sisi nina hakika tukitumia mfumo huo tutarudi katika enzi za miaka ya 70 kuwa ndio wa kwanza kuzalisha zao la mkonge duniani.

Kwa sasa hivi Mkoa wa Mara tayari wana hekta 48 zinazolimwa na wakulima wadogo wadogo. Kwa sasa hivi kama nilivyosema *Katani Limited,* kuna hekta 3,200. Kwa sasa hivi tayari Kituo cha Utafiti cha Mlingano kimeshaanzisha utaratibu wa kupata mbegu kwa njia ya *tissue culture* kinyume na tulivyozoea zamani kupanda kwa kutumia *bubilt 15.8.* Mbegu hizo zitaweza kupanua zaidi kilimo chetu cha mkonge.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua kuhusu mkonge ningeweza kuzungumza sana lakini kwa ujumla napenda tu niseme naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa sababu ndio hoja itakayotusaidia sisi Watanzania kuweza kuvuka hapa tulipo na kuweza kupanga mipango yetu kwa ajili ya maendeleo yetu kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Choya, atafuatiwa na Waheshimiwa Wabunge wawili ambao waliitwa jana lakini hawakuwepo ndani ya Ukumbi nao ni Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Beatus Magayane. Nitawaita kwa mpangilio huo huo. Mheshimiwa Choya.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie. Lakini awali ya yote kabla sijachangia naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe katika Kamati hii. Lakini kilichopelekea mimi nichangie angalau kwa kifupi ni mambo mawili tu.

Jambo la kwanza ni kuhusu mipaka, tatizo linalojitokeza kati ya mpaka wa Wilaya ya Bukombe na Wilaya ya Biharamulo. Hili suala ni tatizo la muda mrefu na tumeshalichukulia hatua zote zinazostahili, tumeshapeleka taarifa kunakostahili kwenye Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya TAMISEMI ili iweze kuunda utaratibu au Tume maalum ya kwenda kusimamia namna ya kuweka vigingi katika mipaka kati ya Wilaya ya Bukombe na Wilaya ya Biharamulo.

Lakini hili tatizo limechukua muda mrefu kiasi kwamba wananchi hawaelewi kinachoendelea na mpaka sasa hivi ninavyosema, kuna tatizo la wananchi kutokuelewa kwamba wao sasa wako chini ya uongozi upi; uongozi wa Wilaya ya Biharamulo au viongozi wa Wilaya ya Bukombe? Ni kwa bahati mbaya sana kwamba na baadhi yetu sisi wanasiasa huwa tunataka, wanasema mwamba ngoma ngozi huvutia kwake, kila mmoja anajitahidi kuvutia eneo liwe kwake. Sasa matokeo sisi tunawachanganya watu kiasi kwamba watu hawatuelewi na wanaanza kuichukia Serikali.

Nilikuwa naziomba Wizara mbili, yaani Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya TAMISEMI watuhakikishie wakati watakapokuwa wanafanya majumuisho kwamba ni lini utaratibu huo utafanyika kwa kuwatumia viongozi wetu wa Mikoa yote miwili, yaani Shinyanga pamoja na Kagera, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Wabunge wahusika ili ipangwe siku maalum kwa ajili ya kwenda kuondokana na tatizo hili. Halafu imekuwa ni mila na utamaduni kwa wananchi walio wengi Watanzania kwa kusaidiana na baadhi yetu sisi Wanasiasa kupigania mipaka ya ndani ya nchi.

Kwa kweli mimi sijaona mantiki. Wananchi hatupaswi kupigania mipaka ya ndani ya nchi kwa sababu nchi ni moja, Mkoa ni mmoja, lakini kutokana na *interest* ya baadhi yetu sisi tunashtukia tumeshawasababishia wananchi kuanza kuvutana wao kwa wao. Sasa naiomba Serikali kwa namna ya pekee ijaribu kujenga ule moyo wa kuipenda nchi, afadhali wote tukapiganie mipaka ya nchi na nchi kuliko kupigania mipaka ya ndani kwa ndani.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tena sana hizi Wizara mbili ziwasiliane ili tutakapomaliza Mkutano huu tutakaporudi twende na jibu kamili na wananchi waelewe kwamba ni lini watakapokaa pamoja waweze kuweka mipaka ambayo inaeleweka ili wananchi wasiendelee kuvutana wao kwa wao. Maana mpaka sasa hivi ninavyosema, kuna hujuma inaendelea kufanyika kwa sababu lile eneo lina misitu ya asili.

Kwa hiyo, watu wanahujumu kwa sababu hawajui wako chini ya uongozi upi. Kwa hiyo, kadri tutakavyoendelea kuwaruhusu kuishi bila kujielewa wako wapi, moja kwa moja hujuma itazidi. Mpaka sasa hivi watu wanachuma au wanavuna maliasili wanapeleka wanakojua. Hata hizi Halmashauri kutokana na kuvutana kwetu sisi kati ya Wilaya mbili, hizi Halmashauri hazifaidi kitu chochote. Kwa hiyo, kila mmoja anavuna anapeleka anapotaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kinachotakiwa, sasa hivi Mheshimiwa Waziri ambaye ameleta Muswada huu namwomba sana awasiliane na Wizara ya TAMISEMI tuhakikishe tumeondoka na jibu. Mheshimiwa mwenzangu Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Mashala na mimi, kinyume na hapa sasa mtashtukia kumeshatokea migongano. Kwa hiyo, naomba kwa namna ya pekee tuondoke na jibu.

Jambo lingine, tutakapoanza kutekeleza sheria hii, hebu tujaribu sana kuangalia maeneo ya Mikoa ambayo iko mipakani. Wameligusia wengi. Kwa taarifa tu, katika nchi yetu ya Tanzania Watanzania, wale wananchi wote ambao wana asili ya Utanzania ni wapole, ni waaminifu, hawana matatizo ya aina yoyote ile. Lakini mtu yeyote ambaye ana mashaka na uraia wake huwa ni mjanja kupindukia. Anaweza akapata vitambulisho vya kila aina ambavyo Mtanzania hawezi kuvipata maana atatumia kila mbinu kupata vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kagera, kwa taarifa tu, wenye vitambulisho, *birth certificates, marriage certificates,* kila aina ya kitambulisho hata kadi za Vyama mbalimbali, walionavyo na ambao wanatembea navyo ni wageni. Mgeni yeyote utakapomwuliza kitambulisho chochote kile atakupa, lakini sio Mtanzania mwenye asili ya Utanzania. Kwa hiyo, tutakapotaka aanze kutekeleza sheria hii, lazima tuhakikishe ile Mikoa yote ambayo iko mipakani, tumefanya uchambuzi wa kina ili tusije tukashtukia sasa wale wajanja wachache wenye hela; maana yake wale ambao wana vitambulisho wana hela kweli na wana uwezo! Kwa hiyo wanaweza kufanikisha kufanya kitu chochote kile ambacho baadaye kinaweza kikahujumu nchi.

Kwa hiyo, naomba tufanye kila liwezekanalo kuhakikisha Watanzania wenyewe ndio wanaohusika katika suala zima la utekelezaji wa sheria hii. Kinyume na hapo tutasababisha madhara yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi matatizo makubwa na mazito na ya pekee ambayo viongozi wa Mkoa wa Kagera wakiwemo kuanzia Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Mkuu wangu wa Wilaya na mimi nikiwemo ambayo tunakumbana nayo, ni tatizo la wafugaji. Kwa taarifa tu sisemi wafugaji wale ambao ni Watanzania. Wafugaji walio wengi wanatoka nchi za jirani, hasa hasa Rwanda.

Kwa kuwa wao kwao hawana sehemu za kulishia mifugo yao, ng'ombe wao wote wanawaleta kwenye mbuga zetu za kulishia. Sasa Mtanzania kwa kuwa yeye bado anategemea kilimo, ndio anayelishiwa mashamba yake. Akijaribu tu kulalamika, yeye anasema bwana mimi nitauza ng'ombe hata wawili, watatu nitakununua.

Kwa hiyo kilichokuwa kinatakiwa hata maeneo ya malisho lazima yawekewe mipaka siyo kwa kutangulizia kwamba wale wafugaji ambao kweli wanaeleweka ni wafugaji ambao ni raia, kweli wapewe kipaumbele maana yake sehemu ya malisho ni sehemu ya nchi yao.

Lakini wale ambao sio nchi yao wameleta tu mifugo, ikiwezekana hata wawe wanatozwa ushuru mkubwa kwa ajili ya kufidia wale wananchi ambao wanalishiwa mashamba yao. Kwa hiyo, katika kutekeleza sheria hii, lazima tuwe waangalifu sana kuhakikisha kwamba wale wafugaji kutoka nje wanatengewa maeneo na wanayalipia kwa sababu ndio waharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Waziri anayehusika na masuala ya mifugo akienda kule akapata malalamiko ya wananchi nafikiri atatuhurumia sisi tunaokaa kule kwa sababu kila mara ni migogoro ambayo haiishi. Kadri utakavyojitahidi kusuluhisha, wewe ndiye unayeonekana adui na kama mnavyojua kwamba maeneo ya pale sisi tuko katikati ya maadui; unachokisema chochote kile unafuatiliwa, unatafutwa kiasi kwamba labda unaweza ukashtukia umeshauawa bila kujifahamu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika kutekeleza sheria hii tuhakikishe tunaliangalia suala zima la uraia wa nchi hii na kama walionitangulia walivyosema, Maafisa Uhamiaji lazima washirikishwe kuanzia ngazi ya chini mpaka ya juu, vinginevyo tutakuwa tunaiuza nchi bila kujielewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri sana na ni Muswada ambao ni mgumu kwa sababu Muswada wowote unaozungumzia ardhi kwa kweli inafaa uangaliwe vizuri sana kwa sababu ardhi ndio uhai. Hatuwezi kuishi bila ardhi, hatuwezi kufanya biashara yoyote bila ardhi, wala hatuwezi kula bila

kuwa na ardhi. Lakini suala la ardhi nadhani tulilizungumzia sana mwaka 1999 tulipozungumza kuhusu *Village Land Act, 1999.* Nadhani wakati huo tulizungumza sana na tuliweka sheria.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea kwamba utekelezaji huo ungefanyika ndio Muswada huu uletwe Bungeni kwa sababu *Village Land Act,* tulisema kwamba Vijiji vyote vipimwe na vipate *certificate* na wananchi wajue ukubwa wa Vijiji. Ujue kwamba Kijiji hiki ambacho unakisimamia, wale ambao ndio *owner* wa Kijiji hicho wajue kwamba ukubwa wa Kijiji ni ukubwa huu, wawe na *certificate.* Mpaka sasa hili halikutekelezwa. Hakuna Kijiji chenye *certificate.*

Sasa unakuja unawaambia tena, huu Muswada unasema kwamba ni kuthaminisha ardhi iwe na thamani. Nakubali, lakini mwombaji atamwomba nani? Au Kijiji kitatoa ardhi kutoka wapi?

Yeye mwenyewe hana miliki kwa sababu hamna hiyo *certificate.* Sasa sijui labda nimwulize Waziri, ni nini kinachozuia *certificate* au upimaji wa vijiji haukupimwa mpaka leo. Hawana *certificate* mpaka leo. Kwa sababu cha kwanza ni hiyo, ndiyo uwezo ukaletwa Muswada huu, watu wakijua kwamba hapa ni eneo langu, hakuna. Jambo lingine nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia wafugaji. Mimi ni mfugaji na kwa kweli nisipozungumza suala la wafugaji kwa kweli itakuwa ni matatizo kwangu.

Kwanza napenda kusema kwamba wafugaji, kila siku wanalaumiwa Wamasai, Wasukuma sijui Wabarbaig, wamekuwa tatizo katika nchi hii na wanaonekana kana kwamba ni watu waharibifu. Lakini mimi nasema kwamba hawa watu, wafugaji nchi hii ni kama mtoto yatima ambaye yuko mbali na mzazi wake. Kwa sababu maeneo ya wafugaji yanavamiwa kila siku, yanavamiwa na wakulima. Katika Muswada huu, ardhi imeonyeshwa iwe na thamani, ndiyo watavamiwa zaidi. Kwa sababu mashamba, kuna maeneo ya wafugaji, malisho ya mifugo, wenzetu wanaona kwamba ni maeneo ya wazi ambayo hayatumiki, wanasema *open land, general land.* Sisi vijijini hatujui *general land* iko wapi. Mpaka sasa hatujui iko wapi na ni sehemu ya Muswada wa Ardhi. Ni kwamba maeneo ya malisho haya, hayo ambayo ndiyo malisho ya mifugo yao ndiyo mnasema *general land* ndiyo mnasema ardhi ambayo haitumiki, ndiyo mnasema ardhi ambayo haina mwenyewe na tunasema ndiyo maana hamuwapi *certificate* vijijini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi mkubwa sana kuhusu Muswada huu. Jambo lingine ni hizi gharama za upimaji. Gharama za upimaji nadhani ni watu wachache sana wanaweza wakagharimia, wakapima maeneo yao, hata kama umepewa. Ni gharama kubwa sana. Watu wanaoweza wakapima mashamba ni matajiri, ni hawa watu wa nje ambao ndiyo wanapora maeneo yetu. Ndiyo sasa wamehalalishwa. Jimbo langu liko mpakani, tunapakana na Kenya. Kenya, Muswada huu nadhani wao wamefanya muda mrefu sana, wamepitisha. Lakini kwa bahati mbaya sana maeneo yale yote ya wafugaji baada ya kupitishwa Muswada huu watu wamekimbilia, wamefika maeneo kuvamia kwa nguvu. Wafugaji wameuza maeneo na sasa wafugaji wa Kenya wamekuwa *squatters* hawana maeneo. Wanaanza kukimbilia Tanzania, maeneo yote, ukipita Kajiado mpaka Nairobi hakuna tena wafugaji. Imekuwa maeneo ya watu wengine sasa kila mahali na ilikuwa ni maeneo ya wafugaji. Ndiyo sasa na sisi tunakaribisha watu kutoka maeneo mengine, wamechukua maeneo hayo yote, yameuza na wamevamia kwa sababu Mahakama mnayotaja hapa kwamba Mahakama kwa kweli Mahakama ndiyo kimbilio la kila mtu. Ndiyo kimbilio la mnyonge, ndiyo kimbilio la watu. Ndiyo tunakimbilia kudai haki. Lakini hivi mtu ambaye hana uwezo anaweza kukabiliana na Mahakama. Mtu mwenye haki, umaskini unaweza ukamkimbiza, akakimbia akaacha haki yake hata kama ipo. Kwa sababu ya pesa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ardhi iliyopo ambayo Mheshimiwa Mwanri jana alizungumzia. Sisi tunapakana. Wale wafugaji waliokuwa akiwazungumzia ni kweli hivyo vijiji vyote alivyovitaja vipo na kuna vya kwangu vya jimbo langu ambavyo tunapakana, wanapata shida sana kutokana na ardhi. Kuna mashamba ya *NARCO, NAFCO* yaliyoko pale, ambayo ni mashamba ya zamani ambayo hayatumiki tena. Tunaomba Serikali wakitoa uamuzi waangalie sana wananchi walioko katika maeneo hayo katika jimbo langu la Longido na jimbo la Siha. Kwa sababu hawana maeneo kabisa, tegemeo lao ni hapo, kabla Serikali ilipokuwa ikitumia mashamba hayo ilikuwa ni mgogoro kila siku, watu wanakamatwa wakitumia kwa malisho, kwa kilimo na mpaka sasa wapo.

Tunaomba Serikali itakapochukua hatua ya kutoa eneo hilo waangalie wananchi walioko wanaozunguka katika mashamba hayo ili wapewe maeneo ya mifugo na ya mashamba.Hebu tuwaangalie watu wetu tusiangalie sana sana, hili niliona kwenye Muswada wanasema kwamba tuangalie sana wazawa. Mtu ambaye siyo mzaliwa, hahusiki na ardhi hii. Lakini sijui kama ni kweli. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, azingatie sana suala la wazawa hasa wananchi wanyonge walioko vijijini.

Mwisho, ningependa kuzungumzia gharama, Serikali iangalie gharama ya upimaji wa mashamba, viwanja na nyumba kwa sababu ni ngumu sana, ni gharama kubwa sana kwa mwananchi wa kawaida. Utaratibu huo uangaliwe upya kupata hati kwa mtu wa kijijini mpaka aje Dar es Salaam ni tatizo na kama Mheshimiwa Waziri unakataa katika majimbo yetu watu wanahangaika sana kwa sababu mpaka afuatilie hati Dar es Salaam. Kwa nini asipewe katika Mkoa wake? Mtu wa Longido kufuatilia hati Dar es Salaam ni gharama kubwa sana hakuna mtu anayeweza. Pale Arusha, kuna Wizara yako, wakubaliwe wapewe hati miliki pale pale Arusha baada ya kupitia taratibu zote siyo kufuatilia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea na naomba Mheshimiwa Waziri azingatie hayo. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu ulioko mbele yetu. Suala la ardhi ni suala muhimu sana na ni muhimu zaidi kwetu sisi Watanzania ambao asilimia kubwa ya wananchi wetu wanategemea kilimo na wanaishi vijijini. Kimsingi Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maudhui ya Muswada kama yalivyoletwa na Mheshimiwa Waziri na kwa kweli lengo ikiwa ni kumwondolea umaskini mwananchi wa kawaida kwa kutambua kwamba ardhi yake ndogo aliyo nayo ina thamani na kuwataka wale wenye mabenki au wanaoweza kutoa mikopo kuitambua kwamba ina thamani. Kwa hilo sina tatizo nalo. Lakini unapokuwa na ardhi ndogo ya mkulima umeshaiweka thamani kiasi hicho lazima pia utegemee matatizo makubwa kwamba yatakuja na ugomvi wa kugombea hiyo ardhi utaanza kujitokeza maana wengi wataanza kuona kwamba ardhi sasa ni pesa. Lakini tatizo kubwa linalojitokeza Mheshimiwa Spika, ni lile linaloitwa sijui ni Kiswahili safi ni kipi, lakini speculation, watu sasa wataanza kuona kwamba ardhi ina faida na wataanza kuhodhi maeneo makubwa kwa ajili ya faida yao ya kuweka kwenye mabenki au kuuza baadaye maana sasa ardhi tupu inauzwa na ina thamani. Sasa watu wataanza kuchukua maeneo ambayo hayana mwenyewe kimsingi na kuanza kuyageuza kuwa mali yao na hapa ndipo linapoanza kuwa tatizo.

Mheshimiwa spika, ningeshauri katika hili, kwamba kwa kuwa tuna Wizara iainishe kwanza matumizi mbalimbali ya maeneo mbalimbali ya ardhi *land use plan* ili ukisha kuwa na *land use plan* ama katika Mkoa au kwa nchi nzima, ndipo unapoweza kusema kwamba sasa ardhi inaweza kuuzwa. Lakini kama hujawa na land use plan tutakachokuja kujikuta, tutakuta kwamba Serikali kama Serikali mipango yake inakwama kwa sababu haitakuwa na ardhi na Serikali itabidi iende kununua ardhi kwa watu binafsi na hapo itakuwa ni hatari kubwa sana. Ukiangalia Kambi ya Lugalo ilipo, zamani ilikuwa ni porini sana. Leo iko mjini. Kwa sababu hatukuwa na *land use plan.* Kwa hakika tungejua kwamba pale patakuja kuzungukwa na wenyeji hii tungeipeleka mbali. Kwa hiyo, ni muhimu kabla ya yote kuwa na *land use plans* katika maeneo mbalimbali na hii itazuia *speculation.* Ukurasa wa tano Mheshimiwa Waziri anazungumzia *the sale of a right of occupancy,* kwamba *the sale of a right of occupancy without an extended improvement may be sold to a citizen of Tanzania.* Hiki kifungu kinaweka mwanya wa ardhi kuchukuliwa na watu wengine. Mimi ningesema kwamba isiwe *may,* bali tutumie neno *shall* na tuweke neno *only, to a citizen of Tanzania only.* Kwa sababu ukiacha nafasi ya mtu mwingine asiye Mtanzania kununua ardhi, ni kwamba tutajikuta hao wameshachukua maeneo makubwa na Watanzania wakabaki hawana nafasi. Lakini itakuwa ni hatari zaidi tutakapokuja kukuta kwamba hawa ambao si Watanzania watakuwa na maeneo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa ambapo Taifa litalazimika kwenda kununua sasa ardhi kutoka kwa hawa ambao si Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kwamba kwa sababu kuna *Tanzania Investment Center,* ambalo wameweka utaratibu wa kuainisha kile wanachokiita land banks, hawa ambao si Watanzania waelekezwe huko ambapo watatumia hizo *land banks* kwa ajili ya *investments* halafu kwa masharti maalum, ardhi ibaki bado ni ya Watanzania wenyewe. Hivi vishamba vidogo tunavyovizungumzia au mashamba ambayo yako katika maeneo ambayo wananchi tayari wanaishi basi yabaki ni kwa ajili ya Watanzania tu kuuziana huku kuwe kwa kati ya Mtanzania na Mtanzania na isiwe vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki ya Muswada huu ni kwamba sasa mkulima mdogo kishamba chake anaweza kukiweka rehani ili apate mkopo kwenye benki. Tatizo linalokuja kujitokeza kwanza kawaida shamba tupu, eneo tupu ambalo halijaendelezwa thamani yake huwa ni ndogo sana hata ukilifanyia *evaluation.* Lakini tutakuja ku-*create more problems,* tukidhania kwamba tunamkomboa huyu mwananchi wa kawaida mwenye kishamba pale atakaposhindwa kurudisha mkopo na ardhi yake kuchukuliwa na huyu mwenye benki au hii Taasisi iliyompa mkopo. Si mtu mmoja hapa atakayeumia. Ni familia, sasa lazima tuwe waangalifu kwamba kwanza tunatoa elimu kwa hawa wakopaji watarajiwa kwamba wanaelewa wanachokwenda kukifanya wanapotoa hii ardhi kama dhamana? Maana yake kama hatutafanya hivyo, tutaleta matatizo zaidi tukidhania kwamba tunawakomboa kwa kuwawekea hii sheria. Ni vyema kuwe na elimu ya kutosha kwa hawa ambao wanategemea kuja kukopa ili vishamba vyao vidogo visije vikachukuliwa na hivyo kubaki wakiwa hawana ardhi kwa familia nzima.

Pamoja na hilo, kifungu cha 127 kimetoa *notice* ya siku 30 kwamba mkopaji akishaambiwa na kupewa taarifa kwamba ame-*default* basi ardhi ile inaweza kuuzwa au ikatwaliwa. Ndiyo haya ninayoyazungumza kwamba ni vema wananchi wetu kwanza wakaelimishwa ni kipi wanachotaka kukifanya kama wanaelewa kweli. Na kama wakishaelewa siku 30 Mheshimiwa Spika, ni ndogo sana kwa mwananchi wa kawaida kwa sababu katika hizo siku hawezi kuhangaika kutafuta pesa za kulipa hili deni katika siku 30. Ni vema muda ukabaki ule ule wa siku 90 na kwa kweli hata inawezekana kuongezwa kwa sababu zile siku 90 walikuwa wamepewa watu waelewa kukopa na maana ya kukopa. Hivi sasa tunazungumzia mwananchi wa kawaida. Sasa ukimpa siku 30 maana yake umeshm-condemn tayari. *(Makofi)*

Kwamba wewe na familia yako ardhi yako sasa inachukuliwa. Ni hatari sana. Lakini sasa hivi ni kwamba hata kama atakopa kwa mfano *CRDB,* Makao Makuu ya *CRDB* yako Dar es Salaam, akikopa *NBC.* Makao Makuu yako Dar es Salaam, mpaka hii *notice* ifike kwangu kule Nyantukuza ninakotoka, kule Nyaronga, siku 30 hazitoshi na hata kama atakuwa na cha kujibu, au atakuwa anahangaika kwamba wafidie apate hizo pesa za kulipa katika hizo siku 30, itakuwa hazitoshi mpaka yule mkopeshaji Makao Makuu apate habari. Kwa hiyo, ni vema huo muda wa *notice* ukaongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 136 kinaweka utaratibu kwamba yule aliyekopesha anaweza pia kuwa mnunuzi wa ile rehani. Hii ni hatari. Kwanza ni *un ethical, interest* ya *banker* ni kuhakikisha mteja anarudisha ule mkopo aliokopa ili aweze kuendelea. Sasa tunapoweka kipengele kwamba hiyo ardhi yeye aliyekopesha anaweza pia akainunua inaleta mashaka na matatizo makubwa zaidi. Kwa sababu ikisha kuwa namna hiyo, inawezekana thamani ya ile ardhi, ardhi ikawa imewekwa chini makusudi na huyu anayefanya *evaluation* kwa kutamani ile ardhi ili baadaye atumie ujanja kuja kuichukua yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kwamba isiwe zaidi ya asilimia 25 chini ya *reserve price.* Lakini ni nani anayeweka *reserve price.* Lakini pia tunazungumza hata kwenye mnada, tunajua matatizo yanayotokea kwenye mnada kwamba ukishaongea na mnaendesha mnada bei inaweza kuwa chini ikakusaidia wewe ambaye unakwenda kununua. Sasa hiki kifungu Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwamba hii *possibility*, uwezekano wa mtu aliyemkopesha mtu kujiuzia yeye mwenyewe, huu utaratibu usiowezekane kwamba ni *un ethical* lakini pia kuna hatari ya wengi wakaja kutamani hii ardhi kwa kujua kwamba ile thamani ya ardhi ni kubwa zaidi kuliko ule mkopo halisi aliouchukua mkopaji na hili litatuletea matatizo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba tuna tatizo. Tatizo ni kwamba mkopaji kwa kweli halindwi, katika hili yule mkopaji anaweza akauza lile shamba. Anaweza akali-*process* akaweka *receiver* na bado anaweza kulinunua yeye mwenyewe. Lakini mkopaji hana hili na hii ni hatari. Ni vema tukaweka utaratibu ambao utamlinda mkopaji na yeye dhidi ya huyu mkopeshaji. Lakini cha msingi, tumeweka utaratibu wa kupitia kwenye Mahakama, Mahakama tunajua matatizo yake. Sisemi kwamba hawatendi haki, lakini matatizo yako mengi. Mimi ningeshauri katika *regulations* atakazoziweka Mheshimiwa Waziri, kwamba yale yote yatakayopendekezwa kama ni kuuza au ni ku-*possess* au ni kujiuzia mwenyewe yule *banker* au aliyetoa mkopo basi yasifanyike mpaka Mheshimiwa Waziri awe amepata taarifa na yeye awe ametoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Baada ya Waheshimiwa watatu waliokuwa wamejiorodhesha kuondoa majina yao. Sasa wengine wote wamepata nafasi ya kusema. Kwa hiyo, tumefikia mwisho wa mjadala wa hoja hii. Na kama nilivyoeleza mapema, tunampa nafasi Mheshimiwa mtoa hoja kujiandaa majibu yake ili aweze kuhitimisha hoja yake saa 11.00 jioni.

Lakini kwa kuwa tumemaliza mapema kabla ya saa 7.00. Ningewashauri Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane moja kwa moja sasa tukitoka hapa badala ya kusubiri saa 7.00, ile Kamati nyingine kwa sababu wanazungumza na watu wanaotoka Dar es Salaam na walipangiwa saa 7.00 itabidi wasubiri saa 7.00 yao ifike. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. Ngoja ngoja samahani, Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka, ameniomba kwamba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 12.00 leo jioni mara baada ya kupitisha Muswada huu unaojadiliwa. Nia ni kupitia marekebisho ya Sheria ya Haki na Madaraka ya Bunge. Kwa kuwa ni marekebisho machache na nimeshaupeleka Muswada huo kwenye Kamati yake, basi ameona ni vizuri waushughulikie mara moja ili wamalize kazi hiyo.

Kwa hiyo, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kikao saa 1200 leo jioni, chumba Na. 133. Shughuli za Bunge zinasitishwa.

*(Saa 06.23 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kabla sijaingia kwa undani, niseme kabisa kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa vile nasimama hapa kwa mara yangu ya kwanza katika mwaka huu nakutakia wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kheri ya mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge hili kwenda kuiwakilisha nchi yetu katika taasisi mbalimbali za uwakilishi katika Bara letu la Afrika, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na timu yake ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini kwake hasa kwa kuuwasilisha Muswada huu kwa ufasaha kweli kweli. Kazi yangu sasa hivi ni kuchangia katika kuunga mkono hoja hiyo lakini pia kujaribu kutoa ufafanuzi kwa maeneo yaliyotokana na hoja nzuri za Waheshimiwa Wabunge hasa kwa maeneo yenye sura ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja la jumla marekebisho yanayopendekezwa kupitia Muswada huu peke yake hayataondoa umaskini wa Watanzania uliopo miongoni mwetu. Lakini kama alivyosema mtoa hoja mwenyewe Muswada huu unatoa fursa kwa wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini watakaopenda kujituma kutumia ardhi waliyopewa kuitumia kama raslimali inayoweza kuwa chanzo cha mitaji ya kupanua shughuli zao za kiuchumi na hivyo kupambana na umaskini. Hasa kujituma hiyo ni upendo wa kila mtu Serikali inaweka tu mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi waweze kutumia raslimali ambayo Mwenyezi Mungu ametupa kwa faida yetu sisi kwa sasa na baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisisitize suala moja la msingi kabisa amelisema Mheshimiwa mtoa hoja lakini lilirudiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa maneno tofauti nalo ni kwamba

kupitia marekebisho haya ya Muswada wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, sheria tunayo, sio kwamba tunatunga sheria mpya lakini kupitia marekebisho haya wala hatufanyi kitu kipya tunachosema ni kwamba mfumo wa kumiliki ardhi nchini kwetu utaendelea kama ulivyo, ardhi itaendelea kuwa ni mali ya umma na mwananchi atapewa fursa ya kuitumia ardhi hiyo kwa masharti ya kwamba aiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwamba ardhi katika mfumo wetu wa miliki ya ardhi, ardhi yote ni ya umma na dhamana ya ardhi hiyo amekabidhiwa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Watanzania ili ahakikishe kwamba ardhi hiyo inatumiwa kwa manufaa ya jamii yetu. Hasa ukielewa dhana hiyo ni kwamba kinachofanyika wewe unapewa tu ile Haki Miliki ya kutumia eneo hilo yaani maslahi yako wewe ni ile Haki Miliki uliyopewa kwa eneo hilo ili uweze kulitumia lakini ardhi inabaki kuwa ya umma umekodishiwa tu pale kwa masharti ambayo ulipewa kama ardhi ya kimila unajua matumizi yake ni nini kama unafuga, unalima kwa misingi hiyo, kama iko katika maeneo ya *public land* ambayo Mheshimiwa Laizer aliniambia bado hajaelewa maana ya *public land* lakini yote hiyo ni mali ya umma wewe itumie kwa masharti ambayo ulipewa. Hilo ni la msingi sana. Suala la kuuza, nitalielezea baadaye, inauzwa vipi lakini ni ile Haki Miliki uliyopewa wewe kwenye eneo hilo ndiyo tunayoiongelea hiyo na ulipopewa uliambiwa endeleza pale je, umeendeleza au hujaendeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hatutungi sheria mpya kwa sababu hata kwa baadhi ya vifungu ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamegusia kwa mfano Kifungu cha 124(j) kile ambacho kinampatia fursa mkopeshaji kwa sababu nyumba au ardhi hiyo umeiachia sana huitunzi sheria inasema mkopeshaji anaweza akatumia fedha zake akaileta katika hadhi nzuri. Sasa siyo kwamba tunaiingiza mara ya kwanza ipo ni Kifungu cha 123 cha Sheria ya Ardhi. Vile vile kwenye hicho Kifungu cha 135(5) siyo kwamba tunakileta sisi hapa kwa mara ya kwanza Bunge lilikubali kimo ndani ya sheria ni Kifungu 134. Kifungu cha 136 kwenye Muswada ambacho kinaongelea mkopeshaji kujiuzia ardhi kimo kwenye Sheria ya Ardhi ya sasa ni Kifungu cha 135. Napenda niseme kwamba ni katika maeneo yale machache ambayo tumejaribu kuifafanua sheria ili ikae vizuri ndio tunakuja kufanya marekebisho hayo lakini tumefanya marekebisho katika *numbering* ya vifungu hivi kwa sababu vingine vimewahishwa na vingine vimekuja baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja iliyotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia asubuhi tumlisikia Mheshimiwa Magayane alizungumzia Kifungu cha 136 kwamba aah wanaweza kufanya mambo yao wakapanga lakini yule mkopeshaji anayeamua kujiuzia ardhi iliyowekwa rehani isipokuwa pale anapotumia utaratibu ule wa wazi wa zabuni hawezi kujiamulia tu lazima apate idhini ya Mahakama na ndio *scheme* inayolindwa humu *scheme* hiyo aende Mahakamani. Pale kwenye *option* kama itaonekana kweli yule mkopeshaji na dalali wamesuka mambo yao ili ardhi ile iuzwe kwa bei poa mwenye ardhi hiyo yaani mkopaji amepewa fursa pia ya kwenda Mahakamani na kuomba Mahakama itamke kwamba walichokifanya ni batili. Kwa hiyo, *protection* bado zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwasikiliza sana Waheshimiwa Wabunge wanasema, nadhani hii dhana ya *bare land* inatuchanganya. Sasa tumejitahidi kupitia hii *schedule of amendments* ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa tumeona tulipatie tasfiri neno *sale* ili lisomeke kama mnavyoona sasa kwenye marekebisho na katika Ibara ya 5 tumeona tuondokane na neno *bare land* lakini nisisitize kama alivyosema Mheshimiwa Waziri jana alipowasilisha hoja yake Muswada huu haupendekezi kuuza ardhi tupu Muswada unapendekeza kuruhusu uhamishaji wa Haki Miliki ya ardhi isiyoendelezwa maana ulipewa uiendeleze ndani ya muda fulani hujaiendeleza amepatikana mtu ambaye ana hamu ya kuiendeleza mmefikia maelewano ndio tunasema sheria iruhusu hali hiyo kwa kuwa nimesema ardhi inaendelea kuwa mali ya umma kinachoruhusiwa kuhamishwa kwenda kwa mtu mwingine ni ile *interest* ambayo mwananchi anayo juu ya ardhi hiyo na maslahi yako katika eneo hilo kama unataka kuiona utaikuta katika hati uliyopewa na Serikali au na kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamishaji wa Haki Miliki ya Ardhi isiyoendelezwa utaruhusiwa tu kama unafanywa na raia wa Tanzania kwenda kwa raia mwingine wa Tanzania hiki ni Kifungu cha 37(9) ukurasa wa tano wa Muswada na huyo Mtanzania ambaye anakubali kuhamishiwa maana ni makubaliano awe amekubali kuiendeleza sio kwamba uende ukakae nayo kwanza asubuhi unaangalia unasema ipo uiendeleze au sasa ndio nakuja kwa hoja ya Mheshimiwa Magayane au unafanywa na raia Mtanzania kwa kutoa Hati isiyo asilia *Derivative Right or interest* kwa mgeni kwa madhumuni ya kuendeleza azma ya

kwanza ambayo ardhi hiyo ilikuwa imetolewa kuiendeleza na wanafanya hivyo kwa njia ya ubia. Sasa hii tunaiona ni fursa nzuri sana kuwawezesha Watanzania kama wewe unaweza kuchangamka ukampata mbia mwenye uwezo wewe ukabaki na ile Haki Miliki yako *The Radical Title* yeye akachukua *Derivative Right* sasa unanufaika kinacho-*matter* pale ni wewe kuwa mwangalifu katika yale maelewano yenu. Lakini hiyo haki siyo asilia hawezi kuigeuza kuwa Haki Miliki kwa sababu taratibu za kubadilisha umiliki wa ardhi upo na naamini kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Serikali inaendelea kuliangalia kwa makini sana suala hili ili watu ambao hawapaswi kuchukua ardhi ya nchi wasijitumbukize huko. Wageni wataingia kuwekeza kwa utaratibu ambao umewekwa na Serikali kupitia sheria hii ya ardhi na sheria nyingine zinazotawala masuala haya.

Mheshimiwa Magayane alisema neno *may* liondolewa lisomeke *shall* sasa ukiandika namna hiyo maana hii ni kuwezesha ni *permissive* sasa ukiiandika *the way* alivyokuwa anapendekeza Mheshimiwa Magayane utakuwa unalazimisha wafanye hiyo *transaction* ya mauzo, sisi hatutaka hilo. Lingine alisema *made only to citizens of Tanzania* sasa hili ndio nimeeleza ukiliandika namna hiyo sheria unafunga mlango kwamba huwezi ukampata mtu wa nje mwenye uwezo ambaye unataka kushirikiana naye kuendeleza ardhi hiyo kwa madhumuni ambayo ardhi hiyo imetolewa. Kwa hiyo, tunapendekeza ibaki hivyo hivyo.

Lipo lingine kubwa ambalo limeongelewa sana ni hili suala la *notice, notice* ya siku 30 ni fupi sana nimeona mengine niyaruke kwa sababu muda wenyewe hauturuhusu lakini nilisemee hili la *notice.* Kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuelewa *scheme* inayopendekezwa maana wameanzia kwenye Kifungu cha 130(5) ambacho kinaelezea mamlaka ambayo mkopeshaji amepewa.

Kitu kimoja ambacho naomba Wabunge waendelee kuisoma vizuri sheria ni kwamba Kifungu hicho cha 130(5) lazima tukisome kwa pamoja na Kifungu cha 132 ukurasa wa 22 ambapo unakuta inaeleza hayo ambayo anapaswa sasa mkopeshaji ayazingatie. Niseme tu kwa kifupi kwamba *scheme* inayopendekezwa kupitia Muswada huu ni kwamba Serikali imejaribu kuweka uwiano mzuri kati ya matakwa ya mkopaji na matakwa ya mkopeshaji. Ndio maana tukasema kwa ardhi iliyotolewa rehani inayotumika kwa shughuli za kibiashara mathalani ni jengo kama mkopaji amechelewa kulipa tunasema pawe na tofauti ya hali hiyo na mahali ambapo mwananchi amechukua mkopo akaweka rehani nyumba yake ya kuishi yeye au ameenda akachukua mkopo sio kampuni yake, Chenge ameunda kampuni lakini yeye Chenge au mke wake ameenda kuchukua mkopo kwa madhumuni ya kuendeleza shughuli za kilimo au ufugaji. Sasa haya makundi matatu haya sheria inasema haiwezekani ukaruhusiwa kutumia haki yako uliyopewa ya *sale* bila kupata utaratibu wa kwenda Mahakamani, inakujaje sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, inaanza hivi, Kifungu cha 127(2) kinamtaka mkopeshaji atoe ilani kwa huyo aliyemkopesha kwamba wewe bwana hutekelezi wajibu wako kwa mujibu wa makubaliano yetu. Kwa hali ya kawaida mawasiliano yatakuwa yameanza mapema sana na wewe uliyechukua mkopo utakuwa unajua kwamba hulipi, ndio maana nimesema tunataka tuweke uwanja ambao unalinda pande zote, sasa hulipa na unajua. Sasa tunasema kama wanaendelea kuwasiliana tu hivyo aah sawa lakini mpaka afike mahali atoe *notice* ya *default* tunasema hivi kama yeye anakusudia kwamba auze ardhi iliyotolewa rehani sasa katika *notice* yake aseme kwamba nakusudia baada ya siku 30 baada ya wewe kupokea ilani hii nakusudia kuuza. Lakini mambo hayaishii hapo wote tunajua kwa sababu nimeeleza kwamba lazima aende Mahakamani anachotakiwa kufanya sasa siku 30 zikiisha sio kwamba anakwenda kuuza haiwezekani lazima sasa ndio aende Mahakamani akawasilishe maombi yake afungue shauri la kuiomba Mahakama kwamba mimi kwa ushahidi huu naomba sasa nipewe *right* ya *possession.* Napenda tuelewane hapa kwamba siku 30 hizo ni zile za kusubiri umeshasema kwamba wewe unakusudia kuuza lakini tunaamini zitazidi siku 30 mpaka ifikie uamuzi wa Mahakama kwamba imesema sasa kweli inauzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano mathalani nyuma ya makazi ilitolewa kama rehani kuchukua mkopo taratibu zilifuatwa mkopaji halipi tumeandikiana halafu hata mawasiliano yamefutika tunaenda kuangalia ile nyumba ambayo ilitolewa rehani tunakuta ni giza watu hawaishi katika hali hiyo hakuna haja ya kusubiri siku 60 au 90 au 30 kwa sababu unajua kabisa hakuna mtu anayeishi mle. Katika hali ya namna hii unaingia tu lakini kama kuna mtu anaishi mle na wewe unataka uiuze bila kuwepo mtu lazima uende Mahakamani ukaombe. Ndio maana tunasema ni vizuri hizo siku 30 zikawa ni zile za kwanza baada ya wewe kukujulisha kwamba nina-*intend* kufanya yafuatayo na katika hili nataka niuze baada ya siku 30 mimi nitachukua hatua nyingine yaani ataenda Mahakamani.

Nilimsikia Mheshimiwa Magayane akisema lakini Mahakamani kule inachukua muda mrefu sana aah tusichanganye sisi tunataka makundi haya yalindwe ila tumesema kwamba Serikali pia inapendekeza kupitia Sheria inayosimamia Taratibu za Mashauri ya Madai *(Civil Procedure Code)* tufanye marekebisho kwenye sheria hiyo ili kuleta ufanisi katika suala zima la *enforcement* ya *mortgages.* Lakini sisi tunaona suala hili kwamba ule wasiwasi ambao Waheshimiwa Wabunge wameuonyesha kwamba muda hautoshi hahusiani na mchakato mzima wa tangu siku 30 kuisha na kuendelea Mahakamani mpaka uamuzi wa Mahakama ukapatikane kwamba sasa sawa chukua *vacant position.* Tukilielewa hilo wala hakuna haja ya kuomba turudi kwa siku 60, 90 au kama alivyopendekeza Mheshimiwa Pawa, tuwe kama Baniani leta nusu tuchukue siku hamsini.

Sisi tunaliomba Bunge lako Tukufu lielewe nia njema ya Serikali kwamba muangalie pia huyu anayekopesha pesa hizi sio za kwake ni amana za wateja wake ambao ni wananchi wa kawaida wewe na mimi na yule. Wewe ukiweza kurudisha mkopo huo ndivyo utakavyomwezeshe yeye kuwakopesha wengine. Tunataka sasa tuone sura hiyo kwamba utaratibu unaopendekezwa ni huo kwamba toa ilani na kama unataka kuuza *property* hiyo sema kwamba utafanya hivyo ndani ya siku 30 na uanze sasa *process* nyingine. Naamini mpaka upate uamuzi wa Mahakamani siwezi kutabiri lakini kama Mahakama zinafanya *efficiently* inaweza kufika hata miezi mitatu au minne. Kwa hiyo, bado naona tuna muda wa kutosha na napenda niwaondolee wasiwasi kwamba tumelalia sana upande wa kumtetea mkopeshaji, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili wazo la kuruhusu kuhamisha Haki Miliki isije kuonekana kwamba ni ujanja fulani tu wa kubadili matumizi ya ardhi ambayo mtu alikuwa amepewa. Napenda nisisitize kwamba haikusudiwi kupitia Muswada huu kuruhusu kutumia uhamisho wa Haki Miliki ya Ardhi isiyoendelezwa kama kisingizio cha kubadili matumizi ya ardhi hiyo. Sheria, kanuni na taratibu zilizopo zinazosimamia masuala haya zitaendelea kusimamia suala hilo. Wewe kama ulipewa ardhi hiyo kwa matumizi ya makazi unataka kubadilisha matumizi yake fuata utaratibu omba kama Wizara ya Ardhi kupitia vyombo husika watakuambia sawa watabadilisha lakini huwezi kutumia utaratibu huu wa kuhamisha Haki Miliki ukaenda kubadilisha matumizi ya awali ambayo yalitolewa kwa madhumuni ya ardhi husika. Nadhani alikuwa Mheshimiwa Msafiri aliyetoa tahadhari hiyo. Waziri alieleza kwamba kwa kazi nzuri ambayo sasa hivi Wizara inafanya kwanza ku-*computerize* hizi Haki Miliki na Offers ambazo zinatolewa maana kwa Sheria ya Ardhi sasa hivi kama hujapewa Hati yako ndani ya miezi sita sheria inakuruhusu uende ukaisajili ile barua ya *Offer* na hiyo *Offer* hiyo inakuwezesha wewe hata ukienda kwenye Benki hata kama Wizara ya Ardhi itachukua mwaka mmoja wewe inakuruhusu maana inatambuliwa na sheria ukaitumia hiyo kuweza kuchukua mkopo.

Naamini Ofisi ya Kamishna wa Ardhi watakuwa makini sana kwenye eneo hili kwa sababu ni afadhali Kamishna akawahi kujua ardhi ambayo imetolewa kwa kusudio fulani haiendelezwi akasema badala ya kuwasubiri hawa waje waanze kubadilishana wao wewe mwenyewe kama unasimamia vizuri utasema ardhi hii hujaiendeleza sasa mimi nataka nitumie madaraka ambayo sheria imenipa naitoa kwako nampa mwingine ambaye ana uwezo wa kuiendeleza. Lakini tunafahamu fika baadhi yetu hata mimi nijishtaki hapa nimepewa kiwanja karibu mwaka wa pili sijakiendeleza inawezekana nikisema kesho wanaweza wakanifuata lakini bado niko ndani ya kipindi kile cha miaka mitatu na kama kuna sababu ya msingi kwa nini hujaendeleza unakwenda kujenga hoja watakusikiliza wakiona imethibitika basi watakuongezea muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno Mahakama limetumika tu *Court* wala hatuelewi ni Mahakama ipi. Napenda niseme tu kwamba kwa sababu tunalifanyia marekebisho Sheria ya Ardhi iliyopo tasfiri ya neno *Court* iliyomo katika Sheria ya Ardhi ndio hilo kwa hiyo ni Mahakama ya Ardhi ndio inayoongelewa hapa.Kuhusu *matrimonial home,* nakwenda kwa haraka maana muda wangu umekwisha, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge msome haya marekebisho ya Muswada ambayo yako katika orodha ya nyongeza ya marekebisho. Tumejaribu kuondokana na ile dhana ya *qualifying spouse* ambayo ilikuwa inawakanganya Waheshimiwa Wabunge maana ilikuwa inaonekana kama tunaanzisha aina mpya ya ndoa. Sasa tumeona tuibadilishe kidogo lakini tujibu hoja ile ya pili, ndoa za mitala pia kwa sababu zinatambuliwa na Sheria ya Ndoa na zenyewe, tuwe wa wazi kama alivyosema Mheshimiwa Halinga kwamba kuweni wa wazi ndoa za kificho zisiruhusiwe. Kwa hiyo, tumejaribu mkikisoma kifungu kipya cha 114 tumekiweka sawa kujibu hoja zote hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa maelezo ambayo tumetoa kwa makundi yanayolindwa ya wafugaji kama unaitumia ardhi yako kwa kufuga, unaitumia ardhi yako kwa makazi au kwa shughuli za kilimo.

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwa undani, niseme kabisa kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa vile nasimama hapa kwa mara yangu ya kwanza katika mwaka huu nakutakia wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kheri ya mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge hili kwenda kuiwakilisha nchi yetu katika taasisi mbalimbali za uwakilishi katika Bara letu la Afrika, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na timu yake ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini kwake hasa kwa kuuwasilisha Muswada huu kwa ufasaha kweli kweli. Kazi yangu sasa hivi ni kuchangia katika kuunga mkono hoja hiyo lakini pia kujaribu kutoa ufafanuzi kwa maeneo yaliyotokana na hoja nzuri za Waheshimiwa Wabunge hasa kwa maeneo yenye sura ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja la jumla marekebisho yanayopendekezwa kupitia Muswada huu peke yake hayataondoa umaskini wa Watanzania uliopo miongoni mwetu.

Lakini kama alivyosema mtoa hoja mwenyewe Muswada huu unatoa fursa kwa wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini watakaopenda kujituma kutumia ardhi waliyopewa kuitumia kama raslimali inayoweza kuwa chanzo cha mitaji ya kupanua shughuli zao za kiuchumi na hivyo kupambana na umaskini. Hasa kujituma hiyo ni upendo wa kila mtu, Serikali inaweka tu mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi waweze kutumia raslimali ambayo Mwenyezi Mungu ametupa kwa faida yetu sisi kwa sasa na baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisisitize suala moja la msingi kabisa amelisema Mheshimiwa mtoa hoja lakini lilirudiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa maneno tofauti nalo ni kwamba kupitia marekebisho haya ya Muswada wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, sheria tunayo, sio kwamba tunatunga sheria mpya lakini kupitia marekebisho haya wala hatufanyi kitu kipya tunachosema ni kwamba mfumo wa kumiliki ardhi nchini kwetu utaendelea kama ulivyo, ardhi itaendelea kuwa ni mali ya umma na mwananchi atapewa fursa ya kuitumia ardhi hiyo kwa masharti ya kwamba aiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwamba ardhi katika mfumo wetu wa miliki ya ardhi, ardhi yote ni ya umma na dhamana ya ardhi hiyo amekabidhiwa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Watanzania ili ahakikishe kwamba ardhi hiyo inatumiwa kwa manufaa ya jamii yetu.

Sasa ukielewa dhana hiyo ni kwamba kinachofanyika wewe unapewa tu ile Haki Miliki ya kutumia eneo hilo yaani maslahi yako wewe ni ile Haki Miliki uliyopewa kwa eneo hilo ili uweze kulitumia lakini ardhi inabaki kuwa ya umma umekodishiwa tu pale kwa masharti ambayo ulipewa kama ardhi ya kimila, unajua matumizi yake ni nini kama unafuga, unalima kwa misingi hiyo, kama iko katika maeneo ya *public land* ambayo Mheshimiwa Michael Laizer aliniambia bado hajaelewa maana ya *public*

*land* lakini yote hiyo ni mali ya umma wewe itumie kwa masharti ambayo ulipewa. Hilo ni la msingi sana. Suala la kuuza, nitalielezea baadaye, inauzwa vipi lakini ni ile Haki Miliki uliyopewa wewe kwenye eneo hilo ndiyo tunayoiongelea hiyo na ulipopewa uliambiwa endeleza pale je, umeendeleza au hujaendeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hatutungi sheria mpya kwa sababu hata kwa baadhi ya vifungu ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamegusia kwa mfano Kifungu cha 124(j) kile ambacho kinampatia fursa mkopeshaji kwa sababu nyumba au ardhi hiyo umeiachia sana, huitunzi, sheria inasema mkopeshaji anaweza akatumia fedha zake akaileta katika hadhi nzuri. Sasa siyo kwamba tunaiingiza mara ya kwanza ipo ni Kifungu cha 123 cha Sheria ya Ardhi. Vile vile kwenye hicho Kifungu cha 135(5) siyo kwamba tunakileta sisi hapa kwa mara ya kwanza Bunge lilikubali, kimo ndani ya sheria ni Kifungu 134. Kifungu cha 136 kwenye Muswada ambacho kinaongelea mkopeshaji kujiuzia ardhi kimo kwenye Sheria ya Ardhi ya sasa ni Kifungu cha 135. Napenda niseme kwamba ni katika maeneo yale machache ambayo tumejaribu kuifafanua sheria ili ikae vizuri ndio tunakuja kufanya marekebisho hayo lakini tumefanya marekebisho katika *numbering* ya vifungu hivi kwa sababu vingine vimewahishwa na vingine vimekuja baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja iliyotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia asubuhi tumlisikia Mheshimiwa Beatus Magayane, alizungumzia Kifungu cha 136 kwamba wanaweza kufanya mambo yao wakapanga lakini yule mkopeshaji anayeamua kujiuzia ardhi iliyowekwa rehani isipokuwa pale anapotumia utaratibu ule wa wazi wa zabuni hawezi kujiamulia tu lazima apate idhini ya Mahakama na ndio *scheme* inayolindwa humu *scheme* hiyo aende Mahakamani. Pale kwenye *option* kama itaonekana kweli yule mkopeshaji na dalali wamesuka mambo yao ili ardhi ile iuzwe kwa bei poa mwenye ardhi hiyo yaani mkopaji amepewa fursa pia ya kwenda Mahakamani na kuomba Mahakama itamke kwamba walichokifanya ni batili. Kwa hiyo, *protection* bado zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwasikiliza sana Waheshimiwa Wabunge wanasema, nadhani hii dhana ya *bare land* inatuchanganya. Sasa tumejitahidi kupitia hii *schedule of amendments* ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa tumeona tulipatie tafsiri neno *sale* ili lisomeke kama mnavyoona sasa kwenye marekebisho na katika Ibara ya 5 tumeona tuondokane na neno *bare land* lakini nisisitize kama alivyosema Mheshimiwa Waziri jana alipowasilisha hoja yake, Muswada huu haupendekezi kuuza ardhi tupu, Muswada unapendekeza kuruhusu uhamishaji wa Haki Miliki ya ardhi isiyoendelezwa maana ulipewa uiendeleze ndani ya muda fulani hujaiendeleza amepatikana mtu ambaye ana hamu ya kuiendeleza mmefikia maelewano ndio tunasema sheria iruhusu hali hiyo kwa kuwa nimesema ardhi inaendelea kuwa mali ya umma kinachoruhusiwa kuhamishwa kwenda kwa mtu mwingine ni ile *interest* ambayo mwananchi anayo juu ya ardhi hiyo na maslahi yako katika eneo hilo kama unataka kuiona utaikuta katika hati uliyopewa na Serikali au na kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamishaji wa Haki Miliki ya Ardhi isiyoendelezwa utaruhusiwa tu kama unafanywa na raia wa Tanzania kwenda kwa raia mwingine wa Tanzania hiki ni Kifungu cha 37(9) ukurasa wa tano wa Muswada na huyo Mtanzania ambaye anakubali kuhamishiwa maana ni makubaliano awe amekubali kuiendeleza sio kwamba uende ukakae nayo kwanza asubuhi unaangalia unasema ipo uiendeleze au sasa ndio nakuja kwa hoja ya Mheshimiwa Beatus Magayane au unafanywa na raia Mtanzania kwa kutoa Hati isiyo asilia *Derivative Right or Interest* kwa mgeni kwa madhumuni ya kuendeleza azma ya kwanza ambayo ardhi hiyo ilikuwa imetolewa kuiendeleza na wanafanya hivyo kwa njia ya ubia.

Sasa hii tunaiona ni fursa nzuri sana kuwawezesha Watanzania kama wewe unaweza kuchangamka ukampata mbia mwenye uwezo wewe ukabaki na ile Haki Miliki yako *The Radical Title* yeye akachukua *Derivative Right* sasa unanufaika kinacho-*matter* pale ni wewe kuwa mwangalifu katika yale maelewano yenu. Lakini hiyo haki siyo asilia hawezi kuigeuza kuwa Haki Miliki kwa sababu taratibu za kubadilisha umiliki wa ardhi upo na naamini kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Serikali inaendelea kuliangalia kwa makini sana suala hili ili watu ambao hawapaswi kuchukua ardhi ya nchi wasijitumbukize huko. Wageni wataingia kuwekeza kwa utaratibu ambao umewekwa na Serikali kupitia sheria hii ya ardhi na sheria nyingine zinazotawala masuala haya.

Mheshimiwa Beatus Magayane, alisema neno *may* liondolewe lisomeke *shall,* sasa ukiandika namna hiyo maana hii ni kuwezesha, ni *permissive* sasa ukiiandika *the way* alivyokuwa anapendekeza Mheshimiwa Beatus Magayane, utakuwa unalazimisha wafanye hiyo *transaction* ya mauzo, sisi hatutaki hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine alisema *made only to citizens of Tanzania,* sasa hili ndilo nimeeleza ukiliandika namna hiyo sheria unafunga mlango kwamba huwezi ukampata mtu wa nje mwenye uwezo ambaye unataka kushirikiana naye kuendeleza ardhi hiyo kwa madhumuni ambayo ardhi hiyo imetolewa. Kwa hiyo, tunapendekeza ibaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo lingine kubwa ambalo limeongelewa sana ni hili suala la *notice, notice* ya siku 30 ni fupi sana nimeona mengine niyaruke kwa sababu muda wenyewe hauturuhusu lakini nilisemee hili la *notice.*

Kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuelewa *scheme* inayopendekezwa maana wameanzia kwenye Kifungu cha 130(5) ambacho kinaelezea mamlaka ambayo mkopeshaji amepewa. Kitu kimoja ambacho naomba Wabunge waendelee kuisoma vizuri sheria ni kwamba Kifungu hicho cha 130(5) lazima tukisome kwa pamoja na Kifungu cha 132 ukurasa wa 22 ambapo unakuta inaeleza hayo ambayo anapaswa sasa mkopeshaji ayazingatie. Niseme tu kwa kifupi kwamba *scheme* inayopendekezwa kupitia Muswada huu ni kwamba Serikali imejaribu kuweka uwiano mzuri kati ya matakwa ya mkopaji na matakwa ya mkopeshaji. Ndio maana tukasema kwa ardhi iliyotolewa rehani inayotumika kwa shughuli za kibiashara mathalani ni jengo kama mkopaji amechelewa kulipa tunasema pawe na tofauti ya hali hiyo na mahali ambapo mwananchi amechukua mkopo akaweka rehani nyumba yake ya kuishi yeye au ameenda akachukua mkopo sio kampuni yake, Chenge ameunda kampuni lakini yeye Chenge au mke wake ameenda kuchukua mkopo kwa madhumuni ya kuendeleza shughuli za kilimo au ufugaji. Sasa haya makundi matatu haya sheria inasema haiwezekani ukaruhusiwa kutumia haki yako uliyopewa ya *sale* bila kupata utaratibu wa kwenda Mahakamani, inakujaje sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, inaanza hivi, Kifungu cha 127(2) kinamtaka mkopeshaji atoe ilani kwa huyo aliyemkopesha kwamba wewe bwana hutekelezi wajibu wako kwa mujibu wa makubaliano yetu. Kwa hali ya kawaida mawasiliano yatakuwa yameanza mapema sana na wewe uliyechukua mkopo utakuwa unajua kwamba hulipi, ndio maana nimesema tunataka tuweke uwanja ambao unalinda pande zote, sasa hulipa na unajua.

Sasa tunasema kama wanaendelea kuwasiliana tu hivyo sawa, lakini mpaka afike mahali atoe *notice* ya *default* tunasema hivi kama yeye anakusudia kwamba auze ardhi iliyotolewa rehani sasa katika *notice* yake aseme kwamba nakusudia baada ya siku 30 baada ya wewe kupokea ilani hii nakusudia kuuza. Lakini mambo hayaishii hapo wote tunajua kwa sababu nimeeleza kwamba lazima aende Mahakamani anachotakiwa kufanya sasa siku 30 zikiisha sio kwamba anakwenda kuuza haiwezekani lazima sasa ndio aende Mahakamani akawasilishe maombi yake afungue shauri la kuiomba Mahakama kwamba mimi kwa ushahidi huu naomba sasa nipewe *right* ya *possession.*

Napenda tuelewane hapa kwamba siku 30 hizo ni zile za kusubiri umeshasema kwamba wewe unakusudia kuuza lakini tunaamini zitazidi siku 30 mpaka ifikie uamuzi wa Mahakama kwamba imesema sasa kweli inauzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano mathalani nyumba ya makazi ilitolewa kama rehani kuchukua mkopo taratibu zilifuatwa mkopaji halipi tumeandikiana halafu hata mawasiliano yamefutika tunaenda kuangalia ile nyumba ambayo ilitolewa rehani tunakuta ni giza watu hawaishi katika hali hiyo hakuna haja ya kusubiri siku 60 au 90 au 30 kwa sababu unajua kabisa hakuna mtu anayeishi mle. Katika hali ya namna hii unaingia tu lakini kama kuna mtu anaishi mle na wewe unataka uiuze bila kuwepo mtu lazima uende Mahakamani ukaombe. Ndio maana tunasema ni vizuri hizo siku 30 zikawa ni zile za kwanza baada ya wewe kukujulisha kwamba nina-*intend* kufanya yafuatayo na katika hili nataka niuze baada ya siku 30 mimi nitachukua hatua nyingine yaani ataenda Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mheshimiwa Beatus Magayane, akisema lakini Mahakamani kule inachukua muda mrefu sana, aah, tusichanganye sisi tunataka makundi haya yalindwe ila tumesema kwamba Serikali pia inapendekeza kupitia Sheria inayosimamia Taratibu za Mashauri ya Madai *(Civil Procedure Code)* tufanye marekebisho kwenye sheria hiyo ili kuleta ufanisi katika suala zima la *enforcement* ya *mortgages.* Lakini sisi tunaona suala hili kwamba ule wasiwasi ambao Waheshimiwa Wabunge wameuonyesha kwamba muda hautoshi hausiani na mchakato mzima wa tangu siku 30 kwisha na kuendelea Mahakamani mpaka uamuzi wa Mahakama upatikane kwamba sasa sawa chukua *vacant position.* Tukilielewa hilo wala hakuna haja ya kuomba turudi kwa siku 60, 90 au kama alivyopendekeza Mheshimiwa Semindu Pawa tuwe kama Baniani leta nusu tuchukue siku hamsini.

Sisi tunaliomba Bunge lako Tukufu lielewe nia njema ya Serikali kwamba muangalie pia huyu anayekopesha pesa hizi sio za kwake ni amana za wateja wake ambao ni wananchi wa kawaida wewe na mimi na yule. Wewe ukiweza kurudisha mkopo huo ndivyo utakavyomwezesha yeye kuwakopesha wengine. Tunataka sasa tuone sura hiyo kwamba utaratibu unaopendekezwa ni huo kwamba toa ilani na kama unataka kuuza *property* hiyo sema kwamba utafanya hivyo ndani ya siku 30 na uanze sasa *process* nyingine. Naamini mpaka upate uamuzi wa Mahakamani siwezi kutabiri lakini kama Mahakama zinafanya *efficiently* inaweza kufika hata miezi mitatu au minne. Kwa hiyo, bado naona tuna muda wa kutosha na napenda niwaondolee wasiwasi kwamba tumelalia sana upande wa kumtetea mkopeshaji, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili wazo la kuruhusu kuhamisha Haki Miliki isije kuonekana kwamba ni ujanja fulani tu wa kubadili matumizi ya ardhi ambayo mtu alikuwa amepewa.

Napenda nisisitize kwamba haikusudiwi kupitia Muswada huu kuruhusu kutumia uhamisho wa Haki Miliki ya Ardhi isiyoendelezwa kama kisingizio cha kubadili matumizi ya ardhi hiyo. Sheria, kanuni na taratibu zilizopo zinazosimamia masuala haya zitaendelea kusimamia suala hilo. Wewe kama ulipewa ardhi hiyo kwa matumizi ya makazi unataka kubadilisha matumizi yake fuata utaratibu omba kama Wizara ya Ardhi kupitia vyombo husika watakuambia sawa watabadilisha lakini huwezi kutumia utaratibu huu wa kuhamisha Haki Miliki ukaenda kubadilisha matumizi ya awali ambayo yalitolewa kwa madhumuni ya ardhi husika. Nadhani alikuwa Mheshimiwa Ruth Msafiri, aliyetoa tahadhari hiyo.

Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba kazi nzuri ambayo sasa hivi Wizara inafanya kwanza na ku-*computerize* hizi Haki Miliki na *offers* ambazo zinatolewa maana kwa Sheria ya Ardhi sasa hivi kama hujapewa Hati yako ndani ya miezi sita sheria inakuruhusu uende ukaisajili ile barua ya *offer* na hiyo *offer* hiyo inakuwezesha wewe hata ukienda kwenye Benki hata kama Wizara ya Ardhi itachukua mwaka mmoja wewe inakuruhusu maana inatambuliwa na sheria ukaitumia hiyo kuweza kuchukua mkopo.

Naamini Ofisi ya Kamishna wa Ardhi watakuwa makini sana kwenye eneo hili kwa sababu ni afadhili Kamishna akawahi kujua ardhi ambayo imetolewa kwa kusudio fulani haiendelezwi akasema badala ya kuwasubiri hawa waje waanze kubadilishana wao wewe mwenyewe kama unasimamia vizuri utasema ardhi hii hujaiendeleza sasa mimi nataka nitumie madaraka ambayo sheria imenipa naitoa kwako nampa mwingine ambaye ana uwezo wa kuiendeleza. Lakini tunafahamu fika baadhi yetu hata mimi nijishtaki hapa nimepewa kiwanja karibu mwaka wa pili sijakiendeleza inawezekana nikisema kesho wanaweza wakanifuata lakini bado niko ndani ya kipindi kile cha miaka mitatu na kama kuna sababu ya msingi kwa nini hujaendeleza unakwenda kujenga hoja watakusikiliza wakiona imethibitika basi watakongezea muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno Mahakama limetumika tu *Court* wala hatuelewi ni Mahakama ipi. Napenda niseme tu kwamba kwa sababu tunalifanyia marekebisho Sheria ya Ardhi iliyopo tasfiri ya neno *Court* iliyomo katika Sheria ya Ardhi ndio hilo kwa hiyo ni Mahakama ya Ardhi ndio inayoongelewa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *matrimonial home,* nakwenda kwa haraka maana muda wangu umekwisha, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge msome haya marekebisho ya Muswada ambayo yako katika orodha ya nyongeza ya marekebisho. Tumejaribu kuondokana na ile dhana ya *qualifying spouse* ambayo ilikuwa inawakanganya Waheshimiwa Wabunge maana ilikuwa inaonekana kama tunaanzisha aina mpya ya ndoa. Sasa tumeona tuibadilishe kidogo lakini tujibu hoja ile ya pili ndoa za mitala pia kwa sababu zinatambuliwa na Sheria ya Ndoa na zenyewe, tuwe wa wazi kama alivyosema Mheshimiwa Edson

Halinga kwamba kuweni wa wazi, ndoa za kificho zisiruhusiwe. Kwa hiyo, tumejaribu mkikisoma kifungu kipya cha 114 tumekiweka sawa kujibu hoja zote hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa maelezo ambayo tumetoa kwa makundi yanayolindwa ya wafugaji kama unaitumia ardhi yako kwa kufuga, unaitumia ardhi yako kwa makazi au kwa shughuli za kilimo utaratibu unaopendekezwa ni mzuri kwa sababu hata yule mkopeshaji akienda Mahakamani akasema umeshindwa kulipa mathalan kwa upande wa ardhi iliyotolewa rehani ambayo inatumika kwa shughuli za kilimo, wewe uliyekopa utakuwa na fursa ya kuieleza Mahakama ukweli wa mambo ulivyo. Unaweza ukamweleza Mheshimiwa Hakimu au Mheshimiwa Jaji, naomba twende kutembelea shamba langu, mkifika pale mtaona ni kweli nimechelewa tu kulipa, lakini pale kuna minazi yangu tayari imeshabeba, kuna ndizi, kuna kahawa au kuna pamba.

Kwa hiyo, mkiniruhusu kwa kipindi ambacho Mahakama itaona kinafaa, yeye ataomba mkiniruhusu kwa miezi sita au mitatu, nitakuwa nimeshapata fedha ya kutosha kuweza kulipa deni hili. Mahakama itasema nasitisha uamuzi wa mali hii isiuzwe tukupatie nafasi wewe uende kujizatiti ukusanye nguvu, uza mazao yako, uweze kumlipa huyo aliyekukopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sura hiyo tumejaribu kuiweka sheria katika hali ambayo inatulinda sote, wakopaji na wale ambao wanasimamia dhamana za wale walioweka fedha katika benki hizo ili na wenyewe waweze kuzipata, waweze kukopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tena kwa kukushukuru wewe, kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao mzuri, lakini hasa kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha Muswada huu. Naamini mchango wangu mdogo katika maelezo haya utasaidia katika kuhitimisha zoezi la kukubali na hatimaye kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Kwanza napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kauli au kwa maandishi. Waliochangia kwa kauli ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Beatus Magayane na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia ama kwa kauli au maandishi kwa ushauri, maoni na mapendekezo mazuri waliyotoa kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada na mikakati ya utekelezaji. Nawashukuru kwa kuunga mkono Muswada na tahadhari zilizotolewa katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa maelezo yake ambayo nina hakika yamesaidia sana kuweza kufafanua vipengele vingi vya kisheria ambavyo vilikuwa vinatutatiza. Kwa hiyo, natumaini baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge watakuwa katika hali ya kuelewa na kuendelea kuunga mkono Muswada huu.

Napenda nitoe maelezo machache kwa baadhi ya maeneo ya jumla. Kwa kuwa muda hauruhusu naomba nisisitize tu mambo machache ya jumla, lakini niahidi kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge wote tunayo na tutatoa majibu ya maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge wote ili waweze kuona hoja zilizotolewa na majibu ambayo yametolewa kwa kila hoja ili iwe kumbukumbu kwetu na itusaidie katika usimamizi wa utekelezaji wa mabadiliko haya na Sheria ya Ardhi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na eneo la elimu kwa umma. Hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba ipo haja, masuala haya yawekewe mkakati maalum na mzuri kuhakikisha kwamba yaliyomo kwenye mabadiliko haya ya sheria kwa ujumla yanawafikia walengwa Mijini na Vijijini na sisi tunakubaliana na hoja hiyo na kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya kuwasilisha Muswada nilieleza hilo na kwa kweli tumekwishaanza. Tumekwishatayarisha mwongozo wa utekelezaji wa Sheria Na. 4 ya mwaka 1999. Tulikwishashughulikia Sheria Na. 5, Sheria ya Ardhi Vijijini ambayo tumekwishaitafsiri kwa lugha ya Kiswahili, sheria yenyewe na kanuni zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatua ya pili ni Sheria Na. 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi yenyewe. Sasa tumekwishaanza kwa kutayarisha mwongozo ambao tutautumia sisi pamoja na ninyi na wadau wote na wanaharakati wote kuweza kufikisha elimu na ujumbe kwa wananchi Mijini na Vijijini. Kwa hiyo, hili napenda niwathibitishie kwamba lipo katika maandalizi na mkishaidhinisha mabadiliko haya tunaingia mtamboni kuweza kuyatafsiri kwa Kiswahili na kuyaingiza katika mwongozo huu ili sasa tuanze kazi ya kuelimisha umma kwa mbinu mbalimbali. Hili naomba kwa kweli kwa moyo wa dhati kabisa kwamba kazi hii ni yetu wote kuanzia sisi Waheshimiwa Wabunge maana tuna nyaraka zote zinazohusiana na sera na sheria za Ardhi tunazo. Sasa ni wajibu wetu kuzielewa na halafu tukapeleka kwa wananchi katika Majimbo yetu na maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tutaendelea kushirikiana na wadau wanaohusika pamoja na TAMISEMI kuhakikisha kwamba watendaji katika Halmashauri zetu kwa kweli wanafanya kazi inayokusudiwa kutoka kwao maana katika mazungumzo ya Waheshimiwa Wabunge wengi na mara nyingi inanisikitisha inakuwa kana kwamba tunawaogopa wale siyo wetu, lakini kumbe wapo chini yetu, wale ni wetu na wana nyaraka zote na wanapaswa kwenda kwa wananchi kueleza. Sasa nini kinagomba.

Kwa hiyo, naomba tusisite katika Halmashauri zetu kuwaita watendaji kuwauliza mikakati iliyopo kwenda kwa wananchi tutoe hii elimu. Nasi kama Wizara tutajitahidi kutumia vyombo vya Kitaifa pamoja na wadau ili kwa kweli elimu iendelee kuwafikia wananchi Mijini na Vijijini. Kwa hiyo, hilo la kwanza ambalo nilitaka nisisitize kwamba tunakubaliana kabisa na kabla ya kuanza kutekeleza mabadiliko haya tutahakikisha kwamba suala hili tumelizingatia kuhakikisha kwamba elimu tunaianzisha kupeleka ujumbe huu kwa wananchi Mijini na Vijijini. Hilo la kwanza ambalo nilitaka nilieleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mashamba au maeneo ambayo yamemilikishwa hayaendelezwi. Nalo limezungumzwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Hili pia linanisikitisha maana hili tumekuwa tukilizungumza kila wakati na sisi Wizara tangu mwaka 1996 tulikwishatoa miongozo na maelekezo kwa Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya kwamba maeneo yote ambayo yamemilikishwa hayaendelezwi lazima hatua zichukuliwe na hatua hazianzii Wizarani zinaanzia kwenye Halmashauri. Kaeni kwenye vikao huko, *Amadori* amepewa hekta kadhaa haziendelezi, kaa kwenye kikao cha Halmashauri, pendekeza, kuna hatua apelekewe ilani ikiisha mkikubaliana na maelezo yake, *okay.* Msipokubaliana mnaendelea na hatua ya pili mnapendekeza hati yake ibatilishwe, ndiyo mnakuja Wizarani. Wizara haiwezi kuanza kuchukua hatua bila ninyi huko kwenye Halmashauri kuchukua hatua hizo na wataalam huko wanajua.

Mheshimiwa Maghoba, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, mpira upo kwenu, tuleteeni mapendekezo ya maeneo ambayo hayaendelezwi, tutachukua hatua. Kuna baadhi ya

Waheshimiwa hapa wamechukua hatua kama Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa Chegeni Masunga, nimekwishazungumza nao kuwaeleza hatua tuliyofikia, lakini maeneo mengine hatuna. Tuleteeni tuchukue hatua na hatua zinaanza huko huko kwenye Halmashauri.

Kwa kweli hili kabisa kabisa nawasihi Waheshimiwa Wabunge, tusijione wanyonge kuwakabili watendaji wetu kwenye Halmashauri, tufanye kazi. Kwa hiyo hili nalirejesha kwenu, lipo kwenu, shughulikieni maeneo ambayo hayaendelezwi yashughulikiwe ili waweze kupewa wananchi ambao wapo tayari kuyaendeleza maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu. Nalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Hili nalo lipo katika utekelezaji, Tume yetu ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi imefanya kazi nzuri sana, imetayarisha miongozo na kuisambaza Vijijini, karibu Vijiji vyote nchini vina miongozo ya jinsi ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu. Wale ambao wamepokea miongozo hiyo na wamekaa hakuna matatizo ya ugomvi kati ya wakulima, wafugaji sijui na nani. Wananchi ni wajibu wao kukaa, kupanga matumizi ya ardhi katika Vijiji vyao na tumewasaidia kuwapa miongozo jinsi ya kukaa na kupanga matumizi bora.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuwa na ugomvi wa wakulima na wafugaji maana mtakaa wenyewe kupanga matumizi yenu. Hatuwapangii sisi, mnapanga wenyewe na wala hakuna atakayekuja kunyang'anya ardhi yenu, anyang'anye kwa vipi? Hofu ya wafugaji inatoka wapi? Ardhi ni yenu nani atakuja kunyang'anya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unazungumzia tu maeneo yaliyomilikishwa na yule anayetaka kwenda kukopa fedha benki, basi watu wengine hawahusiki. Wewe una pande lako la ardhi kubwa, hutaki kwenda kukopa benki, endelea nalo, hakuna atakayekuja kukunyang'anya. Kwa hiyo, tusije kuanza kuzusha hofu ambayo haipo.

Kwa hiyo, napenda sana hili tuelewane ili kwa kweli tukitoka hapa tunalenga kwenye maeneo hayo tu ya hati miliki, kama ni nyumba yako, kama ni shamba lako umeona kwamba ukachukue mkopo benki ndiyo tunazungumzia. Kwa kweli Muswada huu unawezesha pande zote mbili yule mwenye nyumba yake au mwenye shamba anayetaka kukopa basi awezeshwe kufanya hivyo na yule mwenye fedha anayekukopesha naye awezeshwe hivyo. Pande zote mbili ziangaliwe ili utaratibu uweze kuendelea kwa usalama na kwa usawa na kwa haki. Ndiyo madhumuni ya Muswada huu. Hilo ni eneo la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilitaka pia nilisemee ni kwamba hizi sheria ni ngumu lazima nikiri, hizi sheria za Ardhi ni ngumu lakini zipo. Kwanza tuna sera yenyewe, halafu tuna Sheria ya Ardhi Na. 4, tuna Sheria ya Ardhi ya Vijiji na tuna Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ya Mwaka 2002, tunazo, zote zipo. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wanazungumzia migogoro ya ardhi sheria ipo na jinsi ya kutatua migogoro hiyo na sheria tunazo na watendaji huko kwenye Halmashauri wanazo hizo sheria. Sasa wito na rai yangu ni kwamba sisi sote tujitahidi kuzisoma, kuzielewa na halafu tusaidie kufikisha ujumbe kwa walengwa ili kwa kweli mambo mengi ambayo tulikuwa tunazungumzia hapa tayari yana sheria ambazo tungeweza kuzitumia na kuyatatua bila matatizo.

Kwa hiyo, naomba sana kwamba tujitahidi na kama nilivyosema basi katika jitihada hizo ni pamoja na elimu, mpango huu ambao tumeuandaa kwamba tutashirikiana ili kwa kweli sera na Sheria hizi tuweze kuzielewa na zitusaidie kusimamia masuala ya ardhi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kama nilivyosema hoja ni nyingi lakini zote tutazijibu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzipata. Ningependa nimalizie tu kwa kusema kwamba kwa moyo wa dhati kabisa napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kabisa kwa kushiriki na kuchangia kwa njia moja au nyingine katika majadiliano ya Muswada huu.

Umekuwepo msisimko mkubwa wa mjadala unaodhihirisha umuhimu wa raslimali ardhi katika maisha na maendeleo ya Watanzania. Naomba msisimko huu tuuendeleze basi katika Majimbo yetu na maeneo yetu ya uwakilishi tunapokutana na wananchi katika vikao na mikutano ya hadhara. Tuendelee kuelimishana, kuhamasishana, kutambua fursa zilizopo za kutumia ardhi yetu kutuondolea umaskini hatua

kwa hatua. Tushirikiane wote pamoja na wadau na vikundi vya wanaharakati kueneza uelewa sahihi wa sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za Ardhi zilizopo pamoja na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko katika sekta ya ardhi na makazi ni mchakato unaoendelea. Kwa karibu miaka miwili sasa tumekuwa tukiwasiliana na kushauriana na wadau wote wanaohusika na tumebaini maeneo haya na tukakubaliana kwamba tuanzie na marekebisho ya kutuwezesha kutumia raslimali zetu ardhi na fedha katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika pia kwa kuwa siyo rahisi kuziondoa kasoro zote mara moja na kwa kuwa sheria hubadilika kulingana na matakwa ya wakati husika baada ya kujaribiwa katika utekelezaji, basi haya tuliyozungumza na kukubaliana naomba tukubaliane kuanza kuyatekeleza ili mbele ya safari tukiona kwamba kuna matatizo basi tutakubaliana tena kufanya marekebisho hapa na pale ili utekelezaji uwe mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi walivyoshiriki. Natumaini kwa maelezo haya machache tutakuwa tumeelewana ili tuweze kupitisha Muswada huu na tukaanze kazi ya kuelimishana na baadaye utekelezaji na kama kuna maeneo yanayohitaji ufafanuzi mbele ya safari basi tutaweza kushirikiana tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko katika Sheria ya Ardhi wa Mwaka 2003 *(The Land (Amendment) Bill, 2003)***

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza shughuli za Kamati ya Bunge Zima, ningependa kuwajulisha kwamba Muswada huu ingawa mnauona mkubwa lakini kuna vifungu sita tu. Kwa hiyo, kwa sababu ni marekebisho yapo kwenye vifungu sita tu, kwa hiyo, tutawahoji kwa kufuata vifungu hivyo sita.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3
kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyoye)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

*Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko katika Sheria ya Ardhi wa Mwaka 2003*
*(The Land (Amendment) Bill, 2003)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na imeukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao *The Land (Amendment) Bill, 2003* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza Kuhusu Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(Optional Protocol to the Convention on Elimination of all forms of Discrimination Against Women)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ninayo heshima kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(Optional Protocol to the Convention on the Elimination of all forms of Discrimination Against Women)* ambayo inapendekezwa iridhiwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1980, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitia saini Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(Convention on the Elimination of all forms of Discrimination Against Women (CEDAW).* Nchi yetu ilisaini Mkataba huu tarehe 17 Julai,1980 na kuridhia tarehe 20 Agosti,1985. Hadi kufikia mwaka 2002 nchi 170 kati ya 191 za Umoja za Mataifa zilikwisharidhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Mkataba wa *CEDAW* ni kuondoa vitendo vyote vya ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha kuwa wanapata haki na fursa sawa ndani ya jamii. Katika kuimarisha utekelezaji wa *CEDAW,* Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika Kikao chake cha 54 mwezi Desemba, 1999 lilipitisha Azimio la Itifaki ya Nyongeza, hii inajulikana kama *Optional Protocol to the Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women.* Itifaki hii imeanza kutumika tarehe 22 Desemba, 2000 baada ya kuridhiwa na nchi kumi wanachama wa Umoja wa Mataifa. Hadi sasa nchi 59 zimesharidhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ya nyongeza inaweka utaratibu ambao wanawake watakaovunjiwa haki zao watatumia kuwasilisha malalamiko yao kwenye Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba mama wa *CEDAW* endapo watashindwa kupata haki hizo katika vyombo vingine vyote vilivyomo ndani ya nchi mwanachama. Vile vile Itifaki hii inaweka utaratibu wa kuwezesha Kamati ya *CEDAW* kufanya mawasiliano na nchi mwanachama katika kufuatilia malalamiko ya wanawake yatakayokuwa yamewasilishwa kwenye Kamati. Tanzania kwa sasa ina mjumbe katika Kamati hiyo ya *CEDAW.*

Mheshimiwa Naibu Spika, itifaki hii ya nyongeza ina ibara 21 ambazo zimejumuishwa katika vipengele vifuatavyo:-

Umewekwa utaratibu maalum ambao unawezesha wanawake ama binafsi au katika makundi yao kuwasilisha malalamiko ya ukiukaji wa haki zao katika nchi husika kwa Kamati ya *CEDAW*.

Utaratibu huu unataka mawasiliano yote baina ya walalamikaji na Kamati yafanyike kwa maandishi na kwa kumfahamu mwandishi wake, Ibara ya (2) na ya (3). Ili malalamiko hayo yaweze kukubalika hapana budi pawepo na uthibitisho kwamba vyombo vyote ndani ya nchi vimeshindwa kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo.

Aidha, katika Kamati ya *CEDAW* haitayapokea wala kuyasikiliza malalamiko ambayo yalikwishawasilishwa kwenye chombo kingine cha usuluhishi ngazi ya Kimataifa ili kuepusha udanganyifu, kuokoa muda na raslimali (Ibara ya 4). Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya kuwakilishwa lakini ni sharti liwe kwa kibali au idhini ya walalamikaji wenyewe ili kuepuka uwezekano wa kutolewa malalamiko yasiyo ya kweli (Ibara ya 7).

Mheshimiwa Naibu Spika hatua ambazo katika Ibara ya (7), (8) na (9) zimeelezwa na Kamati ya Fedha katika kushughulikia malalamiko ni kama ifuatavyo:-

Kamati inapopata malalamiko inaweza kuijulisha nchi mwanachama kuhusu malalamiko yaliyotolewa na nchi hiyo na nchi hiyo inaweza kuombwa kuchukua hatua za dharura kwanza ili kumlinda mlalamikaji dhidi ya vitendo vinavyoweza kumsababishia madhara wakati suala lake linashughulikiwa na Kamati.

Baada ya Kamati kuyachunguza malalamiko itafahamisha nchi husika kuhusu maoni na mapendekezo yake. Nchi husika inapaswa kujibu katika muda wa miezi sita. Pamoja na majibu ya nchi husika Kamati itaweza kuendelea na uchunguzi wake na kutoa taarifa zaidi kwa nchi hiyo.

Ikibidi Kamati inaweza kufanya uchunguzi zaidi kwa kutuma mjumbe au wajumbe kwenye nchi husika endapo nchi hiyo itakubali. Baada ya kufanya uchunguzi wa kutosha Kamati itapeleka mapendekezo yake kwa nchi ambayo itatoa maoni yake katika kipindi cha miezi cha sita. Utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya *CEDAW* hutatolewa taarifa katika ripoti ya nchi kuhusu utekelezaji wa Mkataba mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 kifungu cha pili cha Itifaki kinazitaka nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa ambazo zimeridhia Mkataba mama wa *CEDAW* kuridhia Itifaki hii ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhiwa kwa Itifaki hii ya nyongeza kutaleta faida zifuatazo:-

- Nchi itakuwa inatimiza wajibu wake kama Mwanachama wa Umoja wa Mataifa.
- Taifa litaongeza kasi ya kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume kufurahia maisha na ustawi bila ya ubaguzi Kitaifa au Kimataifa.
- Tanzania itathibitisha azma yake ya dhati ya kudumisha haki za binadamu na itaimarisha utekelezaji wa sheria na sera zake nyingine katika eneo hilo Kitaifa na Kimataifa.
- Inatarajiwa kwamba kupitia utaratibu huu mbinu kubwa itakayotumiwa ni ya mawasiliano na ushirikiano baina ya Kamati ya *CEDAW* na nchi inayohusika ni dhahiri kuwa Tanzania itaweza kupata taarifa zaidi za ukiukwaji wa haki za wanawake ndani ya nchi na hivyo kuiwezesha kuchukua hatua muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Itifaki hii inaelekeza katika Ibara ya 18 kuwa nchi yoyote mwanachama inaweza kupendekeza marekebisho ya Itifaki hii na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye atawasilisha mapendekezo ya marekebisho na ombi kwa nchi nyingine kuunga mkono pendekezo hilo. Endapo theluthi moja ya wanachama watakubali mapendekezo hayo taratibu za kupitisha pendekezo hilo zifanyika. Pia katika Ibara ya 19 inawezesha nchi yoyote kujitoa katika Itifaki hii kupitia Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kujitoa huko hakutaathiri ufuatiliaji wa malalamiko yatakayotolewa dhidi ya nchi mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba maoni mbalimbali yaliyotokana na makundi mbalimbali yaliyowakilisha Serikali, Waheshimiwa Wabunge, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Kimataifa na Vyombo vya Habari yanatiliwa maanani. Ni mpango wa Wizara kuendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii katika ngazi zote kuhusu Mkataba wa *CEDAW* na Itifaki hii ili utekelezaji wake hulete mafanikio yaliyokusudiwa. Hii ni pamoja na kuweka Itifaki hii katika lugha nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mkataba huu zitahitajika gharama kwa ajili ya kuelimisha jamii ikiwa ni kutafsiri kwa lugha nyepesi na kusambaza kwa walengwa kwa kutumia rasilimali ambazo zitatoka ndani na nje ya bajeti ya Serikali. Aidha, tutashirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Kijamii, Asasi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa na Wahisani.

Kwa vile tumekwisharidhia Mkataba mama wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake; na kwa vile Itifaki hii ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Mkataba mama naona hakuna kipingamizi cha Tanzania kuridhia Itifaki hii. Kwa ajili hiyo basi, nakuomba Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu sasa niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakubali Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki ya Nyongeza ya *CEDAW.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kusoma Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(Optional Protocol to the Convention on Elimination of all forms of Discrimination Against Women).*

KWA KUWA Tanzania imesaini Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu unaozingatia Heshima na Haki sawa kwa Wanaume na Wanawake;

NA KWA KUWA Azimio la Haki za Binadamu namba 217(a)(3) linatamka kwamba kila mwanadamu amezaliwa huru na anayo haki ya kuwa huru, kupewa Heshima, Usawa bila ya kuwepo tofauti yoyote ya kijinsia;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu namba 2,200(a)( 21) unazuia uonevu wowote wa kijinsia;

NA KWA KUWA majukumu ya Mkataba huu ni kutilia mkazo ukatazaji na uondoaji wa aina zote za uonevu dhidi ya wanawake katika nchi zote Wanachama;

NA KWA KUWA lengo kuu ni kuhakikisha kwamba Wanawake wanapatiwa Haki sawa za Binadamu pamoja na kuhakikisha zinafanyika juhudi za wazi ili kuzuia ukiukwaji wa haki hizi na huru wao;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii ya nyongeza na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 18 sasa linaazimia Tanzania kuridhia Itifaki ya Nyongeza Kuhusu Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake *(Optional Protocol to the Convention on Elimination of all forms of Discrimination Against Women).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA K AMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao wakati wa kufikiria Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni namba 102(2) Toleo la mwaka 2003 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo la nyongeza yoyote ile ni kuimarisha chombo husika, Kamati yangu inakubaliana na hatua hii ya Wizara na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefurahishwa na nyongeza hii ambapo madhumuni yake ni kuweka utaratibu ambao Wanawake watakaovunjiwa haki zao watatumia kuwasilisha malalamiko yao kwenye Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba mama wa *CEDAW*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutambua hali hii ni kuheshimu historia ya mwanamke ambaye kwa muda mrefu amekuwa akibaguliwa na kuikabili hali halisi ya dunia ambapo mwanamke bado anahitaji utetezi zaidi kwa maendeleo yake katika mtandao wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali kuleta Itifaki hii ya Nyongeza. Hata hivyo, inaishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wote hasa wale waishio vijijini kuhusu Itifaki na hata Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni ya Kamati ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kuridhia Itifaki hii kutokana na umuhimu wake wa Tanzania na Ulimwengu kwa ujumla.

Aidha, naipongeza Serikali kwa kuleta Itifaki hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili liweze kuridhiwa na kufanya nchi yetu kwenda sambamba na nchi zingine duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa maelezo mazuri yenye kueleweka wakati wa Kikao na Kamati yangu.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bibi Hilda Gondwe, pamoja na Wakurugenzi wa Wizara kwa ufafanuzi wa Itifaki hiyo wakati wa kujibu maswali na kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu Itifaki hii pale wajumbe wa Kamati walipohitaji ufafanuzi.

Kwa mara nyingine tena napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano katika kufikiria Itifaki hii na ninaomba niwatambue kwa kutaja majina ambao ni Mheshimiwa Sophia Simba, ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Janet Mashele, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri,

Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande na Bibi Angelina Sanga ambaye ni Katibu wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumaliza vyema mwaka 2003 na kuingia mwaka 2004 kwa ari na mori kubwa ya kufanya yale yote wananchi wanayoyategemea kutoka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza mchango wa Itifaki ya Nyongeza ya Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, napenda kulalamika kuhusu Idara yako ya *Hansard* kutotunza au kuchapisha *Hansard* kwani sisi sote tunaamini kila kitu kiko katika *Hansard.* Kwa masikitiko makubwa juzi nilikuwa natafuta *Hansard* za mwaka 1996/1997 na 1997/1998 ambazo nilizizungumzia kama Msemaji Mkuu miaka hiyo kuhusu suala lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza hakuna kitu kama hicho katika Ofisi yako. Sasa sijui ni kwa ajili yangu peke yangu au kwa wote kwa miaka hiyo na kuendelea. Sisi tunaamini *Hansard* inaweka kumbukumbu kwa ajili ya historia, utafiti na kadha wa kadha kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hakuna ni maajabu na kweli! Katika kikao chako cha Bunge la Bajeti la mwaka 1996/1997 na 1997/1998 nilitoa mchango mkubwa katika Wizara hii. Baada ya kufuatilia *Hansard* ya mambo niliyoyaomba toka Serikalini kuhusiana na sheria za manyanyaso kwa mwanamke na mtoto naambiwa kuwa *Hansard* hazikuchapishwa. Hili suala naona ni unyanyasaji na upotoshaji wa makusudi kwa watu ambao watataka kuelewa mwenendo wa Bunge letu toka kuanzishwa kwa mfumo wa Vyama vingi vya siasa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi nzima ya Upinzani naomba kuangalia baadhi ya vipengele ndani ya Mkataba huu *Article number one* inayosema kumnyima Mwanamke Haki huru na haki ya kushiriki kwenye siasa, uchumi pia shughuli nyingine za jamii na Kiserikali, naamini kabisa kuwa hata sheria za nchi yetu zinampa mwanamke haki hizo za kushiriki hasa yule wa kijijini kwa ridhaa ya kisiasa, ushabiki wa kisiasa ambapo Wanawake wengi wanapigwa na kuzuiwa kupiga kura.

Kwa mfano, ulio hai ni mama mmoja aitwaye Christina wa Kata ya Nkoma, Wilaya ya Bariadi, alipigwa na Askari nyumbani kwake mpaka mimba yake kuharibika na kulazwa hospitali mwezi mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kama tunashindwa kuhakikisha kuwa tunalinda na kuheshimu sheria zetu tulizozitunga wenyewe je, kuna umuhimu gani wa kuridhia sheria za Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Article number 5(b)* kuhusu kuwajibika kwa baba na mama, mume na mke, kuwalea na kuwaendeleza watoto, kuwajibika huku kwa malezi ni kitu kinachohusisha vitu vingi na siyo utoaji wa fedha tu. Kuna upendo wa wazazi wa pande zote mbili na mtoto akishakosa hilo matokeo yake ni kuwa mtoto wa mitaani kama tunavyowaita. Sheria yetu ya ndani kwa upande mmoja au mwingine inachangia kwenye hilo kwani inawapa akina baba nafasi ya kukataa majukumu ya kumpa mtoto haki ya kukuzwa na wazazi wawili. Kwa maana kuna fedha za matumizi anazoamuliwa atoe baba aliyekataa majukumu ni kidogo mno na hata kama zingekuwa nyingi kiasi gani, bado zisingetosha kuleta upendo kwa familia na malezi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mkataba huu unavyosema kuzuia kudhalilishwa kwa aina yoyote ile kwa mwanamke. Kutokana na ripoti ya Wanahabari Wanawake inasema kuwa mwaka 1996 wanawake 45 walidhalilishwa na kupigwa na waume zao na idadi imezidi kupanda hadi kufikia 281 mwaka 1998. Haya mambo yanatokea kutokana na mila za baadhi ya makabila zinazoona kuwa wanawake ni chombo

cha kuwatumikia wanaume zao. Sasa haya yote yanafanyika si kwa kuwa sheria hazipo katika nchi yetu, tatizo ni kuwa vyombo vilivyopewa mamlaka ya kulinda sheria bado vimelala usingizi wakati watu wanakufa.

Mfano mwingine kama takwimu zilizotolewa mwaka 2000 na ripoti ya *TAMWA* kuwa zaidi ya 90% ya wanandoa wa kike Mkoani Arusha wana makovu kutokana na ugomvi na wanaume zao. Matukio 3,242 ya wanawake hudhalilishwa yaliripotiwa na kufika Mahakamani. Je, kati ya hizo kesi ni ngapi washitakiwa walipewa adhabu au kwenda chuo cha mafunzo?

Katika Mkoa wa Kilimanjaro wanawake 290 waliuawa na waume zao na wanawake 187 walijiua kwa sababu Mahakama zilishindwa kuwalinda na kutoa haki. Wanawake wengine wanashindwa kutoa taarifa kwa kuogopa kuwa Polisi wanashirikiana na waume zao na ni marafiki au na wao wanafanya vile vile kwa wake zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunashindwa kutoa haki kwa sheria zilizopo kwa watu wetu, haki hiyo itatolewa na watu wa nje ambao kwanza wanatakiwa waombe ruksa kwa wale waliokunyima haki hiyo. Naomba kurudia ambao watu wa nje wanatakiwa kwanza waombe ruksa kwa wale waliokunyima haki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya udhalilishaji kwa wanawake siyo tu toka kwa waume zao, hata kutoka katika vyombo vilivyopewa mamlaka ya kulinda na kutunza sheria. Matukio yaliyotokea katika Wilaya ya Tarime ambayo wanawake walipigwa na kisha kuchomewa moto nyumba zao na Askari Polisi kwa amri ya Mkuu wa Wilaya kama ushahidi unavyozidi kutolewa na Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu. Sheria zipo na ni nani atachukua hatua ili kumlinda huyu mwanamke ambaye hali yake ya kipato ni ndogo mno. Kwa mtindo huu sidhani kama kuridhia Mkataba huu ni muhimu wakati tunashindwa kusimamia sheria tulizotunga wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji wanaofanyiwa watoto wa kike walio chini ya miaka 14 na bado ni wanafunzi wa shule za msingi ambapo walimu wao ndiyo wanaotumiwa na watuhumiwa kuwashawishi wanafunzi wao. Mfano, mtoto mmoja jina nalihifadhi anayesoma shule ya msingi Tuliani aliambiwa na mwalimu kwamba aende kwa mama fulani (jina nalihifadhi), mtoto kama kawaida ya watoto kuwa watiifu akaenda, alipofika kwa huyo mama, mama huyo alimkabidhi mtoto kwa baba na baba akambaka huku akimziba mdomo ili sauti isitoke na mama huyo akafungulia redio kwa sauti ya juu sana ili sauti isisikike. Baada ya hapo mengi yalitokea.

Lakini kwa kifupi wazazi walikwenda kushtaki Polisi. Mtuhumiwa aliitwa na aliporudi akaanza kuwatukana wazazi wa huyo binti na kusema hawamuwezi kwani ana fedha. Kusema kweli matukio kama hayo yanatokea sana kwa huyo mtuhumiwa na hakuna hatua inayochukuliwa mpaka sasa kwa nini? Serikali inataka kutwambia kwamba fedha zake zinafanya kazi na watoto wetu wa shule wa walalahoi. Walie tu. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri, anafahamu suala hilo.

Mhatukio mengi yamekwisha kuripotiwa Polisi na mengine kesi ziko Mahakamani. Cha kushangaza ni kuwa Daktari ameshatoa ripoti yake na sheria kuhusu hilo iko wazi ni kwenda jela kuanzia miaka 15 na kadhalika. Sasa ucheleweshaji wa kesi unaopelekea kuharibiwa kwa ushahidi na mwisho watuhumiwa wanaachiwa huru unatoka wapi kama siyo udhalilishaji na kwamba sheria na vyombo vya kuzilinda zipo. Inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Article number 9* ya Mkataba kuhusu uraia wa mwanamke na watoto wake na watoto wake ambao kwa sheria zetu za nchi pindi mwanamke anapoolewa na Mtanzania moja kwa moja raia anakuwa Mtanzania na sheria hii bado sisi kama wanawake inatunyima haki yetu ya msingi, na kama kutakuwa na nchi yoyote yenye sheria kama hizi zetu kwenye uraia maana yake pindi tukiolewa na mtu toka Taifa lingine na hasa kabila tofauti na mimi basi hata watoto hawana haki na upande wa mama kama Mkataba unavyosema *Article 9(2).* Naomba ninukuu kwa Kiingereza: *"State Parties shall grant women equality with men with respect to the nationality of their children."* Hapa kwetu nadhani inawezekana vilevile ili wanawake wasipoteze uasili wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Article number 16(b)* ya Mkataba kipengele kinahusu Haki ya mwanamke kwenye masuala yote yanayohusu kuanzia uchumba mpaka ndoa. Kama msichana kuchagua mchumba ambaye anamtaka yeye kitu ambacho hapa kwetu watu walioelimika na wanaelewa vyema, lakini wao ndiyo wanakuwa wa kwanza kuwachagulia mabinti zao au vijana wao wanaume au wanawake, kwa sababu vijana ni wasichana na wavulana. Wakati wakielewa kuwa huo ni unyanyasaji na udhalilishaji wa mwanamke. Sasa kama ni hivyo, sijui kama kweli kuridhia kwetu Mkataba huu haya niliyoyaainisha yataondoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna unyanyasaji wa utapeli, miaka mitatu hivi iliyopita tulielezwa na Vyombo vya Habari kuwa Askari toka India wakiwa na msichana aliyepewa ahadi ya kuolewa na kisha mchumba kukimbilia Tanzania walikuja kumkamata ili sheria ichukue mkondo wake. Sheria zao zilimlinda mwanamke kwenye suala hili la uchumba wa kitapeli. Kwa hapa Tanzania ni akina dada au wanawake wangapi wamekutana na hali ya namna hiyo na wahusika wasichukuliwe hatua au adhabu ya aina yoyote? Ni wengi sana! Kwa nini Serikali inakaa kimya baada ya kuridhia Mkataba huu?

Kambi ya Upinzani imependekeza kwanza tuwe na sheria zetu zinazoweza kudhibiti utapeli wa namna hiyo ambao wanaume wamekuwa wanautumia kwa maslahi yao binafsi na baadaye turidhie za Kimataifa ili kuondoa mgongano wa sheria kati ya za ndani na za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Article 16(c)* haki aliyonayo mwanaume kuvunja ndoa na mwanamke. Vilevile mwanamke anatakiwa awe na haki ya kuandika talaka yaani kuvunja ndoa pindi mwanaume anaposhinda kuishi vizuri na mke wake. Nadhani mtaniunga mkono kwa hili. Pindi mwanamke anapoomba talaka utaratibu wa Mahakama unakuwa ni mrefu na ziko kesi nyingi sana za namna hiyo Mahakamani. Lakini mwanaume hasa kwa dini ya Kiislam ni kukaa mezani na kuandika talaka tu bila ya kwenda au kufuata utaratibu wa Mahakamani wa kuzunguka na hilo linakubalika. Ni vipi kwa hili kwa upande wa mwanamke? Kwani wanawake wengi wananyanyaswa sana na kunyang'anywa vitu vyao, nguo na kadhalika, vitu vyao vipo kwa wanaume, hivyo wanaishi kwa kuomba omba tu hata nguo za kuvaa sababu kesi iko Mahakamani na Mahakama haitaki kutoa hukumu mapema ili imdhalilishe au kumkomoa mwanamke kwa sababu Mahakimu wengi ni wanaume na marafiki wa watuhumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua za kufuatwa na Kamati *CEDAW* katika kushughulikia malalamiko kama Kamati inatakiwa kutembelea nchi husika endapo tu nchi hiyo itakubali. Kambi nzima ya Upinzani ina wasiwasi kama nchi husika inashindwa kutatua hilo tatizo, hivyo kuruhusu Kamati ya *CEDAW* ni kuonyesha udhaifu wa utendaji wa nchi, kitu ambacho ni aibu na nchi yetu haiwezi kudhalilisha Mahakama zetu. Kwa hali ya kawaida mtu hawezi kuanika udhaifu wake mwenyewe kwa watu wengine. Ikibidi kufanya hivyo, basi Kamati hii ifanye kazi yake bila kuwekewa masharti kwamba iwapo Kamati inaona inafaa kuja nchini kuona hali halisi basi hakuna haja ya nchi kukubali, kwani inaweza kuwa vigumu kukubali na hivyo kumfanya mwanamke kutopata haki yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hakuna muda maalum kuwa baada ya hapo ni lazima tuwe tumeridhia Mkataba huu, Kambi ya Upinzani inaona ni bora kwanza Wizara yetu ifanye utaratibu wa kuuweka kwenye lugha ya Kiswahili na walengwa wote waelewe haki zao za ndani ya nchi na nje ya nchi. Kwa kifupi hakuna haja ya kukimbilia kuliridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya kuridhia Itifaki hii inayowalinda wanawake ili waweze kuwa na haki sawa na wanaume katika maisha yao na shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii ya pekee kuwapongeza nami wale Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote ambao kwa wiki hii nzima na wiki iliyopita tumekuwa tukiwachagua kutuwakilisha katika uwakilishi mbalimbali nje ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mteule, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuapishwa katika Bunge hili katika Mkutano huu wa 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na maelezo yangu na mimi pia naomba kuunga mkono Azimio hii kwa asilimia mia moja na ninaamini kabisa kwamba umuhimu wa kuongezwa kwa Itifaki hii katika suala zima la mahusiano ya Wanaume na Wanawake katika kutoa haki sawa ni suala la kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo msemo unaosema kwamba ili kuwa na maendeleo ni lazima kuhama na maana ya kuhama ni kutoka katika utaratibu mbovu ama utaratibu ambao siyo rasmi kwenda katika utaratibu ambao ni rasmi na wenye mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi unaona kabisa kwamba mtu yeyote anayehama hata kama anahama kwenye nyumba atatoka katika nyumba isiyo bora atakwenda kwenye nyumba ambayo ni bora na yule utakayemkuta anahama kutoka kwenye nyumba isiyo bora na anakwenda kwenye nyumba isiyo bora kabisa basi ujue kwamba huyo ana matatizo.

Kwa hiyo tunaishukuru Serikali yetu ya Tanzania kwa kuona kwamba hata sisi tunatakiwa kuhama kutoka katika utaratibu wa awali wa Itifaki iliyosainiwa mwanzo na iliyokubaliwa na kuridhiwa mwanzo na kukubali ongezeko hili, ili kuweza kuboresha suala zima la utetezi wa wanawake katika jamii ya Watanzania ikiungana na wanawake wengine wote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Itifaki tunayoiridhia leo ina lengo la kuangalia suala zima la uwakilishi wa wanawake katika mazingira ambayo wamekuwa wakiishi kila siku. Mimi nafikiri kwamba haya yote tunayoyaridhia yanahitajika hasa, lakini kama hakutakuwa na msisitizo wa utekelezaji toka tulipoanza kuiridhia Itifaki hiyo kwa miaka ile ya mwanzo na leo tunaongeza kuridhia kipengele kilichoongezeka ni lazima tujiulize nchi yetu imeshapiga hatua kiasi gani katika kuyasimamia yale yaliyopita na kuendelea kusimamia haya yanayoongezeka na tukizingatia kwamba huo wote ni utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado sheria nyingi katika nchi yetu ya Tanzania zimeendelea kumnyanyasa mwanamke na zimeshapitwa na wakati na hazijafanyiwa marekebisho. Kama kweli tunaelewa na kama kweli tunaona kwamba tunatakiwa kuingia katika suala zima la Itifaki hii hatuna budi kuzingatia umuhimu wa kuyafanyia mapitio upya ya sheria zote ambazo zinahusu mwanamke na haki sawa katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisimama katika Bunge lako na kumhoji Waziri wa Sheria na Katiba kuhusu sheria ya matunzo inayombagua mama na kumjali mtoto tu. Lakini naomba nitoe masikitiko yangu majibu niliyoyapata kwa Waziri wa Sheria na Katiba yalitatanisha na naomba kusema leo yanapingana na Itifaki hii ambayo tunairidhia. Si kweli mwanamke asiye katika ndoa anapozaa mtoto anaonekana kwamba eti yeye ni mtu asiyejiangalia na ni mtu ambaye hana mwelekeo wa utambuzi katika maamuzi. Nalikataa hilo. Je, huyo mwanaume aliyempa mtoto alikuwa ni mwangalizi katika maamuzi yake? Alikuwa ni mtu mwenye kufikiria azma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo mambo tunayotakiwa kuyaangalia na kupitia sheria zote ili kama kweli tuna haki ya kumlinda mwanamke katika mazingira yake ya kila siku. Wanawake wengi bado wamekuwa wakiishi katika mazingira yenye shida.

Itifaki inasema kwamba inataka kuwasaidia wanawake kuwa na hali ya raha, amani ili waweze kuishi maisha sawa na wanamume. Wanawake bado wanatumia teknolojia mbovu, wanatumia kuni katika kupikia na matokeo yake wanapozeeka wanazeeka wakiwa na macho mekundu, wanakosa haki katika maisha ya jamii na wanauawa kwa wingi wakisingiziwa wao ni wachawi, itifaki inasema nini katika kulinda haki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya wakulima katika maeneo ya vijijini ni wanawake wamekuwa wakitumia masaa mengi ya uzalishaji kwa dhana hafifu na teknolojia duni. Lakini leo

tunaridhia itifaki ya kumpa haki sawa mwanamke ya kufanya kazi kwa masaa sawa na wanaume, je, teknolojia hizo ambazo bado ni duni zinazomfanya mwanamke afanye kazi masaa mengi zinafanyiwa nini ili kweli tunaporidhia itifaki hii haki ya mwanamke iweze kwenda sambamba ya masaa ya kazi kama vile ilivyokuwa kwa wanamume.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ninapozungumza Wanawake wengi wako katika kazi kubwa ya uzazi, Wanawake wengi sasa hivi wako katika kazi kubwa ya kufagia, kusafisha nyumba na kuosha vyombo, wanawake wengi wako kwenye kazi kubwa ya kunyonyesha watoto kuwaogesha na kuwalea. Je, siku moja wanawake hawa wakiamua wote kuacha hizo kazi wakaacha kunyonyesha, wakaacha kufagia, wakaacha kuosha vyombo na kufanya usafi katika nyumba zao itakuwaje katika dunia hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuyatamka haya nikionyesha kabisa ni namna gani mwanamke alivyo muhimu katika maisha ya jamii yoyote. Ni namna gani uwepo wa mwanamke ni tegemeo kubwa la maisha ya binadamu.

Kwa hiyo ninashukuru na kuipongeza Serikali yetu kwa kuona umuhimu wa Azimio hili, lakini ni wakati muafaka wa Serikali kugundua na kuona kwamba ni lazima utaratibu uwekwe, wanawake wapate taarifa ya haki zao kupitia katika vyombo vinavyotakiwa na hivyo basi wazipate kwa wakati unaotakiwa na bila kunyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kichekeshe kidogo tu wafanyakazi wengi wanaoajiriwa wanapata likizo lakini hawa wanawake wanaofanya hizo kazi kwa masaa mengi hawana hata likizo hizo za kupika wala kunyonyesha wala kulea watoto lakini bado wameendelea kuishi na haki zao bado zimeendelea kufichwa katika mifuko ya watu wachache wajanja.

Mimi nafikiri kwamba ni suala la msingi la kuangalia pia ni namna gani Serikali yetu itajitahidi kuondoa ukiritimba katika vyombo vya maamuzi ya kisheria. Haina maana kama Mahakama zetu zitaendelea kuwa na urasimu mkubwa wa kusikiliza matatizo ya wanawake na kuyatolea hukumu kwa wakati unaotakiwa ninaamini kama mwenendo huu utaendelea basi kamati hiyo ya *CEDAW* itakuwa na kazi kubwa kwa sababu sasa tutahamasisha wanawake kudai haki zao mpaka *CEDAW* kwenye Kamati ambayo imeundwa. Haitakuwa ni heshima ya nchi yetu kama kweli kesi hizo zitachelewa kusikilizwa na hatimaye zitafikishwa nyingi katika kamati hiyo na wakati uwezo ndani ya nchi yetu upo na uwezo huo unasimamia Utawala Bora wa haki na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la kupata haki katika Mahakama liendane na uwezeshwaji wa Mahakama zetu kwa namna moja ama nyingine ili ziweze kufanya kazi zao ipasavyo. Bado hali ya Mahakama zetu ngazi mbalimbali ni ya kusikitisha haijajikamilisha basi tunaiomba Serikali iangalie vitendea kazi, iangalie Mahakimu na kadhalika ili kuhakikisha kwamba wanawake wanapata haki zao katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nishauri Wizara na Serikali ione uwezekano wa kuhakikisha vitengo mbalimbali vinavyojihusisha na utetezi wa haki za wanawake katika maeneo yanayohusu haki hizo za wanawake basi visiishie mijini tu. Kumekuwa na vyombo vingi sana vinavyojishughulisha na masuala ya wanawake na hasa utambuzi wa haki za wanawake lakini kama ilivyo kawaida vyombo hivyo vimejijengea umaarufu katika maeneo ya mijini na labda kwa kuzingatia matakwa ya vyombo hivyo vimekuwa vikifanya kazi katika maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi vijijini bado wana matatizo, wananyanyasika, wanasumbuka, wanateseka hawajui mahali pa kupata haki zao. Tunawashukuru wanaume wachache wengine wamekuwa wakiwasaidia wanawake hao kujua wapi wapate haki zao. Nilikuwa naomba kutoa wito kwa wanamume wote katika nchi ya Tanzania watambue kwamba uwapo wa wanawake katika mazingira yao ni muhimu sana. Haitoshi wao kuwaona wanawake kama ni vyombo vya matumizi ya kawaida ama kuwaona wanawake kama ni watendaji kazi wakubwa katika maeneo yao bila ya kuwasaidia kuwabadilishia maisha yao ya kila siku na kuwapa haki zao. Kipindi hiki sasa cha sayansi na teknolojia ni

kipindi kinachotutaka wanawake na wanamume wote tusaidiane, tuwe na haki sawa na hivyo tutajiletea maendeleo ambayo yataweza kuonekana na kuwa na mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri na katika maelezo ya Wasemaji Wakuu vipengele mbalimbali vimeainishwa na kipengele kimoja cha 15 kinasema kwamba: "Mkataba huu ama itifaki hii tunayoiridhia italetwa faida katika nchi yetu kwa sababu nchi itaongeza amani, usawa kwa wanamume na Wanawake."

Nakubaliana na hilo na ninaamini kabisa kwa juhudi zinazofanywa na Wizara yetu ya Jinsia na Maendeleo hilo likifanyiwa kazi vizuri usawa wa wanamume na wanawake katika shughuli mbalimbali utaendelea. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonyesha mfano halisi miongoni mwa Marais wengine katika ulimwengu huu kwanza kuongeza nafasi za wanawake katika majukumu mbalimbali ya kiserikali, kijamii na kadhalika. Basi tunaamini kabisa mfano huo mzuri ulioonyeshwa na Mheshimiwa Rais wetu utaendelea kuigwa vyema sio tu kwa Rais kama Kiongozi Mkuu wa nchi lakini pia hata katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo naomba kwa heshima na taadhima nipongeze sana Wizara kwa kutuletea itifaki hii, nitoe wito kwa Watanzania wote kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba itifaki hii inafanya kazi ambayo imejipangia hasa katika kuangalia hili suala zima la usawa wa wanawake na wanaume katika jamii kwa manufaa ya familia na hasa watoto wetu ambao ndio wamekuwa ni tegemeo kubwa sana la wanawake na akinababa katika familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kuniona nilikuwa nimechelewa kuomba kuchangia lakini umeniona, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwapongeze ndugu zetu Wabunge waliopata nafasi katika Mabunge yetu ya Afrika na Bunge la *SADC.* Pia nampongeza ndugu yetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais kuingia katika Bunge hili. Tatu, nawatakia wote kheri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa .........

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzunguzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo kengele sio ya kwako.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuleta itifaki hii iweze kuridhiwa. Lakini pia ningependa kusema kwamba itifaki hii ni nyongeza ya itifaki ambayo ilikuwa imeridhiwa siku za zamani.

Kwa hiyo, nilifikiria kusema kwamba si vizuri kuridhia itifaki kwa sababu ya matatizo ndani ya nchi sio sahihi. Kuridhia itifaki kama hii ya kuzuia uonevu kwa wanawake wa kila aina ni muhimu ni kama tunavyotunga sheria. Tunatunga sheria nyingi hapa si lazima ziweze kutekelezeka leo leo. Lakini inakuwa ni chombo ambacho kama linatokea jambo ambalo ni kinyume. Basi Itifaki hii inatumika kushughulikia hilo kulalamika.

Kwa hiyo, Itifaki ya kwanza iliyoridhiwa miaka ile ya 1980 na 1990 ndiyo hiyo ilikuwa inaeleza kwamba mwanamke ni kiumbe ana haki kama mtu mwingine yoyote kuishi katika dunia hii na kufurahia maisha haya ya dunia kama mtu yoyote.

Kwa hiyo, unyanyasaji dhidi ya mwanamke ni kosa kwa mwanamke na kwa mtu yoyote mwingine. Kwa hiyo, kazi ya kwanza ambayo ilifanyika katika nchi yetu tumepitisha mabadiliko ya

Katiba kwamba hakuna mtu atabaguliwa kwa namna yoyote ile kwa dini yake, kwa jinsia yake tumeingiza katika Katiba, kwa hiyo hii ni hatua kubwa katika Tanzania tumeweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumetunga na sheria nyingine kwa mfano sheria hizi za Uchaguzi. Ni kweli hatuwezi kuwa mara moja nusu kwa nusu lakini kweli tunaposema asilimia angalau 30 ya wanawake waweze kuingia katika maeneo mbalimbali ya uamuzi nayo pia ni hatua ya kujaribu kukwepa malalamiko haya ya kuona kama mwanamke ni kiumbe tunaweza kusema ni mwananchi wa daraja la tatu au la ngapi, kwa hiyo wanatakiwa akinamama pia washiriki katika maamuzi mbalimbali ndani ya nchi yao pamoja na ndani ya Bunge.

Halafu eneo lingine ambalo Serikali yetu imeweza kutekelezapia ni katika kuingia shule za msingi. Sasa hivi watoto wa kike na wa kiume wote wanaingia sawa sawa. Tumeingia katika eneo la Sekondari ni nusu kwa nusu watoto wanachaguliwa kwenda Kidato cha Kwanza. Hii ni hatua mojawapo ambayo inaelekea katika utekelezaji wa hili Azimio mama.

Kwa hiyo, ukisema kwamba kwa nini tunatakiwa kuridhia kwa sababu kuna matatizo, hiyo sio sahihi. Kwa sababu kuna vitu fulani vinaweza kutendeka kwa uhakika kwa sababu tuna sheria hii. Sasa hii nyongeza inayokuja sasa tunayoridhia leo ni nyongeza ya ile itifaki ya mwanzo. Sasa kwa Itifaki hii inafika kuna nchi wanaweza mtu akateseka, akaenda kwenye Mahakama wala wasimwonee huruma, wakaenda, kwa mfano tunayo kesi ya yule mama ambaye alipata mtoto nje ya ndoa Nigeria kule akatakiwa kuuawa. Kwa mujibu wa sheria ilikuwa amehukumiwa kuuawa.

Kwa hiyo, ulimwengu umeweza kuandika maandiko mpaka kule Umoja wa Mataifa, dunia nzima ikamtetea yule mwanamke kwa sababu ya vitu kama hivyo. Kwa hiyo, yanatokea katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kesi nyingine, ziko nyingi. Kwa mfano hapa kwetu ndio kuna matatizo mengi ambayo yapo. Sasa kwa mujibu wa sheria hii ni kwamba binadamu unajua kabisa hili ni kosa. Kuna watu wanaweza kujivunia kwamba kumpiga mwanamke ndiyo kumpenda, huu ni uongo.

Sasa watu wanajaribu kutumia udhaifu wetu sisi wanasema kumpiga mwanamke ndiyo maana yake unampenda zaidi ama anasema mwanamke mwenyewe anauliza kwa nini sijapigwa. Huu ni uongo kamili watu wanatafuta utaratibu tu wa kujitetea. Kwa mujibu wa itifaki kama hii ni uonevu kabisa na haya ni maneno ya mtu fulani mwenye tabia hiyo anasema mimi mke wangu eti asipopigwa eti hapendwi. Hata mtoto mdogo analalamika kupigwa. Hizi ni tabia ambazo ni za uongo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa itifaki hii kitu kinachotakiwa kufanyika na Wizara yetu sasa miaka ya 1980 mwamko ulikuwa mdogo, miaka hii sasa ya 2000 mwamko ni mkubwa kuhusu haki za akinamama.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa lazima tuweke hii itifaki katika lugha inayoeleweka kusudi watu wengi waweze kuielewa hasa akinamama vijijini. Sio akinamama tu na akinababa vijijini kwa sababu saa nyingine kama wanaodai kwamba ni kumpiga mwanamke ni haki yao au kama mwanamke hapendwi ni kutokuelewa. Kwa hiyo, tuweke katika lugha nyepesi ambayo wananchi wa kawaida wote wanaume na wanawake waweze kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo moja ambalo tunafanya sisi akinamama, tunafikiri ukombozi wa mwanamke utaletwa na wanawake peke yetu ni lazima na wanaume waelimishwe waweze kuona kwamba mwanamke au mke wake ni sehemu yake ni *partner* ni mwenzake, bila mwanamke huwezi kufanikiwa. Hili limejitokeza wala sio siri, sipendi kuwatia watu uchungu watu ambao wamefiwa na wake zao. Kuna watu ambao wamefiwa na wake zao wamekaa peke yao imekuwa matatizo kweli. Huwezi kuona thamani ya mwanamke mpaka ufiwe naye.

Kwa hiyo, ni vizuri kama ni chombo bora kama unavyokiona wakati umekosa basi kiheshimu ukipende. Maana kama mke wako unambamiza bamiza na huku unasema mke wangu mtu wa maana kwa kweli hiyo si sahihi. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ni lazima tuwafundishe watu wote kumwona mwanamke ni kama chombo chenye maana ambapo bila mwanamke huwezi kufanikiwa. Kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge mko wote hapa

mnajua nyumbani kuna mama anatunza watoto. Wewe hapo usingeweza kuwa Bungeni sasa hivi kama mama yule asingeendelea kutunza watoto wako.

Kwa hiyo, ni mtu ambaye lazima tuelimishe kila mtu amwone mama kama ni mama yake na mke kama ni mama yake, mtoto ni mama, shangazi yako ni mama. Kwa hiyo, huwezi kusema mama yako mzazi ni mzuri lakini mke wako sio. Haiwezekani. Kwa hiyo, tunataka tujenge mazingira kwamba tunapozungumzia mwanamke maana yake mwanao, binti yako, mke wako, shangazi yako, dada yako ndio hao wanawake tunaozungumza. Kwa hiyo, kama katika nyumba mtaona hawa ni watu wa maana basi sheria hii inawasaidia kuelewa kwamba waheshimuni hawa ni ndugu zenu. *(Makofi)*

Halafu kuna wenzetu wanaharakati, kuna wachache wameanza kuwa na vile vitengo vya kuwasaidia akinamama katika mambo ya sheria, Mahakamani wanatoa uwakili. Tunaomba hii Wizara ilisimamie pale kwa sababu Wizara yenyewe haiwezi kuwa kama wakili kwa ajili ya matatizo mbalimbali ya akinamama katika Mahakama. Lakini itafute utaratibu wa kuweza kuwawezesha hawa wachache wanaharakati waweze kutusaidia katika kuwa Mawakili kwa kesi mbalimbali zinazowahusu akinamama Mahakamani hasa kesi za mirathi, kesi za kunyang'anywa mali. Asubuhi sikupata nafasi kuzungumza kwenye suala hili la sheria hii tuliyopitisha sasa hivi ya ardhi watakaoteseka sana katika sheria tuliyoipitisha ni akinamama. Kwa sababu wanawake si wengi wanaweza kwenda kukopa mikopo, hata namna ya kwenda kukopa mikopo hawajui. Lakini kuna mali zilizopatikana kwa wote kwa ujumla watanyang'anywa. Sisemi kwamba itatokea, imeshatokea sasa itatokea sasa hivi.

Kwa hiyo, ni wakati muafaka wale wanaharakati hasa Wanasheria wawasimamie akinamama katika kesi za namna hii. Kwa sababu kutakuwa na kesi mwanamke atabaki mnyonge utakwenda kwa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mbunge nimeonewa hivi wewe utasaidia lakini hutafika mbele ya sheria unatakiwa upitie kwenye sheria. Kwa hiyo, ni muhimu sana wenzetu wanaharakati hasa Wanasheria wajiweke pamoja waweze kutetea akinamama hasa vijijini.

Wakati Waziri wa Sheria alikuwa Mheshimiwa Samwel Sitta na mimi nilikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii tulikuwa tumeunda vituo vya ushauri wa akinamama katika kanda mbalimbali. Hii ilikuwa ni rahisi kwamba wanawake wa kule kijijini wanaweza kufika katika maeneo ya kanda hizo kuliko wote kuja Dar es Salaam au kuja katika miji mikubwa wakapata ushauri wa kisheria na hata kusaidiwa katika mambo ya kesi zao.

Mimi sina hakika zile kanda ziliundwa kweli ama zilififia baada ya Waziri mhusika alipoondoka. Ni mradi ambao ulifadhiliwa vizuri sana na ukawa uenee katika kanda nadhani kama nane katika nchi, lakini sasa sijui kama zipo zile kanda. Kwa sababu kama hazipo ni bahati mbaya kweli matatizo yapo makubwa sana vijijini. Wanawake wanaonewa wananyang'anywa mali zao, mali za familia lakini hakuna wa kuwatetea. Bahati mbaya wakati mwingine naomba niseme hivyo. Mahakimu wengi ni akinababa wakimkuta bwana mmoja ambaye ni mwanaume amekwenda kwenye kesi wako tayari kusimama na mwanaume mwenzao na kumgandamiza mwanamke, ninazo hizo kesi. Ninazo kesi kabisa mimi mwenyewe. Kwa hiyo, kama kungetokea Wanasheria wanaosimamia kesi basi unapogandamiza a unatukanwa. Wakati mwingine wanatukanwa matusi Mahakamani mpaka unashangaa hivi kwa nini Hakimu akamtukane mtu aliyekuja kwenye matatizo. Kama hana sheria si amwambie huna sheria tu. Lakini anafika na kutukana matusi na kusema wewe mwanamke ulitafuta hiyo mali wapi, wewe una uwezo wa kutafuta mali si unapika tu jikoni. Sasa vitu kama hivyo kweli vinaudhi na ndiyo maana nilikuwa naomba kwa mujibu wa itifaki ya *CEDAW* tungetafuta utaratibu wa kupata Mawakili wengi zaidi. Wapo najua akina *TAWLA, SUWATA* wanasaidia lakini tungepata wengi zaidi wanaweza kwenda mpaka vijijini. Kule kuna maonevu, watu wanakufa kinyongo tu hivi hivi kwa kuonewa. Lakini pia na elimu ya juu ya *CEDAW* yenyewe haijafika vijijini kwa usahihi.

Kwa hiyo, ni vizuri basi Wizara yetu kwa kupitia mtandao wa Serikali tukajaribu kupeleka elimu kule vijijini badala ya Maendeleo ya Jamii ya kawaida, lakini pia na haki za mwanamke ambazo ni haki za binadamu zikaelimishwa kule vijijini watu wakaelewa kwa utulivu tu. Tusiwaelimishe wanawake kuhusu haki zao ikawa sababu ya ugomvi ndani ya nyumba. Kipindi hiki ni kipindi cha kumfanya mtu aelewe kwamba hivi ninavyotenda mimi kwa huyu binadamu mwenzangu mbona sio sahihi. Waelewe watabadilika kuliko tukienda kwa nguvu na sisi kusema lazima tunadai hiyo nayo haisaidii. Tunaweza

kuwabadilisha wenzetu akinababa na wanawake wengine kwa kuwaelimisha kwa uzuri, faida na hasara ambazo zinapatikana kwa kutotenda haki kwa mwanamke mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nawashukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba niipongeze Wizara kwa kuleta itifaki hii ila kazi zaidi inahitajika na naunga mkono itifaki. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wanne hao waliochangia hoja ya leo hii. Kwanza naomba nifanye sahihisho dogo, nilipokuwa nasoma hapa itifaki nilitamka kwamba ni Mkutano wa 18. Lakini naomba nisahihishe ni Mkutano wa 14 na sio Mkutano wa 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao wa ukaribu sana. Kwa kweli tunasaidiana katika shughuli hizi za kumkomboa mwanamke. Pia naomba kuwashukuru wataalamu wangu akiwemo Katibu Mkuu ndugu Hilda Gondwe pamoja na ugeni wake katika Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii anatusaidia sana akisaidiana na timu yake na kwa taarifa yenu leo yupo hapa hapa anataka ahakikishe kwamba itifaki hii inapitishwa na Waheshimiwa Wabunge. Mimi naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge na pia ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ushindi wa kishindo alioupata kutuwakilisha sisi katika Bunge la *SADC.* Namshukuru sana na namtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani. Yeye ametoa mawazo ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa niaba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Sophia Simba. Pia tumepata mawazo ya Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, naye ametoa mawazo yake. Pia nimshukuru sana tena sana Mama Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini kwa ufafanuzi alioutoa nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kuishukuru Kamati kwa kuona umuhimu wa itifaki hii na kukubaliana na maelezo ya Wizara kuhusu malengo na madhumuni ya itifaki hii ya nyongeza na kwamba lengo ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji mkataba mama wa *CEDAW* ambao nchi imeuridhia na madhumuni ni kuhakikisha upatikanaji wa haki za wanawake. Napenda kuishukuru Kamati kwa ushauri uliotolewa kwa Serikali kwamba elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi. Mimi ninaafikiana na hilo kwa sababu hata Mheshimiwa Mama Anne Makinda amezungumzia hilo hilo kwamba kuna haja ya kutoa elimu hii ya *CEDAW* sio tu kwa sisi Wabunge bali pia kwa akinamama na akinababa waliopo pale vijijini.

Mimi naomba nitoe ahadi hapa kwamba tutaweze in near future kuandika itifaki hii pamoja na mkataba mama katika lugha nyepesi kama ilivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini naomba pia niseme kwamba kazi hii tumeanza kwa sababu leo kila Mheshimiwa Mbunge hapa tumemgawia Sera ya Maendeleo ya wanawake na jinsia katika lugha nyepesi. Kwa hiyo, tumeanza kazi na tutaendelea. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kwa mawazo yake ni mazuri, lakini namwomba sana aelekeze majadiliano yake katika Itifaki hii ya Nyongeza kwa sababu tusipendelee malumbano ya kisiasa. Sisi hapa tumeleta Itifaki ya Nyongeza na Itifaki hii tumeileta kwa unyenyekevu ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kuridhia kwa sababu Mkataba Mama tayari Bunge hili hili liliridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, pamoja na kwamba umezungumzia kwa uchungu masuala mengi, lakini bado nakusihi kwamba tuelekeze majadiliano yetu kwenye Itifaki hii. Itifaki hii zaidi inalenga kwenye utekelezaji, maana kuna kuunda Kamati ya Kimataifa. Kwa bahati nzuri katika Kamati hiyo leo hii tunajivunia kwamba yupo Mtanzania mwenzetu pale New York kwa jina anaitwa.....

**MBUNGE FULANI:** Anaitwa Christina Kapalata.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Enhee, Mtanzania huyo anaitwa Ndugu Christina Kapalata. Waheshimiwa Wabunge, tukiridhia Mkataba huu haya yote yaliyozungumzwa, ya unyanyasaji, ya ubakaji, mambo yote haya yataweza kupungua kwani wengi tutaelekeza maoni yetu katika Kamati hii ya *CEDAW* iwapo vyombo vyote vya hapa nchini vimeshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeulizwa hapa kwamba tangu kupitisha Mkataba huu Mama ni mambo gani yamefanyika? Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi kwamba mwaka 1995 tulikuwa na Mawaziri wanawake watatu, lakini leo hii mwaka 2004 Mawaziri wanawake wako wanne, Naibu Mawaziri walikuwa watatu mwaka huo wa 1995, lakini leo hii wako watano. Wabunge wanawake tulikuwa 48, lakini leo hii nafurahi kusema kwamba tuko 62. Sasa ni hatua kubwa tuliyopiga, lakini bado najua tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Kwa upande wa watoto, Idara mpya ya Watoto imeundwa, maana hatukuwa na Idara ya Watoto pale Wizarani, lakini leo hii tuna Idara ya Watoto. Kwa upande wa watoto, Baraza la Watoto Tanzania limeundwa mwaka 2002. Watoto 13 walishiriki Mkutano Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watoto uliofanyika New York ,Marekani mwaka 2002. Lakini pia, ninyi wenyewe hapa mlikubali kubadilisha jina la Wizara yetu. Wizara yetu sasa inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika hali ile ile ya kuleta usawa kwa wanawake na wanaume. *(Makofi)*

Kuna kipengele katika Itifaki hii kinachosema kwamba: "Iwapo nchi itakubali ndipo wale wataruhusiwa kuingia hapa Tanzania." Ni kweli kwa sababu hawawezi kuingia katika nchi ya wenzao kiholela, ni lazima kwanza walete barua na tukubali ili tuanze kuandaa *Immigration Procedures* kwa sababu wale ni wageni na watapenda kufika hapa Tanzania. Hilo la kwanza. Lakini pili, ni kutoa ushirikiano wakati wa uchunguzi kwa mfano kutoa visa na ruhusa ya vyombo mbalimbali kuhojiwa maana nia yao itakuwa kufika hapa na kuhoji baadhi ya watu au vikundi. Sasa bila kutuletea taarifa hizo hawawezi kuingia kichwa kichwa, ni lazima waje hapa kwa utaratibu ambao tumeupanga sisi. Mambo mengi hapa yamezungumzwa. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Anne Makinda, ametoa ufafanuzi mzuri tu kwamba ni kwa nini turidhie Itifaki hii ya Nyongeza. Itifaki yenyewe ni ya nyongeza, kama Mkataba Mama tuliweza kuridhia, kwa nini itifaki hii tushindwe?

Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu amezungumzia kwa uchungu sana masuala mengi tu ya wanawake kudhalilishwa, masuala ya kesi, masuala ya ubakaji na amenitaja mimi kwamba kuna kesi moja naifahamu. Ni kweli, huyo mama ambaye alitokea Turiani alifika hapa majuzi na alimlalamikia mtuhumiwa kwa sababu leo hii huwezi kusema kwamba yule kweli amebaka, yeye bado ni mtuhumiwa. Kwa hiyo, amemlalamikia mtuhumiwa na ninafurahi kusema kwamba baada ya kupata maelezo ya yule mama niliwasiliana na *RPC* wa Morogoro, Ndugu Shekiondo kwamba, ahakikishe huyo mtuhumiwa anafikishwa Mahakamani. Baada ya kuwasiliana kwa njia ya simu pia niliandika barua na pia nimemshauri atuletee taarifa kamili ya kesi hiyo. Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, yule mama aliyefika hapa kwanza nashukuru ulianza kumpokea wewe maana yeye ndiyo alianza kumpokea ndipo akaniletea mimi na mimi ndiyo nilifanya kazi hiyo. Kwa hiyo, naomba tusubiri kwa sababu hatuwezi kuingilia mahakama, jibu tukipewa tutakuletea hapa au tutaliletea Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mengi yaliyotolewa hapa ni ushauri, Mheshimiwa Jenista Mhagama naye ametoa ushauri, nashukuru sana kwa ushauri wako na napenda kusema tu kwamba ushauri huo umepokelewa na tutasaidiana ili tuweze kuondoa ukandamizaji na mambo yote ya uonevu hususan kwa upande wa akina mama, lakini naomba kuwakumbusha wanaume kwamba tuwe pamoja katika vita hivi. Ahsante sana. Baada ya hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza Kuhusu Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pengine ni suala la ufafanuzi tu kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge.

Wakati Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, anachangia alisema kuhusu masuala ya *record* za vikao vyetu hivi vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnafahamu, *record* zote zinaandikwa. Wabunge wakicheka inaandikwa wamecheka, wakipiga makofi inaandikwa wamepiga makofi, wote mnafahamu. Sasa kilichotokea kwa hili la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, alikwenda Idara ya *Hansard* kutaka apate yale aliyozungumza mwaka 1996. Kiongozi wa *Hansard* alimweleza kwamba: "Basi uje baada ya nusu saa tutakupatia."

Sasa, Kiongozi wa *Hansard* anasema: "Sikumwona tena kuja, nadhani ana shughuli nyingi." Kwa hiyo, hakwenda angeweza kumpatia. Lakini alilolisema lingine ni kuhusu uchapishaji. Wakati huo wa mwaka 1996 *Hansard* zote zilikuwa zinachapwa na *Government Printer.* Sasa ni masuala ya *Government Printer.* Lakini *record* zote zipo pale maktaba na kule Idara ya *Hansard,* akitaka saa yoyote atazipata. Kwa kweli, angekuwa na nia ya kurudi angezipata zote. *(Makofi)*

Baada ya kuona utaratibu wa *Government Printer* pengine unatucheleweshа wakati mwingine, ndiyo maana sasa kila siku inatolewa *Hansard* na kila Mbunge anapata *copy* yake wakati tunasubiri hizo maalum zinazochapwa sasa na Idara ya *Hansard,* lakini kila siku inatolewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, narudia tena kama angekwenda kwenye Idara ya *Hansard* kama nia ilikuwa akumbushwe yale aliyosema mwaka 1996, angeweza kuyapata yote kabisa. Nadhani hilo analielewa, basi tu pengine ni hamasa tu ya uongeaji. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.11 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano*
*Tarehe 11 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*